Jumanne Oktoba 8, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580043
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Asimulia alivyonusurika kuuawa na simba njiani akienda shambani

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wambura, Tenga wa kwanza msamaha JPM

• **Wakamilisha** taratibu na kuachiwa, meneja TRA akiri kutakatisha mil. 120/-, zaidi wakubali yaishe... *Endelea ukurasa 2*



Aliyekuwa Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, akipongezana na ndugu zake baada ya kuachiliwa huru katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**CHADEMA YAMJIBU MSAJILI WA VYAMA**
CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimemjibu Msajili wa Vyama vya Siasa ikiwa ni siku moja kabla ya muda kiliotakiwa kujieleza kumalizika...

UKURASA WA 4
**KATA 18 ZAUNGA MKONO MAANDAMANO MAKONDA**
WANANCHI wa kata 18 zilizoko kando-kando ya Mto Msimbazi, wamesema wanamuunga mkono Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kwa...

UKURASA WA 8
**WB YAIMWAGIA TRIL. 1.03/- TASAF**
BENKI ya Dunia imetoa mkopo wa masharti nafuu wa Sh. trilioni 1.035 kwa serikali ya Tanzania kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa mradi wa kipindi cha...

## Magufuli awatolea uvivu mafataki

UKURASA 3

## TPA yaanika ‘upigaji’ wa magari mipakani

UKURASA 2

**MICHEZO** MCHENGA YANUKIA UBINGWA BBALL KINGS UK.31 | MAONI, KATUNI UK.6

# TPA yaanika 'upigaji' wa magari mipakani

Na Salome Kitomari

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA), imeeleza jinsi ilivyonusuru gari aina ya Benz iliyokuwa ikimilikiwa na raia wa Congo kupigwa mnada baada ya kubainika dhuluma inayodaiwa kufanywa na watendaji wa bandari hiyo kwa kushirikiana na taasisi zingine za umma.

Hali kama hiyo ilisababisha wateja wengi waliokuwa wanaitumia bandari hiyo kupitisha magari yao kuikimbia na kuikosesha serikali mapato baada ya idadi ya magari yaliyokuwa yapitia nchini kuporomoka.

Akizungumza na wahariri na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko, alisema shehena ya magari inayopitia Bandari ya Dar es Salaam iliporomoka kiasi cha kumfanya kwenda kufanya uchunguzi.

Alisema mwaka 2014/15 magari 164,000 yalikuwa yakiingia nchini, mwaka 2015/16 yalishuka hadi 127,335 na mwaka 2016/17 yaliporomoka na kufikia 93,471.

"Mporomoko huo ulikuwa kilio cha kusaga meno, niliondoka kwenda kufanya kampeni za wafanyabiashara wa magari mimi binafsi, nilikwenda Lubumbashi nchini Congo, nilisikitika sana huduma zetu zilikuwa za ovyo sana," alisema na kuongeza:

"Nilikuta tunapiga mnada magari ya watu, mama mmoja nilimkuta anatokwa na machozi, alinunua benzi lake anataka kulipa kila kitu amekataliwa, watu wetu wameamua gari lipigwe mnada, walihakikisha hatafanikiwa kulitoa ndani ya muda."

Kakoko alisema, gari hilo, lilikuwa limeingizwa kwenye orodha ya mnada kutokana na mazingira yaliyojengeka kuhakikisha mteja huyo hafanikiwi kulitoa kutokana na gharama kubwa kiasi cha kushindwa kuzimudu.

"Wiki hiyo ilikuwa bahati nilikuwapo eneo la tukio, nililitoa kwenye mnada, lakini ilikuwa ni vita kubwa kidogo na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)," alisema na kuongeza:

INAENDELEA UK 26



Wananchi wa Jiji la Mbeya, wakiangalia daraja linalounganisha Kata za Mwasanga na Mwakibete, baada ya kubomoka kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha jijini humo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wambura wa kwanza msamaha wa JPM

Na Beatrice Shayo

ALIYEKUWA Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, ameachiliwa huru katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya kukiri mashtaka yake na kutakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 100.9 kwa awamu tano hadi Septemba 30, 2020.

Wambura alifikishwa kwa mara ya kwanza mahakamani hapo, Februari 11, mwaka huu, akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka 17 yakiwamo ya kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 100.

Awali, kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa hawana rekodi yoyote ya mshtakiwa huyo kufanya makosa ya jinai kipindi cha nyuma, hivyo ameiomba mahakama impe adhabu ili iwe fundisho kwa wengine.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Kelvin Mhina, alimtaka mshtakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 100.9 na kutofanya kosa la jinai katika kipindi cha miezi 12.

Mhina alisema kuwa mshtakiwa huyo ataanza kulipa fidia hiyo kuanzia jana (Oktoba 7), Novemba 31, 2019, Machi 31, 2020, Juni 30, 2020 na Septemba 30, 2020.

Hakimu alisema kwa jana mshtakiwa alitakiwa kulipa Sh. milioni 20 na tarehe nyingine alizopangiwa atatakiwa kulipa kiasi cha Sh. milioni 20.24.

Awali, mahakama hiyo ilimfutia shtaka la utakatishaji fedha na kubakiwa na shtaka la kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu.

Akisomewa maelezo ya awali, alidaiwa kuwa Desemba 20, 2004 akiwa makamu wa TFF walikubaliana na kampuni ya Jeck System, kuingia mkopo wa USD 30,000 kwa ajili ya michuano ya Chalenji na kusaini mkataba huo.

Mshtakiwa alitakiwa kurejesha fedha hizo na asilimia tano baada ya mashindano kuisha.

Mwaka 2014 kampuni ya Jeck System ilimwandikia barua Wambura na aliilaghai TFF kwa kujaribu kujionyesha kuwa yeye alichaguliwa na alipewa mamlaka kisheria ya kukusanya zaidi ya Sh. milioni 100 akijaribu kusema ameruhusiwa na kampuni hiyo wakati sio kweli.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, mshtakiwa alikiri kosa lake.

INAENDELEA UK 26

## Chadema yamjibu msajili wa vyama

Na Mary Geofrey

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimemjibu Msajili wa Vyama vya Siasa ikiwa ni siku moja kabla ya muda kiliotakiwa kujieleza kumalizika.

Barua hiyo yenye Kumb. Na. C/HQ/ADM MSJ/18/04/58, kurasa 13 na viambatanisho saba, inaeleza kuwa hitimisho la uchaguzi huo ni Desemba, mwaka huu, tarehe ambayo itaamua kama Freeman Mbowe ataendelea kuwa mwenyekiti wa chama hicho, nafasi aliyoishika tangu mwaka 2004.

Kwa mujibu wa katiba ya Chadema, Ibara ya 6.3.2(a) inataka kila kiongozi kukaa madarakani kwa muda wa miaka mitano.

Taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Idara ya Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene, ilieleza kuwa iliwasilishwa ofisi ya msajili jijini Dodoma na kupokewa saa 2:13 asubuhi.

"Kupitia barua hiyo, Chadema imemthibitishia Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa chama kinaendelea kutekeleza shughuli zake, ikiwa ni pamoja na uchaguzi mkuu wa ndani kwa kuzingatia taratibu za kisheria, Katiba ya Chama na Kanuni za Uendeshaji wa Chama," alisema Makene.

Alisema viambatanisho saba vilivyowasilishwa na barua hiyo ni sehemu ya muhtasari na orodha ya mahudhurio yenye saini za wajumbe kwa kikao cha Julai 27 na 28, mwaka huu.

Makene alisema katika barua hiyo, Chadema imesisitiza inavyoendesha shughuli zake kwa kuzingatia misingi na taratibu za sheria za nchi, katiba ya chama ya mwaka 2006, toleo la mwaka 2016 na kanuni za uendeshaji wa chama.

Alisema kwa muktadha wa barua hiyo ya Msajili wa Vyama vya Siasa, suala la uchaguzi mkuu wa ndani ya chama unaendelea na utahitimishwa Desemba, mwaka huu kama ilivyoazimiwa na Kamati Kuu ya Chama kwa kutumia ibara ya Katiba, 6.3.3(a).

"Tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Chama inaweza kurekebishwa kwa kusogezwa mbele kwa muda usiozidi mwaka mmoja toka mwisho wa uhalali wa uongozi uliopo. Mamlaka ya kufanya marekebisho hayo yameachwa kwa Kamati Kuu," alisema Makene katika taarifa hiyo.

Alisema barua hiyo imeeleza sababu mbili ambazo Kamati Kuu ilizingatia kutumia mamlaka yake ya Kikatiba kufanya uamuzi huo kuwa ni vikao vya ndani vya uchaguzi wa ndani ya chama kuingiliwa na kuzuiwa na Jeshi

INAENDELEA UK 26

## HABARI KITAIFA

# Asimulia alivyonusurika kuuawa na simba 3 akienda shambani

**Na Stevie Chindiye, NAMTUMBO**

MKAZI wa Kijiji cha Matependwe, Namtumbo mkoani Ruvuma, Tile Bashiru, ameelezea alivyonusurika kuuawa na kuliwa na simba watatu.

Bashiru alinusurika katika mkasa huo mwishoni mwa wiki alipokuwa njiani kwenda shambani.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki baada ya Tile Bashiru kuzingirwa na simba hao akiwa juu ya mti ambao alipanda kwa nia ya kujinusuru kukamatwa.

Akizungumzia tukio hilo, manusura huyo alisema akiwa njiani kwenda shambani kwake, aliwaona simba wakiwa mbele yake takriban umbali wa takribani mita 40, huku macho ya simba hao yakielekea kwake.

Bashiru alisema alipojaribu kukimbia, nao walianza kumkimbiza na ndipo akili ikamtuma hawezi kufika kokote, hivyo kulazimika kuuparamia mti na kukwea juu.

Alisema baada ya kupanda juu ya mti, simba hao walifika katika mti huo huku yeye akiwa juu ya mti na kubaki wakimtazama na kuzunguka zunguka chini hali iliyomlazimu kupiga yowe kuomba msaada kutoka kwa wananchi.

Baada ya kelele hizo, alisema umati wa wananchi ulikusanyika na kwenda katika eneo la tukio kitendo kilichowafanya simba hao kuogopa na kukimbilia msituni, hatua iliyotoa nafasi kwa Bashiru kushuka katika mti na kurudi nyumbani akiwa salama.

Kaimu Mtendaji wa Kata ya Msisima, Saidi Geho, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuongeza tukio lingine la simba kuua ng'ombe watatu wa mfugaji aliyefahamika kwa jina la Lwende Msukuma.

Kutokana na tukio hilo, Ofisa Ardhi na Maliasili wa Wilaya ya Tunduru, Simon Sambalu na Ofisa Wanyamapori, Ernest Nombo, wamepiga kambi katika kijiji hicho wakiwa na askari wa wanyamapori kuwadhibiti simba hao ili wasilete maafa kwa binadamu na mifugo.

Sambalu alisema askari hao wa wanyamapori wanawasaka simba hao kwa lengo la kuwaondoa katika makazi ya watu na askari hao wataendelea kubaki katika maeneo ya kijiji hicho mpaka amani na utulivu itakaporejea kama awali.

Ofisa Mtendaji wa Mji Mdogo wa Lusewa, Estery Mwinuka, aliwataka wananchi wa Matepwende kutulia na kushirikiana na askari wa wanyamapori waliopo katika kijiji hicho ili kuwadhibiti simba.

Matukio ya wanyamapori katika Wilaya ya Namtumbo yanazidi kuongezeka hasa katika vijiji vinavyopakana na pori la akiba la Selous na mapori mengine yenye unasaba na Selous.



# JPM awatolea uvivu 'mafataki'

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameshtushwa na idadi kubwa ya matukio ya wanafunzi kupata mimba mkoani Rukwa, hivyo kuwataka wakazi wa mkoa huo kuacha tabia hiyo na kutafuta watu walioshamaliza shule.

Amesema kwa mwaka jana pekee, wanafunzi waliopata mimba mkoani humo walikuwa 229, hali inayohatarisha mpango wa serikali wa kutoa elimu bure.

Rais aliyasema hayo jana akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Rukwa alipohutubia wananchi mkutano wa hadhara katika Uwanja wa Nelson Mandela baada ya kuzindia mradi wa maji safi uliogharimu Sh. bilioni 35. Mradi huo utakuwa na uwezo wa kusambaza maji lita milioni 20.5 kwa siku.

"Kwa takwimu nilizo nazo, Rukwa ni miongo mwa mikoa inayowapa wanafunzi ujauzito. Nimeambiwa kwa mwaka jana tu wanafunzi 229 walipata ujauzito. Tumeeleza tumekuwa ukitoa fedha kwa ajili ya elimu bure kwa watoto wetu ninyi mnatoa mimba bure sasa tutakuwa tunatoa hela kumbe tunapata hasara," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Ninajua mnakula vyakula vyenye nguvu, mkatafute ambao wamemaliza muda wao. Msiwaonee hawa wanafunzi na nyie watoto muache viherehere mtayakuta tu baadaye. Kwa hiyo hili ni lazima tulisimamie na nyie wazazi tuwafundishe watoto wetu yaani unamwona kila siku anaenda kusoma hata daftari hana na unamwacha tu."

Kutokana na idadi hiyo, Rais Magufuli aliwataka viongozi wa mkoa huo kuzingatia sheria kwa wote wanaohusika na vitendo hivyo.

"Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, vyombo vya dola zingatieni sheria, vinginevyo tutakuwa tunafanya kazi bure. Watendaji wa kata, madiwani na vijiji simamieni hili kwa maana hawa watoto ndio wabunge na mawaziri wa kesho" alisema.

"Hawa ni watoto maskini tusiwarubuni kwa kuwa ni malaika na vyombo vya dola muanze kuwashughulikia hawa watu wanaowapa mimba kwani sheria inajulikana

INAENDELEA UK 26


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TRA

# TAARIFA KWA UMMA

Mnamo tarehe 14 Juni, 2018, Waziri wa Fedha na Mipango alitangaza msamaha maalum wa riba na adhabu kwa Walipakodi wenye malimbikizo ya madeni, na wale ambao wako tayari kuweka wazi madeni ya nyuma kwa hiari yao wenyewe na kulipa kodi ya msingi kwa utaratibu ulioanishwa katika (Amri Na. 282A ya Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018.

Mpango maalum wa msamaha wa riba na adhabu ni fursa maalumu ya muda mfupi iliyotolewa. Utaratibu huu ulianza 01 Julai, 2018 hadi Juni 30, 2019 na ilihusisha malimbikizo ya madeni ya kodi yaliyokuwepo.

Hata hivyo, Serikali kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu), (Nyongeza ya muda wa kulipa)2019 , iliongeza muda wa malipo ya kodi ya msingi kufikia tarehe 31 Disemba 2019 kwa walipakodi ambao;

a) waliomba msamaha wa riba na adhabu za kodi kwa Kamishna Mkuu;
b) waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi;
c) waliingia makubaliano na Kamishna Mkuu ya kusamehewa riba na adhabu za kodi kama ilivyoanishwa katika Amri Na. 282A ya Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018;
d) walianza kulipa kodi ya msingi kwa mkupuo au kwa awamu; na
e) mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2019 walishindwa kulipa kiasi cha kodi ya msingi kilichokubaliwa kwa ukamilifu.

Hivyo, wastahiki wote wa msamaha waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi mnakumbushwa kulipa kodi ya msingi kama ilivyoainishwa kwenye mikataba ya makubaliano wa malipo kabla au kufikia tarehe 31 Disemba, 2019 na kwamba hakuna nyongeza zaidi ya muda itakayotolewa.

Izingatiwe kwamba, pindi mstahiki wa msamaha aliyepatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018 atashindwa kutekeleza sehemu ya masharti ya mkataba wa makubaliano wa malipo, Kamishna Mkuu atabatilisha mkataba wa makubaliano wa malipo na kudai kiasi cha kodi kilichosalia kama vile hakukuwa na msamaha alioutoa. Aidha, hatua za ukusanyaji zitachukuliwa kuanzia tarehe 2/1/2020 bila taarifa nyingine.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Dr. Edwin P. Mhede Ph.D**
**KAMISHNA MKUU**

215445702

# Jafo aagiza mratibu wa Tarura asimamishwe kazi

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo ameagiza kusimamishwa kazi kwa wiki mbili Mratibu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) Mkoa wa Rukwa, Boniface William.



Jafo ameagiza kuchukuliwa kwa hatua hiyo ili kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazomkabili za kutoa kazi za matengenezo ya barabara mkoani hapa.

Agizo hilo alilitoa jana wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga juu ya utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la kuipa mwezi mmoja halmashauri hiyo kuwa imehamisha ofisi zake zilizoko Sumbawanga mjini kwenda mji mdogo wa Laela.

Waziri Jafo alisema kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kuwa Tarura mkoa imekuwa inatoa kazi za utengenezaji wa barabara mkoani humo kinyume cha utaratibu, hivyo kumwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Josephat Nyamuhanga, kumsimamisha kazi William ili kupisha uchunguzi wa tuhuma hizo.

Pia aliziagiza halmashauri zote nchi ambazo madiwani walipitisha maazimio kuwa zihame katika maeneo zilizopo kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi, zifanye hivyo katika kipindi cha mwezi mmoja.

Alisema kuwa lengo la kufanya hivyo ni kutekeleza agizo hilo la Rais na kuona wananchi hawapati usumbufu pindi wanapohitaji huduma kutoka katika halmashauri zao.

Katika hatua nyingine, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Mathias Nyange, alisema tayari jeshi hilo linamshikilia Mkurugenzi wa Kampuni ya Fally Enterprises, Felix Lyowa, ambaye juzi Rais Magufuli aliagizwa akamatwe na kuchukuliwa hatua kutokana na kutekeleza mradi wa Laela wenye thamani ya Sh. bilioni 1.7 chini ya kiwango.

Alisema mkandarasi huyo anadaiwa kutekeleza mradi huo pamoja na mingine yenye thamani ya Sh. bilioni tano mkoani Rukwa chini ya kiwango, hivyo kusababisha wananchi kukosa maji.



Gari la kuvuta magari mabovu (Breakdown), likijaribu kuliinua gari dogo aina ya Vits yenye namba za usajili T802 DFH, lililoacha njia na kutumbukia mtaroni maeneo ya Tabata Barakuda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Kata 18 zaunga mkono maandamano ya Makonda

**Na Elizabeth Zaya**

WANANCHI wa kata 18 zilizoko kandokando ya Mto Msimbazi, wamesema wanamuunga mkono Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kwa wazo lake la kufanya maandamano ya kudai ujenzi wa mifereji eneo la Buguruni Mivinjeni, huku wakimsisitiza kuyaunganisha na usafishaji na uboreshaji wa Mto Msimbazi.

Wananchi hao wamejitokeza kueleza msimamo huo baada ya hivi karibuni, Makonda kutangaza kushirikiana na wananchi wa kata tano za Buguruni Mivinjeni Wilaya ya Ilala, kufanya maandamano hadi Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi Oktoba 10, mwaka huu ya kudai ujenzi wa mifereji.

Wakizungumza katika ofisi za Nipashe, viongozi wawakilishi wa mitaa hiyo, walisema ni vema Makonda akaunganisha na Mto Msimbazi ambao mifereji ya Buguruni Mivinjeni inatiririsha maji humo.

"Tunampongeza sana Makonda kwa wazo la kuandamana hadi Tamisemi, tunamwomba aunganishe na Mto Msimbazi, asiishie Mivinjeni kwa sababu mitaro yote hiyo anayoidai inatiririsha maji katika Mto Msimbazi ambao umejaa mchanga na taka ambazo zinasababisha mafuriko na kuleta athari katika makazi ya wananchi," alisema Godwin Cathbert, Mratibu wa kata hizo 18 za Mto Msimbazi.

"Kwa hiyo sisi tunamuunga mkono moja kwa moja Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, tutaandamana naye hadi huko Tamisemi, tunataka na mto huu usafishwe na kuboreshwa hata ikiwezekana kabla mvua hazijawa nyingi na kuleta athari," alisema Gdwin.

Makonda alitangaza maandamano hivi karibuni alipokagua miradi ya maendeleo wilayani Ilala, baada ya kuzungumza kwa simu na Mratibu wa Miradi ya Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) wa Tamisemi, Emmanuel Ndyamukama na kupewa majibu yasiyoridhisha.

## Kampuni za simu zatakiwa kuendesha kampeni dhidi ya maambukizi Ukimwi

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, amezitaka kampuni za simu za mkononi kuweka ujumbe au tangazo kwenye simu za wateja kwa lengo la kuendesha kampeni ya kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi nchini.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ilieleza kuwa Nditiye alitoa kauli hiyo akiwa kwenye kikao na viongozi wa kampuni hizo na kuwataka watengeneze na kuweka ujumbe au tangazo hilo kuanzia Oktoba 15, mwaka huu.

Alisema ujumbe huo uendelee kuwapo hadi siku ya kilele cha maadhimisho ya Ukimwi yanayofanyika kila mwaka ifikapo Desemba mosi ambao utawakumbusha wananchi kuwa Ukimwi bado upo, ni janga la kitaifa na hauna dawa.

"Ninyi ni mawasiliano na mawasiliano yananihusu, sisi tunapatikana kila dakika kuliko televisheni, redio au magazeti, kila mwananchi anapatikana kwa kuwa ana simu ya mkononi na ninyi mtusaidie kutangaza masuala ya kimkakati ya kitaifa mfano janga la Ukimwi bado lipo, mtusaidie kuweka ujumbe kuhusu ugonjwa huu ili tusaidie wananchi," alisema Nditiye.


Naye Mkuu wa Kanda ya Ziwa wa Kampuni ya simu ya Vodacom, Gwamaka Mwakilemba, alimweleza Nditiye kuwa wako tayari kuandaa ujumbe au tangazo hilo kwa kuwa janga la ugonjwa wa Ukimwi linagusa jamii ambayo ni wateja wa kampuni yao.

Aliiomba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuongeza kasi ya kutoa namba au vitambulisho vya taifa ili kampuni za simu ziweze kusajili idadi kubwa ya wananchi.

Naye Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, Stanslaus Mabula, aliziomba kampuni za simu za mkononi kuwa sehemu ya kupiga vita maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi na kutoa tahadhari kwa wateja wake kupitia ujumbe kwenye simu zao.



TANGAZO


NMB
Karibu yako
NMB Mobile
na KLiK sasa ni
NMB mkononi
Piga *150*66#
au Pakua APP
na Ufungue
Akaunti
Download on the App Store
GET IT ON Google Play
Wakati Wowote
Mahali Popote
#kilakitukwanmbmkononi
Kwa maelezo zaidi piga
0800 002 002
nmbtanzania
Fungua Akaunti
Tupe taarifa zako
+255 Namba ya simu
Jina la Kwanza
Jina la Kati
Jina la ukoo
Jinsia
Chagua uraia
Aina ya kitambulisho
Namba ya kitambulisho
ENDELEA
www.nmbbank.co.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuamue sasa kuhusu kutumia simu shuleni

WIKI iliyopita Shule ya Sekondari ya Kiwanja, iliyoko mkoani Mbeya ilichomwa moto na wanafunzi zaidi ya 13 wanaodaiwa kuwa walighadhabika kutokana na simu zao kuchukuliwa na uongozi wa shule hiyo.

Suala la simu shuleni, si kitu cha kukipuuza kwa sababu tupende tusipende ni vigumu kuwadhibiti wanafunzi wasiingie na simu mabwenini au shuleni kwani wanafahamu wenyewe cha kufanya kumiliki simu hizo.

Vuguvugu la wanafunzi kuruhusiwa kutumia simu shuleni au kuzipiga marufuku kuingiza eneo hilo ni jambo ambalo linahitaji wadau kulizungumza ili kuepusha yale yaliyotokea Sekondari ya Kiwanja.

Vita vya simu shuleni havina mshindi hata kama zitakatazwa wanafunzi wanajua namna ya kuziingiza na kuzitumia bila kugundulika na walimu na watakapobainika na kuzuiliwa si kwamba tatizo hilo litamalizika.

Kwa vile ni vigumu kukataza simu shuleni zama hizi, wakati huu kwani ni nyenzo muhimu ya mawasiliano miongoni mwa watoto wawe sekondari au shule za msingi kwa hiyo zinahitajika sheria na miongozo ya namna ya kumiliki na kutumia simu shuleni.

Tunaona kuwa wanafunzi wanahitaji simu kwa sababu ya kusoma na pia kuwasiliana na familia zao na walimu pia.

Pia simu hiyo ni nyenzo ya kusomea na kujifunzia, kwa hiyo inahitajika miongozo na taratibu za kutumia simu shuleni.

Pengine ni wakati wa kufikiria, hasa wadau na Wizara ya Elimu kuona namna ya kuandaa miongozo na sheria hizo na shule zikaanza kuruhusu wanafunzi kutumia simu.

Lakini ni vigumu kusema kuwa kama taifa tupige marufuku matumizi ya simu shuleni.

Tunaona kuwa zama hizo simu ni nyenzo ya kusomea na kujifunzia. Simu zinaweza kutumiwa kupakua vitini kwenye mtandao ni jambo ambalo halikwepeki. Shule nyingi hazina kompyuta lakini zinaweza kuruhusu wanafunzi kutumia simujanja kupakua vitini na elimu kutoka kwenye mitandao mbalimbali.

Wanafunzi watumie intaneti kusoma na kwa wale ambao hawana simujanja na fedha za kuchukua vitini, shule italazimika kuwa na kompyuta ndogo (mpakato) kwa ajili ya kupakua vitini mtandaoni.

Lakini si hivyo tu kuna mkongo wa taifa ambao unategemewa kusambaza mtandao wa intaneti nchi nzima, ndiyo wakati wa shule nazo kutoa 'vifurushi vya wifi' bure kwa wanafunzi ili wanapopakua vitini viwafikie wanafunzi wote kwa kuwa shule inagharamia kwenye simu na kwenye kompyuta ya simu.

Wanaweza kupakua kutoka kwenye Google na Wikipedia. Hizi ni zama za sayansi na teknolojia huwezi kukwepa teknolojia ya simu ni vyema kulitafakari hili na kulifanyia maamuzi.

Tunaona kuwa simu zina umuhimu wa kipekee shuleni. Kwa mfano ni nyenzo ya mawasiliano baina ya wazazi na watoto.

Simu zinaweza kutumia kuwahakikishia ulinzi wa watoto na utaratibu huu unawezekana kwenye simujanja (smartphones) na hivyo itasaidia kunasa na kufahamu kuhusu watoto watukutu kama wapo shule au wameingia mitaani.

Simu hizo pamoja na mambo mengine zinaweza kutumika kuwasiliana wakati wa dharura. Mathalani kuna uvamizi, ubakaji watoto, yapo mashambulizi na hata utoroshaji wa albino.

Simu kama nishati ya umeme zinahitajika shuleni. Kwa hiyo ni vyema kuandaa utaratibu na muda wa kuzitumia badala ya kufikiria kuzipiga marufuku.

Ndiyo maana tunasema ni vyema shule zikaandaa namna bora ya kutumia simu badala ya kuzipiga marufuku.

Suala la usalama wakati wa kuchaji simu nalo ni la muhimu hivyo, ili kuepusha hatari ya kuleta shoti na umeme au kutokea milipuko kutokana na kutumia chaja mbovu shule ziweke mazingira bora ya kuchajia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Salome Kitomari

# Rushwa ya ngono bado tishio, tupambane nayo

**RUSHWA** ya ngono hufanyika kwa siri baina ya watu wawili kwa anayelazimishwa kutenda hivyo na anayetaka kutenda kwa manufaa yake mwenyewe ili atoe huduma fulani.

Rushwa hiyo iko hata kwenye sehemu za kazi kwamba mtu anatakiwa kutoa rushwa ndiyo apate nafasi ya kazi si kwa uwezo wake, bali kwa rushwa aliyotoa kwa muhusika.

Hilo linakwenda pia hadi kwenye vyuo vya elimu ya juu nchini kwamba wapo wanafunzi wanaomaliza vyuo na kupewa alama zilizosukumwa na mahusiano yao na wakufunzi wao kuliko kuwa na uwezo wa masomo hayo.

Hali hiyo imesababisha wanaobebwa kwa kutumia miili yao iwe wanaume au wanawake, kushindwa kufanya kazi inavyopaswa wanapofika katika maeneo yao ya ajira kutokana na ukweli kwamba hawakuwa na sifa ya kupata ajira husika isipokuwa njia ya rushwa waliyoipitia.

Athari kubwa ni kuwa na watu wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa sababu pamoja na mengine mhusika alitoa rushwa ya ngono ili afaulu kwa kiwango cha juu.

Yaani apate ufaulu (GPA) ya daraja la kwanza, na hivyo hivyo alipofika kazini akatoa rushwa nyingine ili apate nafasi na hata alivyopata nafasi hiyo akaendelea kutoa rushwa ili ajihakikishie nafasi yake.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imethibitisha kuwa rushwa ya ngono ni ngumu kukabiliana nayo, kutokana na mazingira ya utendekaji wake na wahusika.

Aidha, wakati mwingine wahusika hawatoi taarifa kwa mamlaka zinazohusika kutokana na sababu mbalimbali.

Baadhi ya sababu hizo ni kwa mhusika kuchukulia kwamba ikitoa taarifa atadhalilika au kushusha heshima yake iwapo jambo hilo litajulikana.

Wengine ni kutokana na utamaduni wa usiri na mfumo dume na hivyo wamejikuta wakishindwa kupaza sauti.

Hivi karibuni, Rais John Magufuli, alisema rushwa ya ngono kwa wanaume ipo pia kwani wapo wanaohongwa na wanawake, jambo ambalo limeleta changamoto katika utekelezaji wa majukumu.

Rushwa ya ngono ni kati ya makosa 24 yanayoshughulikiwa na sheria ya rushwa ya Takukuru, na wapo ambao wamechukuliwa hatua baada ya kukamatwa.

Rushwa hii ina athari nyingi ikiwa ni pamoja na kudidimiza taifa kwa kuzalisha watu wasielimika, wasio na uwezo wa kutenda kazi na ofisi kukosa ufanisi kwa sababu mapenzi yanakuwa ndiyo kipaumbele.

Lakini changamoto nyingine ni kuongeza maambukizi ya maradhi mbalimbali, kwa sababu baadhi ya wanaojenga mazingira ya rushwa hiyo kutendeka wanajua uhalisia wa afya zao kwamba zina walakini, hivyo kuendeleza maambukizi kwa wengine.

Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), kinafanya kampeni ya kuelimisha jamii kutambua madhara ya rushwa ya ngono na athari zake, pia kuibua habari mbalimbali ambazo zitasaidia kuwabaini wanaohusika na matukio hayo.

Kwa ujumla janga hili linadidimiza taifa na kusababisha watu wasipate huduma stahiki. Aidha, linaongeza wasio na sifa na kuwanyong'onyesha wenye sifa za nafasi husika.

Wakati tukielekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, ni muhimu kuitazama kwa jicho la pekee rushwa hii, kwani inafifisha azma ya kupata viongozi sahihi ambao watawatumikia wananchi.

Yeyote anayekutwa na rushwa ya ngono atambue kuwa ni kosa kisheria na inaweza kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Ni faraja kutokana na taarifa njema kwamba Takukuru ina namna ya kuwahudumia wanaokumbwa na adha hiyo na kwamba taarifa zao zitabaki kuwa za siri.

Muungwana anaona kwamba kama mamlaka zimejitokeza kukabiliana na rushwa hiyo sehemu mbalimbali nchini, basi ni wajibu kwa wanaonyanyasika kwa namna yoyote kwa rushwa hii wakatoa taarifa na hatua zikachukuliwa.

Jamii ikishiriki kutokomeza rushwa hii maana yake nafasi za ajira zitapata watu sahihi, wasomi sahihi na wananchi sahihi ambao hawategemei kutoa kitu au kujidhalilisha ili kupata nafasi fulani.

> **Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imethibitisha kuwa rushwa ya ngono ni ngumu kukabiliana nayo, kutokana na mazingira ya utendekaji wake na wahusika.**

BARUA/MJADALA

# Uchafuzi huu Tandale haukubaliki

***Mhariri habari***

*NINAJITOKEZA kwa mara ya kwanza katika gazeti letu hili lililo na kurasa iliyo mahsusi kwa lengo la kutuwezesha tueleze kero na dukuduku mbalimbali tulizo nazo ili ziwafikie wahusika kwa minajili ya kutatuliwa.*

*Mimi ni mkazi wa Tandale jijini Dar es Salaam. Ninakerwa kwa kweli na tabia iliyoenea katika eneo letu inayofanywa na baadhi ya wakazi wenzetu ya kujisadia ovyo haja ndogo kwenye chupa za maji.*

*Mbaya zaidi wakishajisaidia kwenye chupa hizo za maji huzitupa ovyo kwenye barabara za mitaa mbalimbali na kuziacha bila hata ya kufikiria madhara yake katika suala zima la uchafuzi wa mazingira, lakini pia kwa kuhatarisha afya za wakazi wenzao.*

*Tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu na inaonekana kama vile halijapatiwa ufumbuzi pengine kutokana na kufanyika kwa kificho na hasa nyakati za usiku na hivyo kusababisha ugumu kwa sisi wananchi kuwaona wahalifu hao.*

*Ninaomba kupitia kwako Mhariri watu hawa wasio wastaarabu waache tabia zao hizo. Vilevile naziomba mamlaka za kiserikali zilizo katika eneo letu zilishughulikie suala hili kwa ukamilifu kwani linatuathiri kiafya.*

***Mwathirika-Tandale***

# Walezi tusifuge tabia zisizokubalika

***Mhariri***

*KWA kweli kuna tabia ambayo inanishangaza sana mimi ya baadhi ya wazazi na walezi katika jamii yetu hii ya Kitanzania ambao kwa kiasi kikubwa hawako tayari kusikiliza ushauri wanaopewa na majirani zao juu ya tabia za watoto wao.*

*Katika mtaa ninaoishi hapa Mbalizi mkoani Mbeya, kuna jirani yangu aliye na mtoto mwenye tabia zisizokubalika katika jamii ya kawaida na hata katika mwenendo wa kawaida wa maisha ya watu.*

*Mtoto wake huyu ana tabia ya kukwapua mali za watu na hata kukaba hasa nyakati za usiku na mchana kwenye maeneo yasiyo na watu.*

*Anafanya uhalifu huu kwa kushirikiana na vijana wanaotoka maeneo mengine ya jiji hili la Mbeya.*

*Lakini cha kusitikisha zaidi ni kuwa kwa majirani ambao wameshawahi kwenda kuwaeleza wazazi wake juu ya uhalifu anaoufanya kijana wao, mara nyingi wamekuwa wakikataa kuwa kijana wao hana tabia hiyo.*

*Kwamba wanaoenda kulalamika kwao wanamwonea gere kijana wao kutokana na maendeleo anayoyafanya.*

*Naomba serikali ya mtaa wetu ichukue hatua ya kumkanya kijana huyo ili aachane na tabia hiyo kwani inaweza ikamhatarishia maisha yake siku moja na hasa pale wananchi watakapojichukulia sheria mkononi.*

***Jason Mandyanga- Mbalizi***




# Kuelekea uchaguzi S/Mitaa wagombea mnajipangaje

**Na Gaudensia Mngumi**

MWEZI Oktoba umeanza na kinachotakiwa kuwa kwenye fikra za Watanzania sasa ni kupiga kura ili kuchagua viongozi wa serikali za mitaa na vijiji.

Uchaguzi huo ambao maandalizi yake yameshaanza ni watu kuanza kujiandikisha na kujitokeza kwa wingi na kwenda kupiga kura.

Licha ya kwamba watu wengi hawajahamasika kujua umuhimu wa viongozi wa serikali za mitaa ni vizuri kuwachagua viongozi hao ambao wana jukumu kubwa la kuanza michakato muhimu ya kuwasaidia wananchi katika ngazi za chini.

Uchaguzi wa serikali za mitaa ni muhimu kwani ndiyo wakati wa wananchi kujichagulia viongozi wanaowahitaji.

Si jambo jema watu wakajikausha na kujipa moyo kuwa kiongozi atachaguliwa na wengine. Si afya watu wachache kuwachagulia walio wengi kiongozi. Na hilo si jambo jema kwa kijiji, mtaa na hata taifa.

Mara nyingi imekuwa ni kawaida watu kupokea wito wa kufanya uchaguzi kwa amani, lakini safari hii ni vyema kuzingatia masuala ya haki kwa sababu hakuna amani bila haki.

Ni wakati wa kuzingatia haki na kuwapa wanawake, wenye ulemavu na makundi yasiyo na sauti nafasi ya kushiriki na si kupendekeza watu kwa misingi ambayo italalamikiwa kuwa haikuwa ya haki.

Mambo mengi yanayozungumzwa na kinamama, walemavu na watu wengine kuhusu rushwa iwe ya ngono au ya fedha ni vyema yakasikilizwa kwa sikio la pili.

Mara nyingi wito wa amani umekuwa ukitolewa sana nyakati za kura lakini safari hii iwe haki na amani.

Watu ambao hawana au hawakuwa na haki ya kugombea wanapopewa nafasi na uongozi, ni wazi kazi zao hazitakuwa na tija.

Iwapo uchaguzi utafanyika kwa njia zisizo za haki kwa kuwabagua au kutowajali wanawake na watu wanaoishi na ulemavu ni wazi kuwa viongozi watakaopatikana hawatakuwa na la maana katika kuihudumia jamii.

Kama kawaida matusi kwenye kampeni ni jambo ambalo kwenye chaguzi za nyuma yamekuwa yakisikika.

Hakuna sababu ya kutoka kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa safari hii. Kutukanana majukwaani ni kasoro kubwa ya kiuongozi.

Ni wakati wa kuonyesha ukomavu wa kisiasa na ikibidi kukaa kimya bila kujibizana na wale wanaokutukana.

Suala la kuleta mabadiliko katika jamii kati ya viongozi wa CCM na wapinzani ndilo jambo ambalo wengi wanalitegemea.

Wananchi wanataka kusikia ahadi za mabadiliko, yawe ya utoaji wa huduma kuanzia kwenye ofisi za kijiji, kutatua kero za wananchi na kubadilisha uongozi duni ndicho watu wanachotaka kukisikia.

Haina maana kuendelea kuwa na viongozi wasioweza kujenga choo kwenye ofisi ya kata au ya kijiji kisa eti wamependekezwa na kuchaguliwa.

Licha ya wote kuhubiri mabadiliko ambayo yamefanywa na serikali iliyoko madarakani, ni wakati wa viongozi wa ngazi za chini nao kuonyesha mabadiliko wanayoyasimamia.

Haina maana kuwa na kiongozi wa mtaa au kijiji wakati eneo halina maji na wananchi wanaliwa na wanyamapori usiku wakisaka maji.

Viongozi wana wajibu wa kutoa ufumbuzi wa namna ya kukabiliana na matatizo kama hayo na si kuwa na viongozi wa kukaa kwenye ofisi za kata, mitaa na vijiji.

Ni wazi kuwa wagombea wa CCM wanapotoa ahadi ya mabadiliko, wanafanya hivyo kwa kurejea mafanikio yaliyopatikana, lakini kama kiongozi uliyejitokeza mwenyewe na kutaka kugombea ni lazima useme unaleta jambo gani jipya.

Kwa ujumla, ajenda ya mabadiliko iwe dira, mwelekeo na kioo cha kujitizamia kwa wagombea wote kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa ili kuwe na uongozi wenye nidhamu.

Ikumbukwe kuwa hakuna haja ya kupinga jambo linalozungumzwa na wapinzani kuwa litafanyiwa mabadiliko ili kuboresha hali ya wananchi, ni vyema likatafsiriwa kuwa kero zinazozungumziwa na wapinzani ndizo zinazowakera Watanzania hata ikiwa ni wana CCM.

Hivyo, ni vyema viongozi wakatizama yanayowasumbua wananchi kama ukosefu wa maji, barabara vijijini na mitaani, kuzagaa mitaro ya majitaka na migogoro ya ardhi kuwa ni mambo yanayosumbua wananchi yanayotaka ufumbuzi badala ya kuyaangalia kwenye sura ya upinzani na chama tawala.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Bulaya: Mbowe anatosha Chadema

**Na Kelvin Innocent**

MBUNGE wa Bunda Mjini, Esther Bulaya (Chadema), amesema chama chao, hakiwezi kuteuliwa mwenyekiti wa kukiongoza, na kwamba mwenyekiti wao atabaki kuwa Freman Mbowe.

Bulaya aliweka wazi msimamo huo katika mkutano uliowakutanisha baadhi ya viongozi wa chama hicho na wanawake wa Kata ya Kawe jijini Dar es Salaam.

Bulaya alisema kazi yao ni moja tu ya kuhakikisha wanawahamasisha wanawake kwa wanaume kujitokeza katika kupiga kura kwenye chaguzi wa serikali za mitaa.

"Na nia hiyo tunayo, sababu tunayo na dhamira pia tunayo kutokana na uchumi mbovu uliosababishwa na serikali ya Chama Cha Mapinduzi na ahadi zisizo tekelezeka," alidai.

Pia alisema wamama wajawazito wanatozwa fedha ili kupata huduma ya kujifungua, wakati sera ya afya ikisema huduma za afya kwa mjamzito, mtoto chini ya miaka mitano na wazee ni bure.

"Mjamzito anaambiwa atoe laki tatu ili kujifungua, lakini sera inasema huduma za afya kwa mjamzito, mtoto chini ya miaka mitano na wazee ni bure," alisema.

"Tulipokuwa kwenye Bunge la Katiba tuliwaambia sera hizi hazitekelezeki, lazima iingizwe kwenye Katiba mama ili tuhakikishe afya za Watanzania zinakuwa imara," alisema Bulaya.

Aidha Bulaya alisema inahitajika serikali inayowekeza kwenye uchumi na maendeleo ya watu, na siyo ya vitu na kwamba kwenye taifa lolote maendeleo ya watu ni muhimu.

Aidha, aliwataka wanawake kujitokeza kuwania uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi ujao.

"Kinamama tushikane mikono, na wewe ndiye utakaye kuwa wa kwanza kumshika mkono ili aweze kushinda, na akishinda/kufanya vizuri anafungua milango ya wanawake wengine. Sitarajii mwanamke aongoze kampeni chafu dhidi ya mwanamke mwenzako, sisi tunatakiwa tupendane," alisema.




Meneja Uhusiano wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), William Kallage, akizungumza na wafanyabiashara wakati wa uzinduzi wa klabu ya wafanyabiashara wa Singida jana. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# WB yaimwagia tril. 1.03/- Tasaf

**Elizabeth Zaya na Mary Geofrey**

BENKI ya Dunia imetoa mkopo wa masharti nafuu wa Sh. trilioni 1.035 kwa serikali ya Tanzania kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa mradi wa kipindi cha pili wa Mpango wa Tatu Kunusuru Kaya Maskini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf III).

Hafla ya utiaji saini wa utekelezaji wa mpango huo kati ya pande hizo mbili ilifanyika jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kutia saini mkataba huo, Katibu Mkuu Wiraza ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema awamu ya pili ya mpango huo imelenga zaidi katika kuimarisha miundombinu ya shule, afya na maji. Alisema lengo la mpango katika kipindi cha pili ni kuwezesha kaya masikini kutumia fursa ya kujiongezea kipato kupitia miradi mbalimbali inayoendeshwa na Tasaf.

Alisema awamu hiyo ya pili ya mpango huo wa tatu italenga zaidi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kutoa ajira za muda kwa kaya maskini ikiwamo ujenzi wa shule, zahanati, barabara za kijamii na uchimbaji wa mabwawa ya maji.

"Fedha hizi pamoja na kwamba zitaenda kuzisaidia kaya masikini ambao ni wazee wasiojiweza kufanya kazi na wengine wanaofanana na hao, lakini pia kundi jingine litakalonufaika ni kaya masikini ambazo hazina uwezo, zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi," alisema na kuongeza:

"Hawa watashiriki katika shughuli za kijamii hususani ujenzi wa madarasa, shule za msingi na sekondari, ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, barabara za kijamii na miradi ya maji hususani kuchimba mabwawa ya maji. Baada ya kufanya kazi hizo, watakuwa wanapewa ujira. Tumepata uzoefu kwa wenzetu wa Ethiopia wanafanya hivyo na wamefanikiwa sana."

Alisema serikali imekubali kuendelea na mpango huo ili kupata matokeo mazuri zaidi ya kupunguza umaskini nchini kwa kuongeza uchumi wa kaya kupitia uzalishaji wa kipato.

Pia alisema lengo la mpango huo ni kuziwezesha kaya hizo kuongeza rasilimali za lishe, kujihusisha zaidi na kazi za uzalishaji, kukuza uchumi wa eneo unapofanyika utekelezaji na kuendeleza watoto kwa kuwekeza katika lishe na shuleni.

Mpango huo, alisema unatarajiwa kufika mwaka 2023, na kwamba umeongeza nguvu katika juhudi za serikali za kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi wake.

Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Bella Bird, alisema benki hiyo ilipitisha wazo la kuwezesha mpango huo kwa kishindo baada ya kuona mafanikio makubwa yaliyofanyika katika mpango unaomalizika.

"Nilipowasilisha mada ya mpango huu kwa Benki ya Dunia, ulipitishwa kwa kishindo na hii imetokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na serikali ya Tanzania katika kutekeleza miradi yake" alisema Bella Bird.

Alisema katika kutathmini utekelezaji wa mpango wa kwanza wa Tasaf unaomalizika, walitumia mkaguzi ambaye hafungamani na upande wowote kufanya kazi hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladslaus Mwamanga, alisema katika utekelezaji wa mpango huo, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizofanikiwa na kwamba wamekuwa wakipokea wageni kutoka nchi mbalimbali wanaokuja kujifunza.

SUMAJKT AUCTION MART

MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYO PEWA NA TUJIJENGE TANZANIA LIMITED TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA NYUMBA/ VIWANJA KAMA JEDWALI LINAVYOONESHA HAPA CHINI.

| | JINA | MAHALI ZILIPO | DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Nuru Nassib Ramadhan | Vijibweni Mtaa Kisiwani- Kigamboni | Nyumba | 11/10/2019 Saa 08:00 Mchana |
| 2 | Nuru Angomwile Legembo | Mbondole - Kivule | Kiwanja | 16/10/2019 Saa 04:00 Asubuhi |
| 3 | Abdul Hashim Said | Mbondole Kivule | Nyumba | 16/10/2019 Saa 06:00 Mchana |
| 4 | Naomi Joseph Wambura | Mbondole Kivule | Nyumba | 16/10/2019 Saa 08:00 Mchana |
| 5 | Khadija Hussein Jafarah | Mgeninani-Kijichi | Kiwanja | 24/10/2019 Saa 04:00 Asubuhi |
| 6 | Abdallah Hussein Waziri/ Khadija H. Safarah | Mtaa Wa Kombo-Vingunguti | Nyumba | 24/10/2019 Saa 08:00 Mchana |
| 7 | Haji J. Chitonya/ Franklin Alexander Mlay | Yombo Vituka | Nyumba | 28/10/2019 Saa 04:00 Asubuhi |
| 8 | Frank Isaya Lesilwa/ Nuru Angomwile Legembo | Nzasa 'A' -Mbagala | Nyumba | 31/10/2019 Saa 04:00 Asubuhi |

MASHARTI YA MNADA

1) Mteja anatakiwa kulipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14
2) Endapo Mteja atashindwa kumalizia 75% ya salio lililobaki ndani ya siku 14 hatarudishiwa kiasi alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
3) Gharama zote za kubadili HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI.
Kwa mawasiliano zaidi piga namba:-0716004554 NA 0753063481

215449602

## Vigogo wa NIDA kubadilishiwa mashtaka

**Na Beatrice Shayo**

UPANDE wa mashtaka katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili vigogo sita wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), umedai kuwa upelelezi katika kesi hiyo umekamilika na kwamba wanatarajia kubadilisha hati ya mashtaka baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kutoa hati ya kuipa ruhusa mahakama hiyo kusikiliza kesi hiyo.

Vigogo hao wanakabiliwa na mashtaka 100 kati ya hayo mashtaka 24 ni ya utakatishaji fedha zaidi ya Sh. bilioni 1.1, mashtaka 23 ya kughushi nyaraka na 43 ni kuwasilisha nyaraka za uongo ili kumdanganya mwajiri wao na kuisababishia mamlaka hiyo hasara.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Ladislous Komanya, amedai mbele ya Hakimu Mkazi Salum Ally kuwa kesi hiyo imekuja kwa ajili ya kutajwa na kutoa amri na maelekezo.

Pia alidai kuwa kati ya washtakiwa sita ni wawili pekee waliofika mahakamani.

Alidai kuwa kesi hiyo isingeweza kuendelea jana kwa sababu hatua zote hizo zinakwenda pamoja na washtakiwa wengine ili wasomewe mashtaka upya. Kesi hiyo imeahirishwa hadi kesho na mahakama imetoa hati ya kutolewa washtakiwa gerezani.

Washtakiwa waliokuwapo mahakamani ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Aste Insurance Brokers, Astery Ndege na Xavery Kayombo.

Washtakiwa waliopelekewa hati ya wito gerezani ni Mkurugenzi wa Nida, Dickson Maimu, Meneja Biashara wa (NIDA), Aveln Momburi, Ofisa Usafirishaji, George Ntalima, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 100 kati ya hayo, 24 yakiwa ni ya utakatishaji fedha zaidi ya Sh. bilioni 1.1, mashtaka 23 ya kughushi nyaraka; mengine 43 ni kuwasilisha nyaraka za uongo ili kumdanganya mwajiri wao na kuisababishia mamlaka hiyo hasara.

Mashtaka mengine ni ya kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu (mawili), shtaka moja la matumizi mabaya ya madaraka na mawili ya kula njama.

Wanadaiwa kati ya Julai 19, mwaka 2011 na Agosti 31, mwaka 2015, wakiwa maeneo tofauti ndani ya Jiji la Dar es Salaam walikula njama ya kufanya udanganyifu wa Sh. bilioni 1.175 dhidi ya NIDA.

Maimu na Raymond wanadaiwa Novemba 7, mwaka 2011, wakiwa Makao Makuu ya NIDA, Kinondoni, walitumia madaraka yao vibaya na kusababisha Kampuni ya Gotham International Ltd kupata faida ya Sh. 899,935,494.

# Watumishi waagizwa kufafanua tiba ya wazee

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

MGANGA Mkuu wa Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera pamoja na wataalamu wengine wa afya wameagizwa kuueleza umma taarifa za tiba ya wazee.

Wataalamu hao wa Idara ya Afya wametakiwa kutoa elimu kwa jamii hasa wazee, kuhusu dawa zinazotumika katika matibabu yao zinazopatikana ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Lengo ni kupunguza tatizo la wazee kwenda kutibiwa na kuambiwa dawa hazipo hospitalini na vituoni.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Karagwe, Godfrey Mheruka, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera kwenye maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yaliyofanyika wilayani Karagwe wiki iliyopita.

Agizo hilo lilitokana na hoja ya Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Christopher Mwasongela, akisema kuwa dawa zipo za kutosha lakini si kila dawa inasambazwa katika ngazi zote za huduma.

"Wazee hawayajui haya, zungukeni mkawaelimishe hatua zipi wanapaswa kuzifuata ili kupata huduma wanazostahili na kupunguza malalamiko kwa serikali," alisema Mheruka.

Alisema serikali katika mwaka huu wa fedha imetoa Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya kununua dawa katika wilaya ya Karagwe na kuwa haiingii akilini kusikia wazee wanaandikiwa dawa na kuambiwa dawa hazipo waende wakanunue.

Aidha, alisema kuwa wilaya hiyo imepewa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya ambayo ujenzi wake unaendelea na kuwa utakapokamilika matatizo mengi yanayowakabili wazee yatapungua.

Pia mkuu huyo wa wilaya aliwaagiza maofisa tarafa, watendaji wote wa vijiji na kata, kuhakikisha wanawalinda wazee dhidi ya vitendo vya kikatili wanavyofanyiwa katika maeneo yao.

Alivitaja kuwa ni pamoja na kuchomewa nyumba na kufyeka mashamba.

Haya yanafanyika wakiwatuhumu kwa uchawi na wengine wakitaka wafe ili wachukue mali zao na kuwa watakaobainika kuhusika wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Akijibu malalamiko ya wazee kukosa dawa na kuambiwa waende kununua, mganga mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Mwasongela alisema kuwa serikali inatoa fedha kwa ajili ya dawa, lakini sio kila dawa zinapatikana katika ngazi zote na kuwa zipo zinazoruhusiwa kuwapo katika ngazi za hospitali tu.

# PM aagiza ofisa ununuzi akamatwe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Singida, kumkamata ofisa manunuzi wa Chuo cha Kinampanda kwa tuhuma za ufisadi.

Waziri Mkuu alimwagiza Adili Elinipenda, kumkamata Francis Muyombo, kwa tuhuma za kukiuka taratibu za manunuzi ya serikali na kughushi nyaraka.

Aidha, alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa Sweetbert Njewike, amkamate na kumhoji Joseph Kisaka ambaye alikuwa mzabuni wa chuo hicho kwa kuwapatia vifaa ambavyo ni chini ya kiwango.

Alitoa agizo hilo Jumapili jioni, wakati akikagua ukarabati wa majengo ya chuo hicho kilichopo wilayani Iramba, mkoani Singida na kubaini nyaraka za kupokea vifaa zikionyesha kitasa kimoja kimenunuliwa kwa Sh. 70,000 badala ya Sh. 25,000.

Waziri Mkuu alisema nyaraka za makubaliano ya ununuzi zinaonyesha kwamba walipaswa kununua vitasa ambavyo vinafunga mara tatu (vya three level), lakini alipokwenda kukagua milango kwenye mabweni, ukumbi na bwalo alikuta ni vitasa vya kufunga mara moja (one leavel).

"Serikali imetoa Sh. bilioni 1.4 kwa kila chuo ili kufanya ukarabati wa vyuo vya elimu kikiwamo hiki cha kwenu. Ninyi mnanunua vifaa kinyume na utaratibu wa serikali, hamvikagui, mnaweka tu vitu hafifu ambavyo havidumu. Haiwezekani."

"Nyaraka zenu hapa zinanionyesha mlinunua vitasa 368 vya kufunga mara tatu kwa gharama ya Sh. 70,000 kila kimoja. Lakini vitasa vilivyoko mlangoni vinafunga mara moja ambavyo vinauzwa Sh. 25,000. Haya ni mabweni ya wanafunzi, wanaingia na kutoka kila wakati, ni kwa nini mnaweka vitu duni wakati mnajua vitaharibika mapema? Maelekezo ya ununuzi wa serikali yakoje?" Alihoji.

Alipoulizwa wametumia utaratibu gani kununua vifaa hivyo, Mkuu wa Chuo Hamisi Njau, alisema walikuwa wakitumia kamati ya manunuzi ambayo mwenyekiti wake alikuwa ni Makamu Mkuu wa Chuo na Katibu wake ni Ofisa Manunuzi, ambaye ni Muyombo.

Muyombo alipoulizwa kama walikuwa wana orodha ya gharama za mahitaji kwa ajili ya ujenzi (BOQ) ambazo zilihitajika zinunuliwe iliyowaongoza kufanya manunuzi, alijibu kwamba haikuwapo.

Alisema walikuwa wakiorodhesha mahitaji yao na kuyapeleka kwa mhandisi.

Alipoambiwa aeleze tofauti ya vitasa vya kufunga mara tatu na vya kufunga mara moja Muyombo alijibu kwamba waliambiwa na mhandisi kwamba ndani ya kitasa kuna kibati ambacho kinatofautisha vitasa hivyo.

Waziri Mkuu alisema serikali inakataa udanganyifu kwenye manunuzi na haitavumilia watumishi wasiokuwa waaminifu. "Tena hili duka la huyo Kisaka ni la nguo wala siyo la vifaa vya ujenzi."

Alimwambia Mkuu wa Chuo, alipaswa kusimamia ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati unaofanyika chuoni hapo.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa Sh. bilioni 1.44 ili kukarabati chuo hicho kwenye maeneo ya utawala, kujifunzia, kumbi na mabweni ya wanachuo.

Awamu ya kwanza ya fedha hizo iliingia Novemba, 2017 na awamu ya pili ikawafikia Juni 2018.



Mwonekano mpya wa eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam, baada ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kuondoa wafanyabiashara kandokando ya barabara ya Morogoro ili kupisha upanuzi unaoendelea. **PICHA: SABATO**

# Biashara EAC yadaiwa kudorora

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

BIASHARA miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, (EAC) inazidi kushuka kutokana na uwapo wa vikwazo vya kibiashara ndani ya mipaka ya nchi wanachama.

Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) wametaka hali hiyo irekebishwe ili raia takribani 200 wa EAC waweze kufaidi matunda ya mtangamano.

Kwa mujibu wa ripoti ya Kamati ya Biashara na Uwekezaji ya EAC ya mwaka 2016, thamani ya biashara miongoni mwa nchi wanachama kwa mwaka huo, ilishuka kutoka dola bilioni 3.2 mwaka 2015 hadi kufikia dola bilioni 2.6 ambayo ni sawa na pungufu kwa asilimia 17.4.

Moja ya sababu zinazotajwa kuchangia kushuka kwa biashara katika ripoti hiyo ni pamoja na kuendelea kuwapo kwa vikwazo visivyo vya kodi au 'none tariff barriers' (NTBs).

Aidha, kukosekana kwa mifumo inayodhibiti ufanyaji biashara na nchi wanachama kushindwa, kukataa kuridhia mikataba ya biashara bila sababu yoyote ya msingi.

Wakichangia ripoti ya Kamati ya Biashara Mawasiliano na Uwekezaji ya EALA, kuhusu kuridhia kuanzishwa kwa kamati ya kushughulikia changamoto za kibiashara miongoni mwa wanachama wa EAC.

Baadhi ya wabunge walisema nchi wanachama zimejawa na hofu 'isiyofahamika' kuhusu mtangamano.

Mathias Kasamba kutoka Uganda alishangaa woga uliozigubika nchi wanachama wa jumuiya hiyo yenye wanachama sita.

Alisema hofu ndiyo inayochangia kuua jumuiya kwa kuwa unasababisha malengo ya waasisi wa EAC kufikiwa.

"Kuna woga wa kutekeleza maamuzi tunayojiwekea wenyewe kwa ajili ya manufaa ya watu wetu kwa sababu ambazo hata hazieleweki. Tunaogopana na tunashindwa hata kuridhia masuala tuliyokubaliana wenyewe kwa karibu miaka 10 na mambo yanaenda hivyo hivyo wakati watu wetu wanashindwa kushiriki kikamilifu katika mtangamano," alisema na kuongeza:

"Kwa mfano biashara kati ya Tanzania na Uganda imeshindwa kukua na inashuka kila kukicha. Kampuni 22 tu za Uganda ndiyo zilisajiliwa kuwekeza Tanzania ukilinganisha na kampuni 504 za Kenya zilizowekeza Tanzania.

Ni lazima turekebishe tofauti hizi kwa kuwashirikisha wananchi wetu," alisisitiza Mbunge Mathias Kasamba wa Uganda.

Mbunge Nsavyimana Sophie wa Burundi ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Biashara na Uwekezaji ya EALA, alielezea kushtushwa na ugumu wa mawasiliano baina ya sekretarieti na wizara husika katika nchi wanachama ambako huchukua muda mrefu bila sababu yoyote ya msingi.

Alisema ugumu huo wa mawasiliano ni moja ya urasimu unaokwamisha shughuli nyingi za Jumuiya kwa kuwa hakuna maamuzi ya haraka hasa ya kuondoa vikwazo huchukuliwa hata pale maamuzi na mapendekezo yanapokuwa yametolewa na vyombo vya juu.

Kwa upande wa Abdullah Makame wa Tanzania alitaka vikwazo vyote vinavyokwamisha biashara na utangamano wa watu wa Afrika Mashariki viondolewe haraka, ili kukamilisha ndoto ya waasisi waliotaka Jumuiya iwe ya watu.

## NBC yazindua klabu wafanyabiashara Singida

**Na Happy Severine, SINGIDA**

BENKI ya Taifa ya Biashara NBC imezindua klabu ya wafanyabiashara wa kati na wadogo mkoani Singida, ili kutengeneza uhusiano utakaowasaidia kuboresha biashara zao.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na wa kati (Head of SME), Evance Luhimbo, alisema kuwa klabu hiyo ya wafanyabiashara imehusisha wale wakubwa, wa kati na wadogo lengo ikiwa ni kutengeneza mfumo rafiki wa mafanikio baina ya wafanyabiashara hao na benki yao.

Lihombo alisema klabu hiyo itawaweka karibu wafanyabiashara na taasisi za kiserikali ikiwamo Mamlaka ya Mapato (Kodi), Bima na Brela katika ufuatiliaji wa leseni mbalimbali wanazohitaji.

"Ni matumaini yangu kuanzishwa kwa klabu hii ya wafanyabiashara wa Singida kutarahisisha mabadiliko ya haraka kibiashara pamoja hupatikanaji mwingine wa sekta zinazohusishwa na wafanya biashara," alisema Lihombo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Bravo Kizito, amewataka wafanyabiashara wote wa mkoa huo waliokuwapo kwenye klabu hiyo kuwa na umoja, upendo na mshikamano ili waweze kufika mbali kibiashara na kutimiza ndoto zao za mafanikio.

Kizito alisisitiza kuwa ni vyema wafanyabiashara wakaitumia benki ya NBC kwani kwa sasa huduma zao zimeboreshwa na zimekuwa rafiki kuliko benki zingine nchini, ambapo benki hiyo inajivunia kuwa na wafanyabiashara wanachama wanaonufaika.

Aidha, aliongeza kuwa kwa sasa Benki ya NBC inajivunia kuongeza vituo vya kutolea huduma mkoani Singida kwani kwa sasa vipo (16) ili kuwafikia watu wengi zaidi.

"Nawapongeza kwa kazi nzuri NBC, nawapongeza wafanyabiashara kwa kujiunga kwenye klabu hii, nampongeza Rais John Magufuli kwa juhudi zake kwa benki zetu za Tanzania kwani amekuwa mkombozi wetu hususani kwa wajasiriamali wadogo ili kufikia malengo yao na kuwa wafanyabiashara wakubwa hapo baadaye," Kizito.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara hao, Jonathan Mosses, alisema kuzinduliwa kwa klabu hiyo ya wafanyabiashara wa kati na wadogo kutasaidia kuamsha ari na juhudi za kupata maendeleo.

Mosses aliongeza kuwa ni imani yake wafanyabiashara wote ambao wako katika klabu hiyo wataweza kusaidia na kufikia malengo waliyonayo katika kukuza biashara zao.

# Lipumba ajutia mgogoro wa CUF

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MWENYEKITI wa CUF Taifa, Profesa Ibrahim Lipumba, amewakemea baadhi ya viongozi wa chama hicho ambao wanaendeleza migogoro, kutengeneza makundi, yasiyo na tija na kukigawa chama.

Profesa Lipumba aliyabainisha hayo jana alipozungumza na viongozi na wana-CUF wa Halmashauri za Mbogwe, Bukombe, Kahama Mji, Msalala na Ushetu katika kikao cha ndani na kusema, chama hakiwezi kuendeleza harakati kama kuna migogoro ya ndani na kwamba mtafaruku wa kisiasa ndani ya chama hicho umekidhoofisha.

Alisema mitafaruku iliyokuwapo ndani ya CUF iliwapotezea muda katika kukijenga chama na umewarudisha nyuma.

Aliwataka wanachama kujipanga upya na kuondoa makundi hali ambayo itawaletea ushindi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi ujao na mkuu wa 2020.

"Ndugu zangu, viongozi na wanachama, mgogoro uliokuwapo ndani ya CUF umetupotezea muda nami naufananisha na chuma kimepitishwa kwenye moto mkali na sasa kimekuwa ngangari kisiasa katika kuleta mabadiliko na kuhakikisha haki sawa kwa wote inapatikana," alisema Lipumba.

Mwenyekiti huyo aliongeza: "Pamoja na hali ngumu iliyopo ya kufanya shughuli za siasa nchini kwa vyama vya upinzani, lakini bado kuna fursa za kisiasa."

Alisema zipo fursa ndani ya chama na viongozi pamoja na wanachama wanatakiwa kujiunga pamoja kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

Hata hivyo Profesa Lipumba, alisema ni lazima kuwahamasisha kinamama na vijana wenye sifa za uongozi wajitokeze kwa wingi kugombania nafasi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Aliongeza kuwa ni muhimu ili kuondoa dhana kwenye jamii kuwa anayestahili kugombea nafasi hizo lazima awe mwanamume tu.

Pia aliwataka viongozi kuhakikisha wanaweka vijana au kinamama wenye sifa katika kugombea nafasi hizo na kuongeza vyama vyingi vimekuwa vikishindwa katika uchaguzi mbalimbali kutokana na kuweka wagombea wenye sifa mbaya kwenye jamii.

Kwa upande wake Katibu wa CUF wilayani Mbogwe, Stephan Masanja, alisema, atahakikisha chama chake kinashinda uchaguzi wa serikali za mitaa kutokana na kuwa na wagombea wenye sifa.

Aliongeza kuwa hataruhusu kuwapo makundi kwenye chama na atakayebainika kutengeneza makundi awajibike.



Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja wa Tigo, Mwangaza Matotola (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aonya wanafunzi kupeana mimba

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, amewaonya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuchana na kujiepusha na masuala ya mmomonyoko wa maadili vikiwamo vitendo vya ngono, vinavyosababisha kupeana mimba wao kwa wao.

Anamringi Macha, aliwaambia waache kujihusisha na vitendo vya ngono baina yao hali ambayo itawakwamisha kimasomo pale watakapoambukizwa maradhi na mabinti kubeba mimba.

Alisema kuwa baadhi ya vijana wamekuwa waoga kufanya ngono na wanafunzi kwa kuogopa kufungwa miaka 30 jela na badala yake wanafunzi wamekuwa wakifanya ngono wao kwa wao na mabinti kubeba mimba.

Mkuu wa Wilaya aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mtandao wa Fema Kanda ya Ziwa ambao utahusisha mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara na Shinyanga.

Aidha, itawajumuisha walimu wa shule za msingi na sekondari na wanafunzi wake.

"Siku moja nilikutana na mwanafunzi wa sekondari hospitali ya mji wa Kahama akiwa na mimba kubwa ambayo haiendani na umri wake, nikachukua hatua za kumpeleka polisi kutoa maelezo juu ya nani mhusika wa ujauzito huo, lakini cha kuchangaza alimtaja mwanafunzi mwenzake," alisema Macha.

Aidha, Macha aliwaonya mabinti kuwa kitu ambacho kinasababisha wanafunzi wengi kupata ujauzito ni tamaa na kumiliki mali na fedha.

Aliwaonya kuwa wanatamani simu janja wakingali akiwa bado shuleni, na kuwataka walimu kulisimamia na wakimbaini mwanafunzi anayemiliki simu achukulie hatua asingoje mpaka aharibike.

Macha aliwataka kuacha tabia ya kuwaomba lifti madereva pikipiki na kuwazoea wakati wanapokwenda shuleni.

Aliwaasa kusoma kwa bidii ili waweze kutimiza ndoto zao na kuongeza kuwa miaka ya sasa bila ya kuwa na elimu huwezi kupata ajira popote hata kujiajiri inakuwa ngumu.

Awali akisoma risala Katibu Mkuu Taifa wa Fema, Mwalimu Alex Mbatyani, alisema, ili kuondokana na janga la wanafunzi kuendelea kupata ujauzito Klabu za Fema zilizopo shuleni zinatoa elimu ya madhara ambayo hupatikana mwanafunzi anayejihusisha kwenye mahusiano wakati akiwa na umri mdogo.

Pia alisema kuwa, hutoa elimu ya kujitegemea juu ya kujishughulisha na kilimo, ufugaji na utunzaji wa mazingira wanafunzi wanapomaliza elimu yao ya darasa la saba ama kidato cha nne ikiwa ni pamoja na kuwasaidia watu wanaoishi na ulemavu, wazee na yatima pamoja na wahitaji kwa jumla.

# Takukuru yabaini ufisadi vifaranga vya samaki

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Kagera, imenusuru zaidi ya shilingi milioni 8.2 zilizokuwa zimefanyiwa njama za ubadhirifu wa upandikizaji wa vifaranga vya samaki katika Ziwa Rushwa lililoko wilayani Kyerwa.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Takukuru mkoani Kagera, John Joseph, baada ya Nipashe kutembelea katika ofisi hiyo ili kujua hali ya utendaji kazi kwa ufuatiliaji miradi ya kimaendeleo inayoendelea katika mkoa huo.

Joseph alisema kuwa taasisi ilifanikiwa kubaini njama za uhujumu mradi wa upandikizaji wa vifaranga vya samaki aina ya sato katika Ziwa Victoria kutoka kampuni ambayo haikutajwa Juni 26, mwaka huu.

Aidha, Joseph alisema mzabuni wa kampuni hiyo alipaswa kuwasilisha vifaranga 35,000 kwa gharama ya Sh. milioni 8,750,000 ambapo kila kifaranga kiliuzwa Sh. 250.

Alisema njama hiyo ilipangwa na baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyewa kwa ajili ya kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu kupitia upandikizaji wa samaki.

"Njama ilifanywa na watumishi wa halmashauri, nasi maofisa wa Takukuru tulipata taarifa na kuamua kufika katika ziwa hilo siku ya Septemba 21, mwaka huu, siku ambayo mzabuni alitaka kupandikiza vidaranga," alieleza Joseph.

"Baada ya taarifa hizo tulianza kuhakiki maboksi yaliyokuwa yameletwa na kutakiwa kufika ni 34, lakini kwa mshangao mkubwa ilibainika kuwamo vifanga 2,040 tu kwani kila boksi lilibainiwa kuwa na vifaranga 60 vyenye thamani halisi ya kifedha Sh. 5,100,000 wakati vilivyotakiwa ni 35,000," alisema Joseph.

Aliendelea kusema kuwa, baada ya uchunguzi huo maofisa walibaini kuwa kila boksi lilibeba vifaranga 1,030 na mzabuni kukiri kwamba alifikisha mzigo uliokamilika.

Alisema kuwa mzigo huo ulikuwa umebebwa katika mifuko ya plastiki katika vimiminika kwani halmashauri hiyo ilikuwa imeanzisha mchakato




Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakifakamia mishkaki iliyokuwa ikitembezwa kwa mkokoteni katika eneo la Posta Mpya jijini humo, wikiendi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waanza kufufua kilimo cha kahawa

**Na Ashton Balaigwa, MVOMERO**

WAKULIMA wa Tarafa ya Mgeta wilayani Mvomero mkoani Morogoro, wameanza kufufua kilimo cha kahawa kilichokuwa kikilimwa miaka ya nyuma na kuwa kama zao la biashara kwa kutumia kilimo hicho.

Kilimo cha kahawa katika Tarafa ya Mgeta kilikuwa maarufu katika miaka ya sabini, lakini kilikufa miaka ya 2000 baada ya wakulima wengi kukimbilia kulima kilimo cha kupata fedha za haraka tofauti na hicho ambacho kinachukua muda mrefu.

Akizungumza katika mafunzo ya ujasiriamali na kilimo cha kahawa kwa vikundi 35 vya kata za Bunduki na Bunduki, Diwani wa Bunduki, Prosper Mkunule, alisema kuwa wameshapanda miche 30,000 katika mashamba ya kata hizo mbili ikiwa ni mkakati wa kufanya zao hilo kuwa la biashara.

Diwani huyo alisema kilimo hicho cha kahawa kipindi cha nyuma kilikuwa kikisaidia kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji hivyo katika tarafa nzima ya Mgeta, hivyo kutokana na uharibifu na mabadiliko ya tabianchi, wameamua kukirudisha tena.

Alisema zao hilo lilipoteza umaarufu wake baada ya kuingia kilimo cha nyanya, kabichi na matunda ambapo vijana wengi waliamua kung'oa miti yake na kuanza kupanda mazao hayo ya nyanya na kabichi ili kupata fedha za haraka.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tanzania (CDTF), Henry Mgingi, alisema wameamua kusaidia kukirudisha kilimo cha kahawa katika Tarafa ya Mgeta ili kufanya kilimo endelevu na kupunguza kasi ya uchomaji moto unaosababisha uharibifu wa mazingira katika tarafa hiyo.

Alisema kwa kuanzia, wamegharamia kiasi cha Sh. milioni sita kwa ajili ya kuwapatia mafunzo vikundi 35 vya kata ya Mgeta na Bunduki ili kujua mbinu za kilimo hicho na shughuli za ujasiriamali zilizotolewa na wataalamu mbalimbali pamoja na kugharamia mbegu na miche ya vitalu ambavyo tayari vimeshapandwa.

Mgingi alisema CDTF kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TacRi), walitoa mbegu hizo pamoja na vifaa vya kilimo hicho katika vikundi ili kuanza kuzalisha vitalu.

Mwenyekiti wa kikundi cha Tugendelele, Stephen Msimbe, alisema baada ya kupatiwa mbegu na vifaa kutoka Taasisi hizo za TacRi na CDTF, wameshazalisha vitalu vyenye miche ambayo itagawanywa kwa wakulima wa tarafa waweze kupanda katika mashamba yao pamoja na mingine kugaiwa katika taasisi za serikali.

Mwenyekiti wa Bodi ya CDTF, Mhandisi Leon Msimbe, alisema wameamua kuunga mkono juhudi za serikali kwa kusaidia vikundi vya wakulima kuzalisha malighafi zinazotokana na zao la kilimo ikiwamo kahawa kwa ajili ya kusaidia uchumi wa viwanda.

## NMB yazindua huduma mpya ya kimtandao

**Na Mwandishi WETU**

BENKI ya NMB imezindua kampeni mpya ya dijitali katika kupata huduma za kibenki ijulikanayo kama NMB Mkononi, iliyotokana na kuunganishwa kwa huduma mbili za NMB Mobile na NMB KLiK.

Lengo la kuduma hiyo ni kuongeza ufanisi kwa watumiaji wa simu za mkononi.

Uzinduzi wa NMB Mkononi, ulifanyika jana Makao Makuu ya NMB, jijini Dar es Salaam, ambako ilielezwa kuwa huduma hiyo inalenga kuwahakikishia Watanzania wote fursa ya kushughulikia masuala ya kibenki kwa urahisi katika viganja vya mikono yao.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi huo, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara Ndogo na za Kati wa NMB, Filbert Mponzi, alisema benki yake ilikuwa na huduma za kibenki kwa njia ya simu, lakini imeona umuhimu wa kufanyia kazi mapendekezo ya wateja wao.

"Kwa kuwajali wateja wetu wengi, walioko nchi nzima mijini na vijijini, tukaona ni vema kuchukua mapendekezo yao ya kubadili NMB Mobile na NMB KLiK kuwa NMB Mkononi. Najua wapo watakaojiuliza kwa nini NMB Mkononi?

Mponzi alifafanua hilo na kuongeza maana yake ni benki katika mkono wako, ambako mteja anapata huduma zote za kibenki katika mkono wake, kupitia simu yake, wakati wowote, mahali popote kwa wepesi, urahisi na usalama.

"Kwa kuwa kipaumbele chetu kikuu ni kuwasaidia Watanzania wote, hata walioko vijijini, kutumia lugha wanayoielewa, tukaona ni vizuri tuje na 'brand name' ambayo itawakilishwa kwa Kiswahili na wateja wetu wataona urahisi wa kuijua na kuitumia huduma hiyo," alisisitiza.

Mponzi alizitaja baadhi ya huduma zinazoweza kupatikana kupitia NMB Mkononi kuwa ni pamoja na kufungua akaunti ya benki hiyo, kutuma na kupokea pesa, kutoa pesa bila kadi ya ATM, kuhamisha pesa kutoka benki moja kwenda nyingine, kulipia bili, tozo na kodi mbalimbali za serikali.

Aidha, alibainisha kuwa maboresho hayo ya kihuduma, yataongeza mtazamo chanya wa NMB katika kukuza uwezo na nguvu ya huduma za kifedha zinazotolewa na benki hiyo, ikiwa ni sehemu ya kusherehekea Wiki ya Huduma kwa Wateja chini ya kaulimbiu yao ya Ubora Uko Hapa!

NMB Mkononi inatarajiwa kufanya mapinduzi chanya katika kuongeza idadi ya wateja NMB, kutoka milioni 3.5 wa sasa. Benki hiyo pia ina matawi 230 kote nchini, ikiwa na mawakala zaidi ya 7000 na mashine za kutolea fedha (ATM) 800.

## Kortini tuhuma kubaka mtoto

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MKAZI wa Kijiji cha Kalenge Wilaya ya Uvinza, Dastan Elia (40), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya Mkoa wa Kigoma kwa kosa la kumbaka mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi saba na kumsababishia maumivu makali.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Eva Mushi, na aliposomewa shtaka lake alikana kuhusika na kosa hilo na yuko ndani katika mahabusu ya Gereza la Bangwe kwa kukosa wadhamini.

Hakimu Mushi aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo kuwa awe na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa afisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni mbili.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Edina Makala, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo namba 98/2019 umekamilika na kuomba mahakama hiyo kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kumtaka wakili huyo wa Serikali amsomee mshtakakiwa huyo maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Makala alidai kuwa Julai 5, mwaka huu majira ya asubuhi katika Kijiji cha Kalenge Wilaya ya Uvinza, mshtakiwa alimbaka mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi saba na kumsababishia maumivu makali.

Makala alidai siku ya tukio watoto walikuwa wakicheza mshtakiwa huyo aliwafata na kuwafukuza na baada ya kuwafukuza watoto hao walitawanyika na baada ya watoto hao kutawanyika mshtakiwa aliingia ndani ya nyumba na kumbaka mtoto msichana mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi saba.

Alidai wakati mshtakiwa huyo wakati anaendelea kumbaka mtoto huyo ambaye jina lake limehifadhiwa, aliingia dada wa mtoto huyo mwenye umri wa miaka 5 na kukuta mshtakiwa akifanya kitendo hicho, na baada ya kuona, alikimbia kwa jirani na kumwambia kuwa mdogo wake anabakwa na mshtakiwa huyo.

Aidha aliendelea kudai kuwa jirani huyo aliwaita majirani wengine na kwenda kumchukua mtoto huyo na damu zikiwa zinatoka sehemu zake za siri na kumpeleka kituo cha polisi Kazuramimba, na walipofika walipewa PF 3 kisha kumpeleka Zahanati ya Kazuramimba na daktari alipofamnyia uchunguzi, alibaini kuwa alibakwa.

Aidha alisema upande wa Mashtaka unatarajia kupeleka hapo mahakamani mashahidi 10 na vielelezo 3.

Baada ya Wakili wa Serikali kumaliza kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali aliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi katika kesi hiyo.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 15 mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi katika kesi hiyo.

# Wataalamu wa mifugo wastaafu wapata fursa

**Na Moshi Lusonzo**

SERIKALI imeanza mchakato wa kuwatambua na kuwaingiza katika kanzi data wataalamu wote wa mifugo waliostaafu kwa ajili ya kuwapeleka katika vyuo mbalimbali nchini kuwapa uzoefu wanafunzi wanaosomea fani hiyo.

Akizungumza na viongozi, wataalamu wastaafu na wadau wa mifugo jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema mpango huo utasaidia wataalamu hao kuendelea kutoa mchango wao katika sekta hiyo ili kufikia lengo sekta hiyo kuchangia pato la taifa kwa asilimia 25 mwaka 2025 kutoka 7.9 ya sasa.

Alisema wizara yake imeandaa kanzi data kwa ajili ya kuwatambua wataalamu wote waliostaafu na itakapokamilika itawasambaza katika vyuo vyote vya kilimo kutoa elimu na uzoefu kwa wanafunzi, ili wapate uelewa mpana na hatimaye kufanya kazi kwa bidii kama serikali inavyotaka.

Alisema takwimu inaonyesha hadi mwaka huu nchi nzima kuna maofisa ugani 3,735 pekee ambao hawalingani na idadi ya mifugo iliyopo nchini ambao ni ng'ombe milioni 30, samaki milioni 32, mbuzi milioni 10 na kuku zaidi ya milioni 70.

"Serikali inatambua mchango wa wataalamu wa kilimo waliostaafu waliojitoa kwa nchi yao, lakini tumeona haitoshi waendelee kukaa nao huko nje, tumeamua kwa makusudi kuwaingiza katika mpango wa maboresho ya vyuo vyetu ili waende huko wakatoe elimu yao na uzoefu kwa vijana wanaosomea fani hii muhimu," alisema Prof. Ole Gabriel.

Alisema wakati mpango huo unafanyiwa kazi, wizara hiyo inaendelea kukutana na wadau mbalimbali wa mifugo kuangalia namna ya kufanya sekta hiyo ichangie vya kutosha ukuaji wa uchumi wa viwanda.

"Sekta ya mifugo unahusika kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa viwanda kutokana na kutoa malighafi nyingi, tunataka kuona viwanda vyote vinavyozalisha bidhaa inayotokana na mifugo wanapata malighafi zao hapahapa nchini na hapo tutakuza ajira na uchumi wa watu wetu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wastaafu hao, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Rasilimali (TIB), Maria Mshingo, aliishukuru serikali kwa kuanzisha mpango huo kwani utawasaidia wao kuendelea kuitumikia nchi yao.

"Wenzetu katika nchi nyingine wamekuwa na mpango huu siku nyingi, wastaafu wamekuwa wakitoa ushauri na kuwapa uzoefu wanafunzi katika vyuo tofauti ili kuwaongezea uwelewa. Mimi naamini tukipangiwa kwenda huko sekta hii itakuwa na mwelekeo mzuri na italeta tija kwa nchi yetu," alisema Mashingo.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akikwepa matope na takataka zilizosambaa baada ya mvua kunyesha katika eneo la Mabibo jijini humo, jana. **PICHA; MIRAJI MSALA**

# UDSM kukilea Chuo cha Madini Dodoma

**Na Gwamaka Alipipi**

IDADI ya wataalamu wa madini nchini inatarajia kuongozeka baada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kuingia mkataba na Chuo cha Madini Dodoma wa kukilea kitaaluma.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini wa mkataba huo jana, jijini Dar es Salaam, Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. Willium Anangisye, alisema hatua ya Chuo cha Madini Dodoma kulelewa na UDSM kitawasaidia kupata fursa ya kukua na kuingia katika wigo mpana wa kitaaluma.

"Sisi UDSM tunagusa nyanja nyingi za kitaaluma ikiwamo taaluma ya madini, idara yetu ya Jiolojia imetoa wataalamu wanaoheshimika duniani na imekuwa na mchango mkubwa sana kitaifa, hivyo ninawahakikishia mpo katika mikono salama," alisema Prof. Anangisye.

Aliongeza kuwa UDSM kina uzoefu wa kulea vyuo vingine kwa miaka mingi, hivyo chuo hicho kitakuwa katika mikono salama ya kulelewa kitaaluma.

"Wanafunzi wa Chuo cha Madini Dodoma wote watahitimu wakiwa na viwango bora, tutaangalia viwango vya walimu, kama wewe ni profesa utapaswa kutuletea machapisho yako, tutayapima, tusiporidhika nayo tutakushusha kama hutaki tutakuondoa," alisema Prof. Anangisye.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Prof. Saimon Msanjila, alisema mchakato wa kukiweka Chuo cha Madini Dodoma kulelewa na UDSM ulianza muda mrefu, lakini ulikuwa unakwamishwa na masuala mbalimbali.

"Mwaka 2003 ulikwama, mwaka 2007 ukakwama tena, mwaka 2019 tukasema lazima ufanyike na suala la chuo kulelewa siyo geni duniani, hakuna chuo kilichoanza chenyewe," alisema Prof. Msanjila.

Alisema hatua ya UDSM kukilea Chuo cha Madini Dodoma itasaidia kukuza mitaala, miundombinu pamoja na uwezo wa wanafunzi hali itakayoongeza idadi kubwa ya wataalamu wa madini nchini.

"Wafanyakazi wa Chuo cha Madini hakuna atakayepoteza kazi, kwa wale watakaoondolewa kwa kutokuwa na sifa nitawachukua mimi na kuwapa kazi wizarani kwa maana nina kazi nyingi sana pale," alisema Prof. Msanjila.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alisema: "Ninawahakikishia, Chuo cha Madini Dodoma kitapata malezi bora, mtapata ujuzi ulio bora katika sekta ya madini."

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 8, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 19


**Chuo cha Utumishi wa Umma kinavyoendeleza ndoto za JPM**

Ukurasa 18


Pundamilia wa ajabu aliyepatikana Kenya sasa amehamia Tanzania


Ukurasa 17

## Uwajibikaji huu alianza nao Mwalimu Nyerere



# Mwanafunzi miaka 13 avumbua mfumo rahisi katika kujifunzia

Ukurasa 16

ELIMU KUTOKA POLISI

# Tanzania bila ya dawa za kulevya inawezekana -2



IGP Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**

***WIKI iliyopita tuliwaletea sehemu ya kwanza wa mada hii kuhusiana na tatizo la dawa za kulevya nchini linavyoendelea kuathiri taifa na jamii kiujumla.***

TUKAONA kwamba kosa la dawa za kulevya ni miongoni mwa makosa ya jinai ambalo kisheria limekuwa likipewa mtazamo wa kipekee kulingana na athari zake kijamii na kitaifa.

Tuliishia kwenye kipengele cha mikakati ya kijamii ambayo ni pamoja na kuimarika kwa mfumo wa utoaji taarifa kutoka kwa jamii husika kutokana na uhamasishaji na uelimishaji kuhusu athari za dawa za kulevya, unaotolewa na Jeshi la Polisi pamoja na wadau wake.

Endelea katika sehemu hii ya pili na ya mwisho ya mada hii:

**MIKAKATI KITAIFA**

Kutungwa kwa sheria mpya Na 5 ya mwaka 2015 ambayo imefanya baadhi ya marekebisho katika sheria ya zamani wa kuweza kuziba mianya na mapungufu yote ambayo wahalifu wamekuwa wakiitumia katika kukwepa mkono wa sheria.

Kuundwa kwa Mamlaka Ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ambayo imepewa nguvu ya kukamata, kupeleleza, kukusanya taarifa za uhalifu na wahalifu wa dawa za kulevya, hivyo kusaidia Jeshi la Polisi na taasisi nyingine zisizo za kiserikali zinazojihusisha katika kupambana na uhalifu huu katika kupunguza kasi za ongezeko la tatizo.

Wizara ya Afya kama Wizara simamizi katika kutibu, kuratibu na kutoa ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa za kulevya imeruhusu na kuendelea kutengeneza mazingira mazuri kwa wadau wa taasisi binafsi, mashirika ya dini na wananchi wenyewe kuanzisha vituo vya kulelea waathirika wa dawa za kulevya (sober houses) kwa gharama ndogo ambazo familia au jamii wanaweza kuwapeleka waathirika hao kwa tiba na ushauri nasaha.

Serikali ikisaidiana na taasisi za kidini zimesaidia katika kulibeba jukumu hili kwa kusaidia katika uelimishaji, utoaji wa misaada mbalimbali na utoaji ushauri kwa waathirika wa dawa za kulevya kwa kuwatengenezea mazingira bora ya kuweza kuachana na vitendo vya kihalifu na kufuata maagizo ya Mwenyezi Mungu.

Serikali ya Tanzania bado imeendelea kuboresha mahusiano yake kitaifa, kikanda na kimataifa, ikizingatia kuwa vita ya dawa za kulevya si ya kuimaliza kwa nchi pekee pasipo ushirikiano na nchi mbalimbali.

Hivyo Tanzania bado ni mwanachama hai katika jumuiya za SARPCCO, EAPCCO, SADC, INTERPOL na taasisi nyingine za kigeni, ambapo imekuwa ikishiriki katika, mafunzo, mikutano, Semina, kongamano na operesheni mbalimbali zinazofanywa kwa pamoja na jumuiya hizo.

**WITO WA JESHI LA POLISI KWA JAMII**

Jeshi la Polisi Tanzania linaamini kuwa pamoja na kwamba tatizo la dawa za kulevya ni la dunia nzima, Tanzania kama taifa huru lenye wananchi wenye mapenzi mema na nchi yao, wanalo jukumu la pamoja kwa kuunganisha nguvu za pamoja baina ya viongozi, taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla katika kuzuia na kupunguza tatizo hili, kwa kushirikiana na vyombo vya dola katika kutokomeza tatizo hili pasipo kushurutishwa.

***Imetolewa na:***
***Ofisi ya Uhusiano***
***Makao Makuu ya Polisi.***
***S.L.P. 9141,***
***DAR ES SALALAAM***



TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Kiswahili chapendwa duniani

"BURA yangu sibadili kwa rehani." Maana yake langu nalithamini hata kama kwa wengine halina thamani.

Wakati baadhi ya Watanzania hawathamini lugha yetu ya taifa, mataifa kadhaa duniani yanairai* Tanzania iwapelekee walimu wa Kiswahili.*Rai ni kitendo cha kumwambia mtu maneno mazuri au kumtendea mema ili akubali kutekeleza haja fulani.

Marekani ya Kaskazini, nchi kadha wa kadha* za Ulaya Magharibi na Afrika zinaiomba Tanzania iwapelekee walimu wa Kiswahili. Hata hivyo wakalimani* wengi walio nchi za nje wanatoka Kenya, sio Tanzania! Penye miti hapana wajenzi!

*Kadha (nomino) ni tamko linalotumiwa kutaja jambo lisiloainishwa bayana: Watu kadha walihudhuria mkutano. Msemo: Nimejia kadha, sikujia kadha wa kadha. Maana yake nimefika kwa ajili ya masuala fulani mahususi wala si kwa shughuli nyingine.

'Kadha wa kadha' ni ibada ya faradhi inayotekelezwa baada ya kupita wakati wake. 'Kadhaa' (kivumishi) a kiasi/idadi maalumu; haja aliyokuwa nayo mtu; matakwa, mahitaji.

'Kadhi' ni hakimu wa Kiislamu anayehukumu kwa kufuata sheria. 'Kadhia' ni jambo lililojiri; tukio la kuhuzunisha. 'Kadhibisha' ni kitendo cha kukanusha ukweli wa jambo.

*Wakalimani (mmoja aitwa mkalimani) ni watu wanaofasiri maelezo ya lugha moja kwa lugha nyingine; mtapta/watapta; mtarijumani/watarijumani.

Baadhi ya nchi za Mashariki kama Urusi kuna vitabu vinavyoeleza maana ya maneno ya Kirusi kwa Kiswahili. Mfano: Panidyelynik/Jumatatu; Ftornik/Jumanne; Srida/Jumatano; Chitvyerk/Alhamisi; Pyatnista/Ijumaa; Subota/Jumamosi na Vaskrisyenye/Jumapili.

Kinachosikitisha ni kwamba wakati lugha ya Kiswahili inathaminiwa na mataifa mengine yaliyoendelea kuliko Tanzania, sisi twatumia maneno ya kihuni yanayozungumzwa mitaani!

Mfano: "Samatta shangwe kama lote." Hiki ni kichwa cha habari kwenye gazeti la michezo. "Kama lote" maana yake nini?

Hata hivyo, "Ukuchapao (ukupigao) ndio ukufunzao." Maana yake unajifunza jambo baada ya mchapo huo.

Methali hii yaweza kutumiwa kumshauri mtu anayelalamika baada ya kufikwa na jambo fulani. Anapaswa kujua kuwa mtu hujifunza kutokana na shida iliyompata au adhabu aliyopewa. Ni dhahiri kama walivyosema wahenga kuwa "Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Twafunzwa kuvitegemea vitu vyetu wala sio vya watu wengine.

Sasa soma baadhi ya maneno yatumiwayo na magazeti ya michezo nchini. "Azam ni mzuka kama wote." Maana sahihi ya 'mzuka' ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na huweza kumtokea mtu; pepo.

Maana nyingine ya 'pepo' ni mahali panapoaminiwa kuwa Mungu atawaweka wale waliotenda mema ili waishi milele kwa raha na starehe baada ya kuwafufua na kuwahukumu; paradiso, edeni, janna, firdausi.

'Kama' ni kitendo cha kutoa maziwa kutoka kwenye kiwele; ushanga; mfano wa. Maana ya 'ote' ni bila ya kubakia. Waandishi wanapoandika "Azam ni mzuka kama wote" wana maana gani?

"Kocha mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera ana mambo nyie, jana buana ametamka maneno mazito juu ya straika wake, David Molinga akidai eti kama asipofunga mabao 15 hadi 20, yupo radhi akatwe mkono au kulipa faini ya Dola 1,000 (zaidi ya Sh2 mil)."

Waandishi wanapaswa kutambua na kutofautisha maneno ya mazungumzo na yanayoandikwa. Pia watambue matumizi ya maneno ya wakati uliopita, uliopo na ujao.

"Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera ana mambo nyie" ni maneno ya mazungumzo si ya kuandikwa. "Jana (wakati uliopita) "buana ametamka. Ingeandikwa 'jana alitamka.' 'Buana' ni maneno ya waandishi badala ya 'bwana' ambalo ndilo neno halisi na sahihi. Ukiwauliza, wanasema "lugha inakua!"

Kama ndivyo, mbona nchi haiandikwi na kutamkwa 'inchi?' 'Nchi' ni sehemu ya ardhi ambayo haikufunikwa na maji; bara. Sehemu ya ardhi ambayo imegawanywa kwa mipaka ya kisiasa na inayotambulika kwa jina la taifa lake. 'Inchi' ni sehemu moja ya kumi na mbili ya futi moja, urefu unaokaribia sentimeta 2.5.

Ili nisipoteze muda kueleza mtiririko m-baya wa sentensi, nimeamua kuzungumzia maneno ya mwandishi kuhusu 'kukomaliza,' 'penzi' na 'kutinga.'

Sipati maana ya 'kukomaliza' kwani si neno la Kiswahili nijuacho. Badala ya neno hilo mwandishi angeandika 'komaa' lenye maana ya pevuka au iva, kwa mfano matunda, nafaka na mazao mengine. Pia kuwa mtu mzima, fikia umri wa kuzaa.

Ujumbe niliotumiwa: "Mzee Maro shikamoo. Mimi ni msomaji wako. Naomba kufahamu kipi sahihi wakati wa kujitambulisha. "Kwa jina naitwa Frank John Kimara" au "Kwa majina naitwa Frank John Kimara?" Natanguliza shukrani." (0754 378 887).

Jibu langu: Kwa nini kueleza maneno mengi? Sema "naitwa Frank John wa Kimara, inatosha. Wengine hukosea zaidi wanapojitambulisha kwa kusema: 'naitwa Bwana ...' ilhali wao ni wanaume!"

**Akanijibu: "Asante sana."**
**Methali: Upishi ni kuni.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

SAYANSI

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Dar es Salaam inahitaji mapafu ya uhakika ili ipumue vizuri

AWALI ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Dunia na vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.

Kipekee alituumba wanadamu tumiliki na kuvitawala vyote: majini, nchi kavu na angani.

Ndiyo maana baadhi ya mataifa yenye nguvu kiuchumi yanathubutu kwenda kuchunguza nini kilichopo katika anga.

Harakati zote hizo ni katika kutafuta kumiliki na kutawala: wamefika kwenye Mwezi wakaona nini kinajiri huko.

Bado wanakazana kufika kwenye sayari nyingine kama Mars na Jupiter na nyinginezo nyingi.

Hakika Mungu ni mwenye nguvu na wa ajabu. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu alipomuumba binadamu na akamuweka duniani kuwa mmiliki na mtawala wa vyote vilivyomo; alihakikisha binadamu ataendelea kuishi kwa kuvuta hewa safi oksijeni (oxygen-O2) na kutoa gesiukaa (carbon dioxide-CO2).

Huo ndio msingi wa uhai wetu kupitia kupumua na mengine yakifuata (chakula, mavazi, nyumba na kadhalika). Kisayansi tunafahamu kuwa gesi aina ya natrojeni (nitrogen) inachukua sehemu kubwa katika hewa kwa asilimia 78 wakati gesi aina ya oksijeni ni karibu asilimia 21 ya gesi zote angani.

Vilevile, kuna gesi aina ya "argon" kwa asilimia 0.93 na gesiukaa (CO2) asilimia 0.04, lakini pia kuna vigesi vingine pamoja na unyevunyevu (water vapour) kwa asilimia 0.03.

Kadhalika Mwenyezi Mungu aliweka misitu na mimea mbalimbali kwa makusudi ili tuendelee kupata oksijeni ya kutosha na wakati huohuo gesiukaa ikibakia kwenye viwango visivyoleta madhara kwa binadamu na wanyama wengine.

Hali hiyo inamaanisha nini kwetu sisi binadamu? Kiuhalisia misitu, miti na mimea mingine juu ya ardhi na ndani ya maji (aquatic plants and other living organisms) ndiyo mitambo asilia ya kutengeneza oksijeni na kufyonza gesiukaa kuitoa angani na kuihifadhi kwa usalama wetu.

Misitu, miti na mimea huota na kukua na katika kufanya hivyo kunahitajika maji na virutubisho mbalimbali vinavyopatikana kwenye udongo lakini pia kuwapo gesiukaa na nguvu ya jua.

Katika mchakato huo ndipo gesiukaa, ambayo ikiachiwa ikaongezeka sana kwenye mfumo mzima wa hewa angani, inasababisha madhara kwetu sisi binadamu lakini pia kwa viumbehai wengine kutokana na kuongezeka joto duniani na hivyo kupelekea mabadiliko ya tabianchi (temperature rise and climate change).

Kimsingi gesiukaa inatumiwa na mimea katika mchakato wa kutayarisha chakula kwa mchanganyiko wa maji na virutubisho vingine (kutoka kwenye udongo wenye rutuba ya kutosha) na kwa msaada wa nguvu ya jua hutengeneza chakula kinachohitajika kwa miti na mimea kukua.




Msitu wa Kazimzumbwi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

> Kwa miaka ya hivi karibuni, Jiji la Dar-es-Salaam limekuwa na magari mengi yanayotumia muda mwingi barabarani kutokana na foleni kuwa ndefu kupita kiasi.

Ni katika utaratibu huo unaowezesha misitu, miti na mimea kutoa (release) gesi aina ya oksijeni na kuiongeza kwenye mfumo wa hewa angani. Kwa maneno mengine: misitu, miti na mimea mingine juu ya nchi na majini; hutusaidia kuondoa gesiukaa hewani na kuingiza gesi safi ya oksijeni ambayo tunahitaji sana kwa uhai na maisha yetu wa kila situ.

Iwapo Mwenyezi Mungu aliumba dunia tunapoishi akaweka kiwango cha gesiukaa cha chini sana kiasi cha kutoleta madhara kwa binadamu na viumbe wengine, je ongezeko la gesiukaa (zaidi ya asilimia 0.04) kwenye mfumo wa hewa angani linasababishwa na nini?

Kusema kweli dunia sasa imesheheni watu wengi sasa zaidi ya bilioni saba (7) na China ikiwa na zaidi ya watu bilioni 1.4 wakati India ikiwa na zaidi ya bilioni 1.3 bilioni.

Bara la Afrika sasa kina watu zaidi ya bilioni 1.3. Kutokana na ongezeko kubwa la binadamu duniani pamoja na kiu ya kujitafutia maendeleo; shughuli nyingi kupitia mikono ya binadamu zikapelekea kuzalisha gesiukaa nyingi kupita kiasi.

Isitoshe dunia imeendelea kupoteza misitu ya asili kwa kasi kubwa kutokana na shughuli za kilimo au ufugaji zisizo endelevu na pia kuchoma moto misitu na mapori kiholela.

Shughuli za viwandani na majumbani na katika maeneo ya biashara ikiwa ni pamoja na masuala ya usafiri hasa katika Majiji na Miji, zimeshamiri sana na kusababisha ongezeko kubwa kwa gesiukaa (CO2) angani.

Kwa majiji kama Dar-es-Salaam ambayo yana idadi kubwa ya watu na hali ya mazingira yake kuchafuliwa na gesiukaa na aina nyingine za gesi kama methane, ethanol na nyinginezo; kutokana na shughuli za viwandani, nyumbani na usafirishaji: kunahitajika "MAPAFU" ya kutusaidia kupumua vizuri.

Mathalani, kama kutakuwepo na miti mingi na maeneo yenye misitu iliyohifadhiwa na kutunzwa ipasavyo katika Jiji la Dar-es-Salaam na viunga vyake; hali hiyo itasaidia sana kuleta unafuu kwenye mfumo wa gesi angani.

Kwa miaka ya hivi karibuni, Jiji la Dar-es-Salaam limekuwa na magari mengi yanayotumia muda mwingi barabarani kutokana na foleni kuwa ndefu kupita kiasi.

Hali hiyo imekuwa chanzo kikubwa cha kuchafua mazingira (environmental pollution) katika Jiji la Dar-es-Salaam na viunga vyake. Madhara yake ni makubwa hasa kiafya kwa sababu ya kuendelea kuvuta gesi zisizofaa kwa uhai wa binadamu na viumbe wengine.

Kwa kuwepo na misitu na kupanda miti ya kutosha kwenye sehemu tunazoishi (urban tree planting) na kutunza maeneo yenye misitu ya asili, kutasaidia kupunguza gesiukaa angani kwa manufaa ya afya zetu.

Kwa kuzingatia hilo, taasisi isiyo ya kiserikali ya Uhifadhi na Utunzaji wa Maliasili na Mazingira (Wildlife Conservation Society of Tanzania-WCST); inatoa wito kwa wadau, taasisi za sekta binafsi na za umma, mashirika na wadau wetu katika maendeleo (development partners) kuwa wakati ni sasa wa kuchukua hatua za kimkakati kuhakikisha kunakuwapo na Dar-es-Salaam ya kijani yenye maeneo ya misitu ya asili itakayokuwa ni mapafu ya jiji.

Manispaa zote ziweke mpango mahsusi kuwezesha kila anayepewa kiwanja apande miti miwili, mitatu au zaidi katika eneo lake.

Wataalam wa misitu, kilimo na mazingira washauri ni aina gani za miti inayofaa kwa mazingira ya Dar-es-Salaam.

Angalizo ni kupata miti mizuri (ornamental trees) pamoja na kufyonza gesiukaa na kutupatia oksijeni, iweze kutoa kivuli kwa ajili ya kuboresha hali mahalia (ameliorate microclimate) hasa nyakati za jua kali. Vilevile, miti ya matunda itafaa sana kuongeza lishe kupitia matunda pia kuboresha mazingira.

Pamoja na kupanda miti, tujitahidi kusimamia na kutunza maeneo yenye misitu ya asili kama Pugu na Kazimzumbwi, Vikindu na Pande ili maeneo hayo yaweze kuwa kichocheo cha kupunguza gesiukaa kwenye anga la Jiji la Dar-Es-Salaam na viunga vyake na wakati huohuo kuendelea kutoa gesi ya oksijeni kuboresha afya zetu.

Nichukue fursa hii kuwaomba wadau wote hususani Marafiki wa Pugu na Kazimzumbwi "Friends of Pugu & Kazimzumbwi" kwa pamoja tuhakikishe maeneo hayo yaliyohifadhiwa kisheria tangu 1954 yanaendela kuwanufaisha wakazi wa Jiji la Dar-es-Salaam.

Hakuna lisilowezekana, tutimize wajibu wetu na penye nia pana njia, tutafanikiwa Mwenyezi Mungu atusaidie.

***Mwandishi ni Mwenyekiti wa WCST, anapatikana kupitia fkilahama@gmail.com; +255756007400; +255714250050***

UVUMBUZI

**NA BEATRICE PHILEMON**

# Mwanafunzi miaka 13 avumbua mfumo rahisi katika kujifunzia

• Unaitwa 'Test Yourself App' • Hakuna haja wanafunzi kubeba mabegi yaliyojaa vitabu • Unapunguza matumizi ya chaki....



Moses Mbaga (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wenzake, uongozi wa shule na mgeni rasmi Dk. Charles Msonde (waliokaa wa pili kushoto),mara baada ya Mahafali ya wanafunzi wa darasa la saba katika shule ya msingi Montessori Msimbazi Centre. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**

UBORA wa elimu una mahitaji mengi kutoka kwenye miundombinu ya shule iliyo katika viwango kwa maana ya madarasa, maktaba, maabara, vyoo, nyumba bora za walimu na walimu wenye sifa stahiki katika masomo yanayofundishwa.

Aidha, elimu bora inahitaji upatikanaji wa kuridhisha wa vifaa vya kufundishia ikiwa ni pamoja na vitabu vya ziada na kiada, mbao za kuandikia zenye viwango, chaki, madawati, samani kwa ajili ya walimu na vingine vyenye mchango madhubuti.

Lakini unahitaji wanafunzi walio tayari kupokea taaluma na fursa ya kupata mahitaji ya kimasomo kurahisisha ujifunzaji wao bla kusahau maslahi ya walimu.

Katika mchakato wote wa kuwa na wanafunzi walio na taaluma stahiki, sayansi na teknolojia inaendelea kuwa na mchango wake katika sekta ya elimu kuanzia kwenye miundombinu ya shule, walimu na pia kwa wanafunzi.

Kwa mfano sayansi na teknolojia inaendelea kuja na vifaa bora zaidi kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia ambapo sasa kuna 'power point' badala ya ubao wa kuandikia kwa chaki na zana zingine mbalimbali katika dhima nzima ya kuboresha mazingira ya utoaji wa taaluma.

Katika mlolongo huo huo wa kuweka mazingira bora ya utoaji wa taaluma katika zama hizi za sayansi na teknolojia, mwanafunzi mwenye umri wa miaka 13 ameweka historia kwa shule yake na wanafunzi wenzake ya kuja na uvumbuzi.

Mwanafunzi huyo, Moses Mbaga, amefaulu kutengeneza mfumo (APP) utakaosaidia walimu kuandaa notisi na wanafunzi wakaweza kuzisoma mtandaoni (online).

Mwanafunzi huyo ambaye ni mhitimu wa Darasa la Saba kwenye Shule ya Msingi Montessori, Msimbazi Centre iliyo wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam anauita uvumbuzi wake huo 'Test Yourself App'.

Akizungumza na mwandishi wa Makala haya, Mbaga anabainisha lengo la uvumbuzi wake kuwa ni pamoja na kupunguza ubebaji wa madaftari kwa wanafunzi.

"Kupitia uvumbuzi huu, mwanafunzi hahitaji kubeba begi lenye lundo la daftari, kwani akishaingia mtandaoni, kwa mujibu wa ratiba ya masomo yake kwa siku hiyo, atayakuta tayari yameshawekwa na walimu wake," anasema na kuongeza:

"Hivyo yeye ni kusoma hizo notisi zilizowekwa na mwalimu, na kama kuna maswali kuyajibu kupitia mtandaoni, ambapo mwalimu atasahihisha na kama kuna makosa yatarekebishwa."

> "Mbaga aliniandikia barua na kunieleza kuwa ametengeneza mfumo wake (App hiyo), hivyo anahitaji mitihani ya miaka ya nyuma aweze kuiweka katika APP yake hiyo (Test Yourself App).

Mbali na kupunguza mzigo wa kubeba madaftari, Mbaga anasema uvumbuzi huo unapunguza pia matumizi ya chaki kwa upande wa walimu.

"Mwalimu hahitaji tena kwenda darasani kwenye ubao kuandika notisi na chaki, ni kuingiza notisi za somo lake, maswali, majaribio ama kazi za nyumbani kwenye mtandao, ambapo mwanafunzi anaweza kuingia na kuzifikia na pia kufanya kazi zake alizomwachia," anasema.

Lakini lengo la tatu la uvumbuzi wake huo, anasema Mbaga ni la kuwezesha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kwa watoto wa shule za msingi.

### WAZO LILIWEZEKANAJE?

Mwanafunzi huyu anasema ameweza kutengeneza mfumo huu kutokana na kufundishwa somo la Tehama shuleni kwake lakini na hamasa yake ya kujisomea kozi mbalimbali mtandaoni.

"Aidha, kama nilivyosema hapo juu baada ya kuona wanafunzi wanapata shida kubeba mabegi yaliyojaa daftari na vitabu kwenda na kurudi kutoka shuleni," anasema na kuongeza:

"Lakini ukweli kwamba hivi sasa wanafunzi wanaweza kusoma mtandaoni kutokana na maendeleo makubwa ya Tehama shuleni kwetu na katika shule zingine hapa nchini."

'Mvumbuzi' huyu anamshuru mwalimu wake wa ICT, Ayub Iddi na kaka yake Tito Mbaga kwa kumhamasisha hadi akafikia ngazi hiyo ya uvumbuzi.

Anabainisha kwamba, alianza kutengeneza APP yake hiyo mwezi Juni 2018.



Moses mbaga (aliyekaa) akiwa darasani katika shule ya msingi Montessori Msimbazi Centre, akionyesha waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali jinsi APP yake inavyofanya kazi.

### UTAMBULISHO WA UVUMBUZI

Mbaga anasema tayari ameshafika Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) kuonyesha APP yake kwa Katibu Mkuu Mtendaji, Dk. Charles Msonde na Mkurugenzi wa ICT wa NECTA, Dk. Joseph Mbowe ambao walimshauri aongeze vitu vingine ili kuiboresha zaidi.

"Natarajia kuzindua uvumbuzi wangu mwishoni mwa mwaka huu endapo nitakuwa nimetimiza matakwa ya NECTA, ili wanafunzi na walimu wa shule za msingi, waanze kuutumia mfumo huu," anasema.

### MTUMIAJI

'Mtaalam' huyu anabainisha kwamba

ili mwanafunzi atumie APP hii, anatakiwa awe na akaunti ili aingie kuona notisi za masomo, majaribio, mitihani, matokeo ya majibu ya maswali aliyoyafanya na pale alipokosa.

"Kazi ya mwalimu katika mfumo huu ni kuingiza masomo, maswali na kusahihisha na kazi ya mwanafunzi ni kuchagua masomo, kufanya mitihani, kupata majibu ya mitihani na masahihisho," anasema.

Anawashukuru wazazi wake kwa kumuunga mkono kwa kiasi kikubwa kwani kila alipotaka kusoma kozi za mtandaoni, baba yake alimlipia gharama zote zilizokuwa zinatakiwa.

### MIPANGO YAKE YA BAADAYE

Mbaga anasema ana mpango kuisadia Tanzania kiteknolojia, ili iwe katika viwango vya juu kimataifa.

"Nawasihi vijana kuwa wabunifu, wafikirie mambo makubwa kwa maendeleo ya Tanzania kama ilivyo kwa nchi zingine," anasema.

### NECTA

Katika halfa ya kuaga wanafunzi wa Darasa la Saba kwenye shule hiyo ya Msingi ya Montessori Msimbazi Centre, Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Msonde anaweka wazi juu ya uvumbuzi huo na jinsi kama NECTA, walivyoupokea.

Dk. Msonde anasema Mbaga ndiye aliyemvutia kwenda kwenye shule hiyo kushiriki hafla hiyo ya kuhitimu darasa la saba kwa sababu ya mshangao mkubwa alioupata kufuatia uvumbuzi huo.

"Kwa sababu sijawahi kuona mwanafunzi wa shule ya msingi hata wa kidato cha sita aliyeweza kuniandikia barua ya kuja kuniona ofisini kwangu, lakini Mbaga ameweza kufanya hivyo," anasema na kuongeza:

"Mbaga aliniandikia barua na kunieleza kuwa ametengeneza mfumo wake (App hiyo), hivyo anahitaji mitihani ya miaka ya nyuma aweze kuiweka katika APP yake hiyo (Test Yourself App).

Dk. Msonde anasema baada ya kuisoma barua yake, waliimuita kwenye ofisi za Baraza ili awaeleze mwenyewe kuhusu mfumo wake kwa lengo la kuthibitisha kama kweli ni wa kwake ama ametengenezewa na mtu mwingine.

Anabainisha mbali na yeye, Mbaga alifanikiwa kukutana na Dk. Mbowe anayeongoza zaidi ya watalaam 30 wa Tehama katika Baraza na kuwaonyesha App yake.

Anasema alichokiwakilisha ni kipaji cha aina yake, uthubutu na kwamba hicho ndicho walichoangalia kwa ngazi yake, kwani ni kitu kikubwa sana.

Anabainisha, walipima pia uwezo wake wa utambuzi (IQ).

"Baada ya kutuonyesha hatua kwa hatua tulithibitisha kuwa ni mfumo wake na tukamuelekeza maeneo ya kuiboresha ili baadaye iweze kutumiwa na wanafunzi na walimu wa shule za misingi," anasema na kuongeza:

"Kama tuna vipaji kama hivi kwa nini visiendelezwe?"anahoji.

Dk. Msonde anasema anaunga mkono vilevile kusikia kuwa Mbaga ameanza kufundisha wanafunzi wenzake.

"Haya waliyojifunza pamoja na Tehama, naomba wazazi muwe pamoja na watoto ili waweze kutimiza ndoto zao, msiwaache kuwaongoza na Mungu atawabariki,"anasema.

MWALIMU WA TEHAMA

Akimzungumzia Mbaga, Mwalimu Iddi ambaye anafundisha Tehama katika shule hiyo anasema wao kama shule wamempa msingi wa masuala ya kompyuta na kumsimamia hasa katika mahitaji yanayohitajika ngazi ya msingi.

"Masuala ya Tehama yana wigo mpana sana, tulikuwa tunamwongoza na tukagundua kipaji chake akiwa darasa la tatu...aliniambia katika darasa hilo kuwa

ana Tablet," anasema na kuongeza:

"Akaniomba barua pepe (email) yangu na kwamba niwe namtumia kazi zake au majaribio yake ya nyumbani kwenye barua pepe (email) yake."

Mwalimu Iddi anasema mwanafunzi huyo alimwambia kwamba anapotumia tablet inamuokolea muda na kuwa hata na muda wa kwenda mahali kumtembelea jamaa na kujisomea.

"Aidha, akiwa darasa hilo la tatu, Mbaga alianza kuniandikia barua pepe ya kuomba kazi zake za shule au nyumbani, kitu ambacho kilinishangaza sana kuona mtoto mdogo anaweza kuandika barua pepe, na ndipo nilianza kutambua kipaji chake," anasema.

Shule ya msingi Montessori Msimbazi Centre inafundisha elimu ya Tehama kuanzia darasa la kwanza hadi darasa la saba.

### MZAZI

Rodgers Mbaga ni mzazi wa 'mtaalamu' huyu. Anasema kuwa mtoto wake alianza kuonyesha kipaji cha pekee tangu akiwa na umri mdogo wa miaka mitatu.

Anabainisha wakati huo akiwa mdogo na hajui kusoma, aliweza kutumia simu ya aina yeyote kiasi cha kuingia kwenye michezo ya simu (games) ndani ya muda mfupi.

"Hili liliwashangaza wengi, hasa majirani...katika umri huo aliweza kusaidia familia na majirani walipopata changamoto yeyote inayotokana na matumizi ya simu janja (smartphones).

"Alikuwa mdadisi kiasi kwamba, nilipomnunulia midoli (toys) hakumaliza siku nzima, lazima ataivunja kwa nia ya kujua linafanyaje kazi au ndani kuna nini," anasema na kuongeza:

"Mara kadhaa nilimwadhibu kwa kumuona ni mharibifu wa vitu, kumbe sikujua alikuwa anajifunza jambo...

baada ya kujua kusoma na kuandika, aliweza kujifunza kutumia kompyuta kwa kipindi kifupi."

Anasema baada ya kujua matumizi ya kompyuta aliweza kujifunza vitu vingi mtandaoni.

Mzazi huyo anafafanua tayari mwanaye anavyo vyeti kadhaa baada ya kufuzu kozi mbalimbali alizozifanya mtandaoni.

"Mapema mwaka jana, alianza kutengeneza tovuti (website) na hatimaye mwaka huu akaanza kutengeneza mobile apps, na kwa sasa ndio anakamilisha kuboresha app yake kwa ajili ya kuwawezesha watoto wa shule za msingi kufanya mitihani mbalimbali ili kuboresha uwezo wao kielimu.

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Uwajibikaji huu alianza nao Mwalimu Nyerere

**Na Nickolaus Kasera**

JUMANNE wiki iliyopita, sehemu ya kwanza ya safu hii ilijikita kuelimisha kuhusu uwajibikaji, ikiwa na marejeo maalum ya kinachofanywa na asasi za kiraia, kupitia mifumo inayoitwa; Pets na Sam.

Kwa kukumbusha, Pets (Public Expenditure Tracking System), maana yake ni mfumo wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma kuanzia zinakotoka, hapo ikiwa ni ngazi zote za serikali, mashirika binafsi, michango ya wananchi na misaada, hadi mtumiaji wa mwisho ambaye ni mwananchi.

Kwa ujumla, ni aina ya nyenzo inayotumika kufuatilia rasilimali katika ngazi mbalimbali. Narudia katika Sam (Social Accountability Monitoring); inaangukia kwenye tafsiri ya ufuatiliaji wa uwajibikaji kijamii. Hiyo ni kati ya zana za ufuatiliaji na usimamizi wa rasilimali za umma, inayosisitiza misingi au kanuni za haki katika utoaji huduma za kijamii.

Wiki hii ni mwezi tunapoadhimisha miaka 20 tangu kuondokewa na muasisi wa Taifa, Rais wa Kwanza wa Jamhuri la Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere. Tunapenda kujikita zaidi kwenye umuhimu wa ushirikiano baina ya asasi za kiraia na taasisi zinazotambulika kisheria, mathalan Takukuru, Jeshi La Polisi na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Wadau wote kwa kauli moja, wanakubaliana kwamba kasi ilikufa na kupungua. Vita dhidi ya rushwa na kuimarisha uwajibikaji ni sharti la kuwapo utashi wa kisiasa.

Kwenye hili la utashi wa siasa, Tanzania chini ya serikali ya Rais John Magufuli, imeonyesha kwa vitendo kwamba haitawavumilia watendaji pekee, ila wote watakaojihusisha na vitendo vinavyokiuka maadili.

Takukuru wao wana Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu yaTatu (2017 – 2022). Mkakati huo umeainisha ari ya Watanzania kupambana na rushwa na uhitaji wa ushirikiano wa wadau.

Ni dhahiri kwamba taasisi ya Wajibu Institute of Public Accountability, imejikita kwenye uwajibikaji, eneo ambalo ni kinga madhubuti dhidi ya upotevu wa rasilimali taifa. Ni tatizo ambalo Mwalimu Nyerere siyo tu aliyaona, bali aliyakemea kwa nguvu zote.

Leo tukimkumbuka Hayati Mwalimu Nyerere ni muhimu tukumbuke utashi aliyouanzisha wa kisiasa ya kuchukia, kukemea na kukataa rushwa za aina zote kwenye jamii ya Watanzania.

Utashi huo wa awamu ya kwanza, umekuwa chachu kwa kiongozi wa sasa Rais Dk. Magufuli, ambaye hajasita kuonyesha namna ufisadi unaweza kuangamiza ndoto ya mamilioni ya Watanzania wa leo na vizazi vijavyo.

Sheikh Mohammed Bin Rashid Al Makhtoum Mfalme wa Mfalme wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), amechapisha kitabu chake kiitwacho 'My Story' kilichonikumbusha jitihada za Rais Dk. Magufuli kukabiliana na janga la ukosefu wa uwajibikaji.



Hayati Mwalimu Julius Nyerere, katika zama zake za uongozi. **PICHA: MAKTABA**

Al Makhtoum ana namna ya kutafsiri isiyo rasmi kwamba: "Ufisadi ni adui wa maendeleo. Tusingefika hapa tulipo ndani ya miaka 50, bila ya utashi wa kisiasa na kufanya maamuzi magumu, sio tu kutamani maendeleo, pia kuyafanyia kazi maendeleo yenyewe."

Ni mara ngapi umesikia matamshi haya kutoka kwa Rais Dk. Magufuli? Malengo ya maendeleo yetu hayawezi kufikiwa, bila ya ushirikiano ya wadau, matumizi ya teknolojia ya habari na uwapo wa mfumo wa elimu unaokuza maadili, kuanzia shule za msingi hadi ngazi ya vyuo vikuu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wajibu Institute of Public Accountability, Ludovick Utouh, analieleza hilo kupitia ufafanuzi kwamba hatuna budi kumshukuru Rais kwa utashi huu wa kisiasa, ambayo ndiyo chachu kuu ya kuhakikisha uwajibikaji unakuwa mkakati endelevu kitaifa ya kuhakikisha maendeleo endelevu yanapatika kwa Watanzania wote.

Tuna mengi ya kujifunza kutoka UAE, kupitia kitabu kilichotungwa na mfalme wao, kina kurasa kadhaa muhimu, tutafakari tunakoelekea na tuwajibike ipasavyo.

**Kwa mawasiliano: samawatiarts@yahoo.com**

JE, WAJUA?

# Pundamilia wa ajabu aliyepatikana Kenya sasa amehamia Tanzania



Pundamilia wa ajabu aliyeonekana Kenya kwenye Mbuga ya Mara amehamia Tanzania, kwenye Mbuga ya Wanyama ya Taifa ya Serengeti. **PICHA: MTANDAO.**

PUNDAMILIA wa ajabu ambaye hivi karibuni alionekana katika mbuga ya wanyama ya Mara nchini Kenya, amevuka mpaka na kuingia ndani ya Mbuga ya Wanyama ya Taifa ya Serengeti.

Amevuka mpaka pamoja na pundamilia wengine waliokuwa wanahama wakichanganyika na Nyumbu, limeripoti gazeti la Nation nchini Kenya.

Kinyume na pundamilia wengine wenye mistari, kwenye ngozi yake pundamilia huyo ana madoadoa meupe na mistari michache myeupe inayofifia mwilini mwake, jambo lililomfanya kuwa ni wa kipekee.

Taarifa ya kuhamia kwake nchini Tanzania imethibitishwa na makumi ya watalii na walinzi wa mbuga za wanyama pamoja na katibu wa shirika la madereva wa magari ya utalii nchini Kenya, Felix Migoya.

Migoya amesema kuwa pundamilia huyo mchanga mwenye umri wa mwezi mmoja hivi, kwa sasa yuko katika eneo la Kaskazini mwa Mbuga ya Wanyama ya Serengeti.

Alipinga taarifa za uvumi kwamba kivutio hicho kipya cha utalii katika Mbuga ya Wanyama ya Mara, kilikamatwa na kufungiwa ili kihifadhiwe mahali pake kama ilivyoelezwa katika mitandao ya habari ya kijamii katika kipindi cha wiki tatu zilizopota, Linaripoti gazeti la Daily Nation la nchini humo.

"Taarifa za mitandao ya kijamii ni feki, pundamilia anayeonyeshwa kwenye mitandao ya kijamii ni mkubwa na alikamatwa nchini Afrika Kusini katika tarehe ambayo haijulikani, miaka kadhaa iliyopita," anasema Migoya.

Wazazi wa pundamilia huyo mchanga wako katika kipindi cha mwaka cha kuhama kwa zaidi ya mamilioni ya nyumbu baina ya Mbuga ya Wanyama ya Serengeti na Hifadhi ya Wanyama ya Maasai Mara, tukio ambalo huwavutia watalii kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Tukio hilo, ambalo liliwekwa katika orodha ya "Maajabu Saba ya Dunia," kwa kawaida huanza katikati ya mwezi Juni hadi mwezi Oktoba.

Katika kipindi hiki, nyumbu hukutana kabla ya kufanya safari yao ya kurejea sambamba na mamia ya pundamilia, swala na wanyama wengine wanaotafuta malisho.

Pundamilia huyu wa ajabu mweusi kwa mara ya kwanza aligunduliwa na kupigwa picha mapema mwezi Septemba karibu na mto Mara na Antony Tira, mwongozaji maarufu wa safari za watalii kutoka kabila la Wamasai na alimpiga picha hiyo katika kambi ya utalii ya Matira Bush, iliyopo ndani ya mbuga ya wanyama.

Tira alimuita pundamilia huyo mchanga jina la baba yake 'Tira.'

**UTAMBULISHO WAKE**

Si mweusi kabisa, na kutokana na utofauti wa ngozi yake katika sehemu mbalimbali za mwili wake, rangi yake, pundamilia huyo amekuwa maarufu ghafla na amekuwa kivutio cha watalii katika mbuga ya Mara.

Migoya anasema, huenda sasa watalii wakaelekea Serengeti kwani watu wengi wanamfuata kiumbe huyo wa ajabu.

Tangu mpigapicha Tira alipotuma picha ya pundamilia huyo na kuwaalika watu kuja kumuona, watu wengi wamekuwa wakiongezeka katika hifadhi ya wanyama ya Mara na kusababisha 'msongamano' mkubwa wa watu katika hifadhi hiyo. **BBC**

RIPOTI

## Utafiti mpya gumzo athari za kiafya za ulaji nyama

UTAFITI wenye utata unasema kupunguza kula nyama, soseji, nyama ya kusagwa ni kupoteza wakati kwa watu wengi.

Utafiti huo ambao unatofautiana na tafiti za awali zilizofanywa na mashirika makubwa duniani, unasema kuna ushahidi mdogo kwamba ulaji wa nyama husababisha athari za kiafya.

Baadhi ya wataalamu wamepongeza "utafiti" huo, lakini wengine wanahofia huenda "ukawaweka watu hatarini"

Kula zaidi ya vipande vinne vya nyama zilizopitia viwandani zaidi ya mara nne kwa wiki ni hatari, ulibaini uchunguzi wa awali uliofanywa miongoni mwa watu 1,000 nchini Ufaransa, na kuchapishwa kwenye Jarida la Thorax.

Watafiti wanaamini kuwa huenda sababu ya matatizo hayo ikawa ni matumizi ya kemikali ya nitrite, inayowekwa kwenye nyama hizo kuzizuia kuoza ambayo hutumiwa kwenye vyakula kama Soseji, na samaki (salami).

Lakini wataalam wanasema kuwa uhusiano wa hatari hizo haujaidhinishwa, na uchunguzi zaidi unahitajika kufanyika kuthibitisha hilo. Ulaji nyama kupita kiasi umetajwa kuwa chanzo cha saratani ya utumbo.

Shirika la Kimataifa linalofanya utafiti wa saratani liligonga vichwa vya habari wakati liliposema kuwa nyama husababisha saratani. Pia lilisema kuwa nyama nyekundu huenda ikasababisha magonjwa, lakini hakuna ushahidi wa kutosha.

**SASA SWALI ULAJI NYAMA NI HATARI KWA AFYA?**

Nchini Uingereza pekee inaaminika kuwa nyama iliyohifadhiwa kwa kemikali, huchangia visa 5,400 ya saratani ya utumbo kila mwaka.

Pia ulaji wa nyama ya aina hiyo umehusishwa na kisukari aina ya pili. Makubaliano ya kisayansi ni kwamba kula sana nyama ni mbaya kwa afya yako.

**UTAFITI UNASEMA NINI?**

Watafiti wanaoongozwa na Vyuo vikuu vya Dalhousie na McMaster nchini Canada, walichunguza ushahidi ulioangaziwa na watafiti wa awali.

Matokeo ya utafiti uliochapishwa katika Jarida la kimatibabu la Annals of Internal Medicine, unaashiria kwamba ikiwa watu 1,000 watapunguza kula kiwango cha nyama wanachokula kila wiki, yatakayotokea ni kwamba:

Katika maisha yao, kutakuwa na vifo vichache vinavyotokana na ugonjwa wa saratani. Kwamba kwa miaka 11 kutakuwa na vifo vichache vitakavyotokana na maradhi ya moyo.

**UTAFITI HUO KIMSINGI UMEPOKELEWAJE?**

Kevin McConway, Profesa wa takwimu zilizotumika katika Chuo Kikuu cha Open, aliuta utafiti huo kuwa "sehemu kamili ya kazi"

Naye Profesa David Spiegelhalter, kutoka Chuo Kikuu cha Cambridge, anasema:

"Uhakiki huu wa kina bado haujapata ushahidi mzuri wa faida muhimu za kiafya, zinazotokana na kupunguza ulaji nyama…kwa kweli, hakupatikani ushahidi wowote mzuri."

Lakini badala ya kuwa na hofu juu ya ulaji wa aina moja ya chakula, watu wanapaswa kula vyakula vyenye virutubisho vya kiafya na vya aina mbalimbali, wanashauri wataalam.

Wataalam wanasema watu wanapaswa kula nyama nyekundu si zaidi ya gramu 70 kwa siku, ama kiwango hicho hicho cha nyama iliyopitia viwandani kwa ajili ya kuwa na afya bora.

Kiwango hiki ni sawa na takriban Soseji moja ama vipande viwili vya nyama kwa siku. **BBC**



ELIMU

## NA MANENO SELANYIKA

# Chuo cha Utumishi wa Umma kinavyoendeleza ndoto za JPM

MWANZONI mwa mwezi ujao, Rais John Magufuli atakuwa anaadhimisha miaka minne tangu aingie madarakani, mwishoni mwa mwaka 2015.

Ndani ya kipindi hicho cha miezi 48, Rais Magufuli, maarufu JPM, amefanya mengi kuonyesha dira ya Tanzania mpya yenye mwelekeo wa uchumi wa viwanda ili kutimiza lengo la kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Taasisi za umma ndizo zimebeba ajenda hiyo kwa kuhakikisha zinatoa huduma kwa wananchi katika mchakato huo wa kufikia malengo hayo muhimu ya kiuchumi.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) ambacho uongozi wake unaeleza kuwa umedhamiria kuiunga mkono serikali kufikia malengo yake kwa kutoa elimu bora kwa watendaji wa umma.

Mkuu wa chuo hicho, Dk. Emmanuel Shindika, anasema kimepanuka kutokana na kuboreshwa kwa vitendea kazi na kuongeza idadi ya kozi, huku idadi ya wanafunzi nayo ikiongezeka.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPSC, Dk. Emmanuel Shindika. **PICHA: MTANDAO**

Kwa mujibu wa Dk. Shindika, kozi zitolewazo na chuo hicho ni Utunzaji Kumbukumbu na Nyaraka inayotolewa katika matawi ya Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya. Kuna kozi ya Uhazili (Secretarial) inayotolewa katika matawi ya Dar es Salaam na Tabora.

Kozi nyingine ni Rasilimaliwatu ambayo inatolewa katika matawi ya Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya. Pia kuna kozi za Utawala wa Umma inayotolewa (Mtwara, Singida na Tanga), Ununuzi na Ugavi (Tanga) na Utawala wa Serikali za Mitaa (Mbeya).

Dk. Shindika anasema chuo pia kinatoa mafunzo katika ngazi ya shahada ya kwanza katika fani za Uhazili na Menejimenti ya Utunzaji Kumbukumbu na Nyaraka katika tawi lake la Dar es Salaam.

"Watumishi wa umma na wananchi wenye sifa za kujiunga na kozi ya shahada katika kozi za Uhazili na Menejimenti ya Utunzaji Kumbukumbu na Nyaraka, wajiunge na kozi hizi kwa ngazi hiyo... chuo kimepanuka na kimeboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji," anasema.

Kutokana na uwekezaji mkubwa ambao serikali imeufanya katika maeneo ya rasilimali watu na vifaa, Dk. Shindika anasema anaamini chuo sasa kina nafasi kubwa ya kuiwezesha serikali kufikia malengo yake ya kutoa elimu bora na kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati unaochagizwa na viwanda.

"Tuna nafasi ya kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya viwanda na yenye uchumi wa kati kwa kufundisha watumishi wa umma mafunzo ya muda mfupi na mrefu," anasema.

Mkuu huyo wa chuo anasema TPSC imekuwa ikitoa mafunzo kwa watumishi wa umma kutoka taasisi mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi wao mahali pa kazi.

Anasema chuo kimeweka jitihada kubwa katika kutekeleza kazi za msingi ili kuendana na dira na dhamira yake pamoja na utekelezaji wa malengo ya serikali.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Dk. Shindika anabainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia 2014/15 hadi 2018/19, chuo kilitoa mafunzo maalum ya muda mfupi na mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi wa umma.

"Lengo ni kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi," anasema.

Anabainisha kwamba, chuo kikitumiwa na watumishi wa umma ipasavyo, kitasaidia katika kuboresha ufanisi kwenye maeneo ya kazi kwa kuwa kimejikita zaidi katika mafunzo ya vitendo, hivyo kumwezesha mhitimu kuwa na uwezo kiutendaji.

"Hiki ni chuo cha kitaaluma, kinahimiza zaidi mafunzo kwa vitendo, watumishi wa umma wanaopitia hapa, uwezo wao kiutendaji ni mkubwa," Dk. Shindika anatamba.

Anasema iwapo waajiri watawapeleka watumishi wao kwa wingi katika chuo hicho, serikali itakuwa na uhakika wa maeneo mengi ya kazi kuwa na huduma zinazotolewa kwa ufanisi na tija.

**WITO**

Anatoa wito kwa taasisi mbalimbali za umma na hata sekta binafsi kukitumia chuo hicho kupeleka watumishi ili wajengewe uwezo na kuongeza ufanisi sehemu za kazi na hivyo kutoa huduma bora kwa umma.

"Ni muhimu sana kwa taasisi za umma nchini kuwaleta watumishi wao wapya hapa kwetu kujifunza namna ya uendeshaji wa ofisi, utunzaji kumbukumbu, sheria na taratibu za utumishi wa umma," anasema na kuongeza:

"Lakainai vilevile namna ya kukabiliana na changamoto za kiutumishi hasa kwa kasi ya mabadiliko ya kiuchumi."

Dk. Shindika anfafanua kuwa katika mafunzo yatolewayo na chuo hicho, yapo yanayowalenga watumishi wa serikali walioko kwenye ngazi za mwanzo, za kati na za juu katika fani za uongozi (nadharia na vitendo).

Vilevile utawala na mafunzo ya ukarani kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

**MAFANIKIO**

Dk. Shindika anayataja mafanikio ya chuo hicho kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa matawi manne kutoka mawili mwaka 2000 hadi kufikia sita hadi mwaka 2017.

"Chuo kilipoanza kilikuwa na tawi la Tabora na Dar es Salaam pekee, lakini hadi sasa tumeongeza matawi mengine manne ambayo ni Singida, Mbeya, Tanga na Mtwara," anasema na kuongeza:

> Kisha kupewa Mitihani ya kuwapima ili kuona kama wanafaa kupanda vyeo, mfano, maofisa utumishi na makatibu muhtasi.

"Chuo kinajipanga kuyaimarisha matawi yake yote ili kutoa elimu katika mazingira bora zaidi."

Mkuu huyo wa chuo anataja mafanikio mengine kuwa ni utoaji wa mafunzo ya muda mfupi, ushauri wa kitaalamu na kufanya utafiti kwa taasisi za umma na binafsi katika maeneo ya uongozi, menejimenti na utawala.

"Pia tumefanikiwa kusimamia na kuendesha mitihani ya watumishi wa umma (Public Service Examinations) ambapo kada mbalimbali za utumishi hupimwa kwa kupewa mitihani baada ya kufundishwa chuoni," anasema na kuongeza:

"Kisha kupewa Mitihani ya kuwapima ili kuona kama wanafaa kupanda vyeo, mfano, maofisa utumishi na makatibu muhtasi."

Mafanikio mengine anayoyataja mkuu huyo wa chuo kuwa ni utoaji na usimamizi wa elimu bora ya vitendo kwa wahitimu yenye kuwajengea uwezo wa kiushindani katika soko la ajira la sasa. Mengine anayataja kuwa ni ukarabati wa majengo ya tawi la Dar es Salaam na ujenzi wa jengo jipya tawi la Tabora.

Serikali imekuwa ikiwaasa wakurugenzi wa halmashauri nchini kuwapeleka watumishi wao katika chuo hicho ili wapigwe msasa na kwenda sanjari na kasi ya mabadiliko katika sekta ya utumishi wa umma nchini na duniani.


***Mwandishi anapatikana kupitia 0786461073***



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

JUMATATU ijayo (Oktoba 14) ni Maadhimisho ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere. Wadau wajadili mchango wake kwenye sekta ya elimu nchini.



### NEMES TEMBA (M/KITI WA CHAMA CHA WATU WENYE UALBINO

NINAMKUMBUKA Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa mengi aliyofanya kwa nia njema ya kulijenga taifa letu.

Nikijikita kwenye sekta ya elimu, ambayo kimsingi ndiyo moyo wa ustawi na maendeleo kwa nchi yeyote duniani; Nazitazama kauli za mwalimu, hasa katika hotuba aliyoitoa Machi 5, 1999 wakati wa kupokea Shahada ya Heshima ya Udaktari (Doctor of Letters) kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Katika hotuba hiyo alizungumzia suala la elimu ambapo alisema: Kwanza, elimu yetu iwe ni kwa wote. Kama elimu yetu ya msingi haitakuwa kwa wote, basi watakaoikosa zaidi watakuwa wasichana.

Kila mtoto katika nchi hii awe wa kiume au wa kike lazima apate kiwango cha chini cha elimu kama haki yake. Mfumo wa sasa wa miaka miwili (2) ya elimu ya awali na miaka saba ya elimu ya msingi kwa maoni yangu una mantiki na unawezekana.

Tutaongeza kiwango kadri uwezo wetu utakavyokuwa unaongezeka. Mwalimu aliipenda na kuitetea elimu. Alipenda watu wote wapate elimu. Alizingatia jinsi na jinsia katika utoaji wa elimu. Alipenda kuitazama Tanzania yenye wasomi waadilifu na wajenzi wa taifa kwa kutumia stadi walizopata katika mchakato mzima wa kujifunza.

Pili, elimu yetu haina budi kuwa bora. Hasa elimu ya msingi lazima iwe ni nzuri sana; kwa sababu hii ndiyo elimu rasmi pekee, ambayo Watanzania wengi wanaweza kuipata.

Hivi sasa ubora wa elimu yetu ya msingi unatisha kabisa. Hatuna budi kuchukua hatua kama jambo lenye umuhimu wa pekee kitaifa.



### DK. LUTGARD KAGARUKI (MKURUGENZI MTENDAJI WA CHAMA CHA KUDHIBITI TUMBAKU NCHINI)

KWANZA kabla ya yote niseme kwamba nitamuenzi milele Baba wa Taifa aendelee kupumzika kwa amani, amefanya makubwa sana kwa nchi hii kwamba hadi leo ninajivunia kuwa Mtanzania.

Aliwapenda sana Watanzania, aliwatumikia kwa moyo wote, hakuiba wala kufisadi na hakujilimbikizia mali. Alidumisha amani, uhuru wa kujieleza na kukusanyika. Alijenga viwanda ili vijana wapate ajira, wahuni wakavihujumu.

Lakini kwa kuwa unahitaji kujua sehemu moja tu ya elimu, basi niongeze kwa kusema kwamba nimesoma bure kuanzia elimu ya msingi.

Tulikuwa tunalipa kidogo, ila sekondari, chuo kikuu hadi masters (Shahada ya Umahiri) katika chuo cha hadhi huko Uingereza (London School of Hygiene & Tropical Medicine of the University of London); Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), tulipewa kila kitu ikiwamo malazi, chakula, vitabu pamoja na fedha za kujikimu.

Tumesoma kwa raha sana, tukitegemea vichwa vyetu na si fedha ya wazazi. Mtoto wa maskini na tajiri wote tulikuwa sawa.

Hivyo kwa upande wa elimu nitaendelea kumkumbuka sana mwalimu, ambaye kwa kweli amefanya makubwa kwenye elimu hasa kwa kuzingatia kwamba baada ya nchi kupata uhuru, alitangaza vita dhidi ya maadui watatu, ambao ni ujinga, maradhi na umaskini.

Akasema kwamba ili maadui wawili, maradhi na umaskini waondoke, ni lazima kwanza kumuondoa ujinga.



### MESHACK KAPANGE (KATIBU WA CHAMA CHA KUTETEA MASLAHI YA WALIMU)

HUWEZI kuzungumzia elimu ya Tanzania bila kumtaja Baba wa Taifa, kutokana na ukweli kwamba alijali elimu na alitaka Watanzania wote wapate elimu bora na jumuishi. Anajali elimu ya ufundi itakayowafanya Watanzania wawajibike na kuijenga Tanzania yao.

Na haya pia ndiyo yanayofanywa na Rais wa sasa John Magufuli, akiwa na kaulimbiu ya Tanzania ya Viwanda. Labda nikumbushe kwamba hili jina la Mwalimu halikuwa jina tu bali lilitokana na taaluma yake ya ualimu. Kimsingi elimu ni jambo ambalo alilipa kipaumbele sana.

Alifanya kila njia kuhakikisha watu wote wanapata elimu, kuanzia watoto hadi wakubwa. Alihakikisha anajenga mfumo wa elimu, uliotoa nafasi kwa mtu yeyote kulingana na uwezo wa akili yake, na hakuangalia tajiri au maskini bali wote walipata elimu hadi ngazi vya chuo kikuu.

Kikubwa ambacho alikuwa akiamini ni kwamba elimu ni haki ya kila mtu, na alitamani elimu iwe ni ya kumjenga mwanafunzi kuwa mdadisi wa mambo na mwenye kiu ya kutafuta elimu, na iwe nyenzo ya kumkomboa mwanadamu.

Alitamani elimu ijumuishe nadharia na vitendo, na ijenge tabia ya kushirikiana, si kushindana na ubinafsi. Alitaka wanafunzi shuleni wawe wanajishughulisha na kazi za mikono, ikiwamo kilimo, ufugaji na useremala.

Hiyo ilikuwa ni fursa ya kufahamu mambo mengi, ambayo hayapatikani darasani, kwani kazi za mikono alizichukulia kama njia moja ya shule kujenga msingi wa kujitegemea kwa mahitaji yake.



### MAGDALENA SAKAYA (MBUNGE WA KALIUA MKOANI TABORA)

TUNAPOJIANDAA kuadhimisha miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa letu, Mwalimu JK Nyerere, tunayo mengi ya kujivunia aliyoyafanya kwa nchi yetu. Mimi ninakumbuka mengi na msingi wa maendeleo ya taifa letu yamewekwa na yeye.

Kwanza amani umoja na mshikamano wa Watanzania ni tunu ya kwanza muhimu sana aliyotuachia Baba wa Taifa. Kitendo cha kutangaza kupambana na maadui watatu ujinga, umaskini na maradhi aliweka msingi wa maendeleo ya Tanzania.

Mwalimu alitaka Watanzania wasome, alianzisha shule za vipaji maalum, vyuo vya maendeleo ya jamii, ambavyo leo vingi vimegeuzwa malengo yake. Alianzisha vyuo vikuu vya kimkakati kama Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoa mitaala mbalimbali ikiwamo uhandisi na mingine mingi.

Aidha, kwa mtu mwenye umri mkubwa atakuwa anakumbuka kwamba Watanzania tulifundishwa na Baba wa Taifa kwamba elimu haina mwisho na ndio maana alituhimiza tujibidishe kwenye elimu. Katika hilo, alianzisha elimu ya watu wazima.

Kama unakumbuka, enzi hizo vijijini na mijini watu walihimizwa kusoma kisomo cha watu wazima ili wajiongezee elimu, kuanzia kujifunza kusoma na kuandika hadi kujipatia ujuzi na maarifa katika fani na taaluma mbalimbali.

Alianzisha elimu ya watu wazima baada ya kuona Watanzania wengi hawajui kusoma wala kuandika.



### BENJAMIN NKONYA (KATIBU MKUU CHAMA CHA WAMILIKI WA SHULE BINAFSI (TAMONGSCO)

TANZANIA ina historia ndefu kwenye lugha ya Kiswahili, kwani badala ya kutumia lugha za kigeni, nchi iliegemea katika Kiswahili.

Hizi zote zilikuwa jitihada za Mwalimu Nyerere ambaye hata wakati wa kampeni za Chama Cha Tanu, alitumia Kiswahili kwa ajili ya kuwaunganisha Watanganyika na hilo lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa, kwani wale ambao walikuwa hawajui lugha hii walijifunza na ndiyo pekee ambayo imesaidia kuiunganisha Tanzania yote yenye makabila zaidi ya 100.

Kwa hiyo unapozungumzia Mwalimu kwenye upande wa elimu, mimi ninasema kwamba amesaidia sana kuwaunganisha Watanzania kupitia lugha ya Kiswahili, ambayo sasa matumizi yake shuleni yameiletea Tanzania manufaa makubwa baadhi yake yakiwa ni kuwafanya wanafunzi wamudu vizuri masomo ya shule za msingi, kuunganisha Watanzania, ingawa hilo nimeshalisema.

Vilevile kuondoa migogoro ya kijamii itokanayo na ukabila na kuiletea Tanzania heshima kwa kuwa mwasisi wa lugha, ambayo sasa ni moja ya lugha kubwa za SADC na duniani kote. Miongoni mwa viongozi, ambao watakumbukwa kwa kuwa watetezi wa tamaduni, lugha na falsafa huru za Kiafrika, ni Baba wa Taifa, ambaye alikuwa akisisitiza matumizi ya Kiswahili kama lugha asilia, ambayo raia wa Tanganyika wakati huo walitakiwa kuitumia ili kuelewana ipasavyo.



## DC Mbarali ataka wananchi kutoisubiri serikali

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani wa Mbeya, Reuben Mfune, ametoa agizo kwa wananchi wote wilayani humo kuhakikisha wanashiriki kwenye ujenzi wa vituo vya afya badala ya kuendelea kuisubiri serikali.

Mfune alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki alidai kuwa wananchi wamekuwa wakitegea kukamilisha ujenzi wa vituo vyao vya afya wakiisubiri serikali jambo ambalo ni kunyume na utaratibu mpya ulianzishwa ambao unahimiza wananchi waanze na serikali inakuja kumalizia kuleta vifaa tiba, wataalamu na mambo mengine.

"Mambo mazuri yanakuja na kuhusiana na huduma za afya, anzisheni ujenzi wa vituo vya afya ili serikali ije iongeze nguvu, mkiisubiri serikali mtachelewa kujiletea maendeleo kwa sababu haiwezi kufanya kila kitu," alisema Mfune.

Pia alisema serikali kwa kutambua umuhimu wa huduma za afya wilayani Mbarali ilitenga fedha zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kujenga hospitali mpya ya kisasa ili wananchi wapate huduma za afya kwenye mazingira mazuri.

Vilevile, alisema serikali imekuwa ikiwasaidia wazee kwa kuhakikisha wanapata matibabu kwenye mazingira rafiki.

Alisema serikali inatoa gawio la fedha kupitia mradi wa TASAF ili waweze kujikimu na kwamba baadhi ya wazee wanatumia fedha hizo kuanzisha miradi, kama ujenzi wa nyumba, ufugaji na wengine wamezitumia kusomesha watoto.

Katibu wa Baraza la Wazee wilayani humo, Hezron Kapwela, alisema maeneo mengi hayana vituo vya afya na zahanati hali inayosababisha wazee kutembea umbali mrefu.

# Wapongeza kuanzishwa kituo waathirika dawa za kulevya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAATHIRIKA wa kutumia dawa za kulevya mkoani Mbeya wamepongeza jitihada za serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuanzisha Kituo cha Methadone katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya kwa kuwa kimesaidia kuboresha afya zao ikilinganishwa na ilivyokuwa awali.

Wakizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe waathirika hao walisema kuwa huduma hiyo imewasaidia kuondokana na matumizi ya dawa za kulevya na kwamba dawa za Methadone wanazipata bila gharama yoyote.

Miongoni mwa waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya, Atuganile Mwailenge, alisema tangu aanze kutumia dawa hizo zimemsaidia kuepukana na matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema amekuwa akihudhuria kila siku kuchukua dawa katika kituo hicho kilichopo katika Hospitali ya Rufani Kanda Mbeya na kwamba hadi sasa ameona mabadiliko makubwa.

Baraka Charles, alisema aliingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya baada ya kushawishiwa na marafiki zake, lakini bahati nzuri ndugu zake walimpeleka kwenye kituo hicho na kumsaidia kuacha na sasa afya yake imeimarika.

"Tunaishukuru serikali kwa kuanzisha kituo cha Methadone hapa Hospitali ya Rufani Kanda Mbeya kwa kweli kimekuwa msaada kwetu, tangu nianze kutumia afya yangu imeimarika na nzuri zaidi hizi dawa tunazipata bure kabisa nawasihi vijana wote ambao wameathirika na dawa za kulevya wafike kituo hiki waanze dozi," alisema Charles.

Daktari wa magonjwa ya akili katika hospitali hiyo, Stephano Mkakilwa, alisema watumiaji wa dawa za kulevya ambao tayari wamekwishaanza kutumia dozi ya methadone wasiache mpaka pale watakapopona kabisa.

Alisema dozi ya methadone haina muda maalum wa kutumia isipokuwa mwathirika anapaswa kuendelea kutumia mfululizo kwa kipindi cha miaka miwili. Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mbeya, Dk. Goodlove Mbwanji, alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 2017 na mpaka sasa kinahudumia waathirika 261 wa dawa za kulevya ambao kati yao wanawake tisa na wanaume 252.

Alisema licha ya kutoa huduma za methadone, pia hospitali ipo kwenye mikakati ya kufungua kituo kikubwa kinatachohusisha shughuli mbalimbali ikiwamo bustani na michezo.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Shigamba katika Halmashauri ya wilaya ya Mbeya, wakivuna zao la Pareto juzi, ambapo wanalalamikia soko kuwa baya kutokana na mnunuzi kuwa mmoja na hivyo kukosa ushindani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waomba kujengewa vituo vya afya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANANCHI wa Kata za Tembela na Mwasanga zilizopo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya wameiomba serikali kuwajengea vituo vya afya ili waondokane na changamoto ya kutembea umbali mrefu na gharama kubwa kufuata huduma za matibabu Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Waliyasema hayo jana walipozungumza na Nipashe kuhusu upatikanaji wa huduma za afya katika kata hizo kutokana na jiografia zake kuelekea msimu wa mvua. Walisema wamekuwa wakipata adha ya kusafiri kufuata huduma za afya maeneo mengine kutokana na kata zao kutokuwa na vituo vya afya na kuiomba serikali kuwaunga mkono kumalizia ujenzi kwa kuwa tayari walionyesha jitihada.

Miongoni mwa wananchi wa Kata ya Tembela, Faida Mkola, alisema walikubaliana kujenga kituo cha afya na tayari walianza ujenzi, lakini changamoto iliyopo ni ukata wa fedha hivyo wanaiomba serikali iwaunge mkono.

"Sisi wananchi tunaoishi pembezoni kila jambo tunakuwa wa mwisho kulipata, hadi sasa hatuna kituo cha afya licha ya kuonyesha jitihada za kujenga, lakini hatujaungwa mkono na serikali badala yake tunatumia muda mrefu kufuata huduma za matibabu sehemu ngingine," alisema Mkola.

Naye Bertha Mpongole, mkazi wa Kata ya Mwasanga, alisema hakuna jitihada zozote zinazofanywa na serikali katika kuwaunga mkono hali inayosababisha wajione sio sehemu ya jamii kwa sababu hata ujenzi wa zahanati walitumia nguvu kazi zao pekee.

Akizungumzia changamoto hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye alifanya ziara ndani ya kata hizo na kusikiliza kero za wananchi alitoa maagizo kwa serikali kuhakikisha ujenzi wa vituo vya afya na zahanati unakamilika kwa wakati ili wananchi waanze kupata huduma.

Alisema wananchi wanapaswa kuwabana madiwani wao kwa kuwa ndio wawakilishi kwenye vikao vya Baraza la Madiwani ambako hupitisha bajeti kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Pia alisema madiwani wa kata za Tembela na Mwasanga wanapaswa kutambua vipaumbele vya wananchi wao na kuvipigia chapuo badala ya kuangalia maslahi yao binafsi wakati walichaguliwa ili kuwatumikia wananchi.

"Kata za Tembela na Mwasanga zina jumla ya wakazi 600 idadi ambayo ni kubwa inapaswa kuwa na huduma zote muhimu za kijamii nashangaa kuona hakuna lolote lililofanyika kuhusua afya, nawaomba madiwani watumikieni wananchi kama mlivyoahidi," alisema Chalamila.





# BMH kufikisha huduma za kibingwa vijijini

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KUTOKANA na maeneo ya vijijini kukabiliwa na ukosefu wa huduma za afya za kibingwa, Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) imepata magari matatu ili kusaidia kutoa huduma hiyo, kupitia mpango wake wa huduma mkoba kwa maeneo ya vijijini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema magari hayo yana thamani ya zaidi ya Sh. milioni 335.145 ambayo yataisaidia hospitali hiyo kutoa huduma za afya na kuwezesha mpango kutoa huduma kwa jamii ya Watanzania walioko vijijini.

Alisema, magari hayo yatasaidia katika utekelezaji wa suala zima la uchangiaji damu wa hospitali hiyo ambao utaanza baada ya kukamilika kwa ujenzi wa benki ya damu mapema mwaka ujao.

"Katika kuendelea kuimarisha huduma katika hospitali yetu tuko katika mchakato wa kujenga benki ya damu ambayo inatarajia kukamilika mapema mwakani, hivyo kupatikana kwa magari haya kutatusaidia katika utekelezaji wa mpango wa kuchangia damu," alisema.

Dk. Chandika aliongeza magari hayo yataiwezesha BMH kwenda shuleni na katika taasisi mbalimbali ili kuhamasisha wananchi na umma wa Watanzania kujitolea damu ambayo itahifadhiwa kwenye benki ya damu ya hospitali.

Alisema ukusanyaji wa damu utakaofanywa na hospitali hiyo utasaidia katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa damu katika mikoa ya kanda ya kati.

"Kumekuwapo na ongezeko la mahitaji ya damu katika mikoa ya Kanda ya Kati kwa sababu ya ongezeko la watu katika Mkoa wa Dodoma na benki ya damu ya Hospitali ya Mkoa (General) haiwezi kukidhi mahitaji. Benki yetu ya damu itasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa damu," aliongeza.

Alisema ujenzi wa benki ya damu katika hospitali hiyo ambayo kwa sasa iko katika hatua za mwisho, utakuwa na umuhimu zaidi wakati wa kuanza utoaji wa huduma ya kupandikiza uboho inayotarajia kuanza kutolewa hospitalini hapo mwakani.

Dk. Chandika alitumia fursa hiyo kuishukuru serikali kuwezesha hospitali hiyo kupata magari hayo, huku akiwataka wafanyakazi wa hospitali hiyo kutunza ili yatumike kwa muda mrefu jambo ambalo litasaidia kutimiza wajibu wa hospitali wa kutoa huduma za afya kwa ufanisi.



Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), Wilaya ya Chamwino, Idda Siriwa, akitoa elimu kwa watu wenye ulemavu jinsi ya kuepukana na upokeaji na utoaji rushwa katika kipindi hiki cha uchaguzi wa serikali za mitaa na vitongoji, wakati wa mafunzo ya ujasiriamali kwa makundi maalum ya walemavu yaliyofanyika kijijini Buigiri wilayani humo, mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yaweka bayana mikakati yake kwenye lishe

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imejipanga kuweka kipaumbele katika kukabiliana na tatizo la utapiamlo na udumavu nchini kwa makundi maalum kama wazee, watoto na kinamama wanajawazito.

Hayo yalibainishwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Uratibu na Uwekezaj, Dorothy Mwaluko, alipokuwa akifunga mkutano wa wadau wa lishe kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama.

Alisema hatua hiyo itasaidia azma ya serikali kuondoa changamoto ya utapiamlo na udumavu hapa nchini.

Aidha, aliwataka maofisa lishe nchini kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia lishe bora ili kuondoa changamoto ya utapiamlo na udumavu katika jamii.

Alieleza kuwa maofisa lishe wanapaswa kuongeza juhudi katika kutoa elimu kwa kushirikiana na wadau kuhusu umuhimu wa lishe bora.

"Kipaumbele lazima kiwekwe katika makundi maalum kama wazee, watoto, kinamama wanajawazito na wale wanaonyonyesha ili kufanikisha azma ya serikali kuondoa changamoto ya utapiamlo na udumavu hapa nchini," alisema Mwaluko.

Hata hivyo, alisisitiza matumizi ya sanaa, vyombo vya habari na viongozi wa kisiasa wakiwamo wabunge katika kuelimisha umma kuhusu athari za utapimlo na udumavu hapa nchini.

"Serikali itawashirikisha wabunge vinara wa masuala ya lishe katika kupiga vita utapiamlo hapa nchini," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Zainab Chaula, alisema kuwa maazimio ya kikao hicho yanapaswa kutoa majawabu yatakayowezesha kuondokana na utapiamlo na udumavu hapa nchini.

Aliongeza kuwa serikali imeweka mazingira wezeshi ya kufanya kazi na wadau katika kukabiliana na changamoto ya utapiamlo na udumavu katika maeneo yote nchini ili kujenga jamii yenye afya bora.

Aidha, Dk. Chaula aliwataka washiriki wa mkutano huo kuhakikisha kuwa kila mmoja anakuwa sehemu ya mapambano dhidi ya utapiamlo na udumavu hapa nchini ili kujenga jamii yenye afya bora hasa wakati huu Taifa linapojenga uchumi wa viwanda na kutekeleza azma ya kuleta ustawi kwa wananchi.

# Wanawake sasa wapewa mbinu ya fursa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WANAWAKE wametakiwa kutumia fursa zilizopo ili kujikwamua kiuchumi ili kusaidia kufikia azma ya uchumi wa kati ifikapo 2025.

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya serikali ya Purple Planet, Hilda Kisoka, alipokuwa akifungua mafunzo ya 'women in action' kwa wanawake 150 wa Jiji la Dodoma.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kutaka kumuinua na kumhamasisha mwanamke ili kushiriki katika ujenzi wa uchumi kupitia fursa mbalimbali ambazo serikali ya awamu ya tano inazitoa.

Kisoka alisema hivi sasa serikali ya awamu ya tano inasisitiza suala zima la viwanda hivyo wanawake wanapaswa kuamka ili kuanzisha viwanda vidogo kupitia ujasiriamali mbalimbali wanaoufanya.

Alisema taasisi hiyo inalenga kuwafikia wanawake 2,000 kutoka kanda tano hapa nchini ili kuhakikisha wanawake wanainuka na kuchangamkia fursa za maendeleo.

"Semina hii ni muhimu sana kushiriki wanawake kwa sababu inafundisha uthubutu kwa kuwa imekutanisha wanawake waliofanikiwa na wanaohitaji kutimiza ndoto zao," alisema.

Alifafanua ili kufikia malengo endelevu wanapaswa kuweka jitihada katika kazi wanazofanya na kuleta usawa wa kijinsia kwa jamii.

Naye Mkurugenzi wa Unique & Bakery, Sella Mkisi ambaye ni Mwenyekiti wa Purple Planet jijini Dodoma, alisema lengo la semina hiyo ni pamoja na kuwainua wanawake wenye ndoto zao kwa kubadilishana mawazo na kupeana mbinu za uthubutu.

Alisema wanawake wengi wanaweza lakini wamekuwa wakihofia kujitokeza.

Alieleza kutokana na hilo Purple Planet imeandaa semina hiyo kwa ajili ya kuwakutanisha wanawake ambao wapo katika makundi matatu kwa pamoja ili kuwasaidia wale wanaoanza kutimiza ndogo zao waweze kufika.

Kwa upande wake, Christina Mpete alisema semina hiyo iwe chachu ya wanawake kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

**"Semina hii ni muhimu sana kushiriki wanawake kwa sababu inafundisha uthubutu kwa kuwa imekutanisha wanawake waliofanikiwa na wanaohitaji kutimiza ndoto zao," alisema.**



# Waliorejea shule kwa kupata ujauzito wafuzu vizuri

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JUMLA ya wanafunzi 29 kati ya 99 waliopata ujauzito wakiwa chini ya umri wa miaka 18 kuanzia mwaka 2005 hadi 2010 katika Wilaya ya Kati Unguja wamefanikiwa kuendelea na masomo yao na kumaliza elimu ya lazima.

Wakitoa ripoti ya uhakiki wa wanafunzi waliobeba ujauzito na kurejeshwa shule kwa Wilaya ya Kati Unguja, maofisa sheria ofisi ya Mrajis wa Elimu, Msellem Mzee Mikidadi na Zuwena Mataka Hafidh, wamesema baadhi ya wanafunzi hao wamefaulu vizuri masomo yao hadi kidato cha sita.

Walisema katika ripoti yao wamebaini kuwa kati ya wanafunzi 29 waliorejea shule 15 wamemaliza kidato cha pili, 23 wamemaliza kidato cha nne, wawili kidato cha sita, wawili wamemaliza stashahada, mmoja amemaliza shahada ya kwanza na tisa wameajiriwa na kujiajiri wenyewe.

Walieleza kuwa ripoti yao pia imebaini sababu zilizowafanya wanafunzi hao kupata ujauzito ni baadhi yao kuwa na ushirikiano mdogo baina ya walimu na wazazi, umbali wa makazi ya wanafunzi na shule, ushiriki wa mapenzi katika umri mdogo na matumizi mabaya ya simu.

Akifungua mkutano huo wa uwasilishaji wa ripoti, Mrajis wa Elimu na Katibu wa Baraza la Elimu Zanzibar wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Siajabu Suleiman Pandu, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanya marekebisho katika baadhi ya vipengele vya Sheria ya Elimu, mwanafunzi anayepata ujauzito aliye chini ya umri wa miaka 18, aendelee na masomo ili apate haki yake ya elimu ya lazima.

Alisema kuwa mwanzo wa utekelezaji wa sheria hiyo ulikuwa mgumu kutokana na baadhi ya wanafunzi wanaopata ujauzito huwa hawaendelei na masomo wakati sheria inawaruhusu kuendelea.

Alieleza kuwa watoto hao hushindwa kuendelea na masomo kutokana na unyanyapaa kwa jamii na baadhi ya wazazi huwafungisha ndoa baada ya kupata ujauzito.

Kwa upande wao washiriki wa mkutano huo walishauri kuwapo adhabu kali kwa wahusika wote ili kupunguza vitendo hivyo vya mimba za mapema, kufanywa kwa uchunguzi wa afya kwa wanafunzi mara kwa mara, pamoja na kuondoa usiri hasa katika kutekelezwa sheria za vitendo hivyo.

Kwa upande wao wasichana hao waliopata ujauzito waliomba serikali kuwasaidia kupata ajira kwa kuwa baadhi yao wameshamaliza masomo na wamepata vyeti vizuri, lakini hawana ajira.

"Tunaishukuru serikali kwa kuturuhusu kuendelea na masomo shuleni baada ya kupata ujauzito na sikukata tamaa nilendelea na masomo na sasa nimemaliza kidato cha sita nimewashinda hao waliokuwa hawajapata ujauzito ambao baadhi yao hawakufaulu," alisema msichana huyo (jina linahifadhiwa).



Mkazi wa kisiwa cha Tumbatu, Kaskazini Unguja, Jabu Omar Kheir, akizungumza katika mkutano wa utoaji elimu kuhusu umiliki wa ardhi ulioandaliwa na Tamwa Zanzibar, kisiwani humo juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wafanyakazi wahimizwa uadilifu kujiepusha rushwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema iwapo wafanyakazi na watumishi wa umma watazingatia uadilifu katika majukumu yao ya kuhudumia umma, watajiepusha na rushwa.

Akizungumza katika Baraza la Wawakilishi, alisema vitendo vinayoambatana na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi kamwe haviwezi kuvumilika mahali popote pale iwe ndani au nje ya nchi.

Alisema wapo baadhi ya watendaji na watumishi wa umma wasio waaminifu wakiendelea kuhujumu uchumi kwa kupokea rushwa na kuisababishia serikali hasara au wananchi wake kuwaweka katika mazingira magumu wakati wanapohitaji huduma za kijamii.

Alisema zipo tuhuma za uhujumu uchumi na upokeaji rushwa zipatazo 108 ambazo upelelezi wake haujakamilika zilizoripotiwa katika taasisi zinazopambana na rushwa hadi kufikia mwaka 2018.

Balozi Iddi alitoa maelekezo kwa taasisi zinazohusika na ufuatiliaji wa masuala ya rushwa na uhujumu uchumi kisheria kuondoa usiri na kuharakisha upelelezi wake ili wahusika wafikishwe katika vyombo vya sheria ili haki ichukue mkondo wake.

Alisema vitendo vya rushwa kwa upande mwingine vimekuwa vikichangia ongezeko kubwa la udhalilishaji kutokana na kipato kikubwa kinachompa kiburi na jeuri mhusika wa vitendo vya upokeaji rushwa.

Pia alisema udhalilishaji kwa sasa umekuwa tishio nchini na kutoa sura mbaya inayoashiria waathirika kupata kipigo, kutelekezwa kwa watoto wachanga, talaka zisizo na utaratibu pamoja na watoto wenye umri mdogo kushirikishwa kwenye biashara zikiwamo za dawa za kulevya.

Alisema vitendo hivyo vinakwenda kinyume na mila, silka, desturi na utamaduni wa taifa, hivyo aliwakumbusha wazee, jamii na viongozi wa ngazi tofauti wakiwamo wananchi kusaidia kupinga masuala hayo yanayodhalilisha jamii na taifa.

"Serikali inavisisitiza vyombo vyote vinavyohusika pamoja na wadau wote kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, Zanzibar bila ya unyanyasaji na udhalilishaji inawezekana," alisisitiza Balozi Iddi.

# Tumbatu waomba huduma usajili ardhi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANANCHI wa kisiwa cha Tumbatu wameomba kusogezewa karibu huduma za usajili wa ardhi ili kufanya utaratibu wa kusajili mali zao na kupata hatimiliki.

Wakizungumza katika mkutano unaohusu umiliki wa ardhi kwa wanawake huko Tumbatu Kaskazini Unguja, walisema kuwa huduma hizo zitakaposogezwa katika kisiwa hicho itawasaidia kusajili ardhi.

Walisema wananchi wengi wa kisiwa hicho wanamiliki ardhi, lakini hawana hati inayowatambulisha umiliki halali wa ardhi hizo.

Jabu Omar Kheir, ambaye ni miongoni mwa wananchi wa kisiwa hicho aliiomba serikali kuwasogezea huduma hizo katika ofisi za wilaya ndogo Tumbatu ili kuepuka usumbufu wa kufuata huduma hizo mjini katika Idara ya Ardhi.

Alisema jiografia ya kisiwa hicho kimezungukwa na bahari, hivyo inakua vigumu kufuata huduma nje ya kisiwa hicho.

Naye Ofisa Mwandamizi kutoka Idara ya Ardhi, Haji Mrisho, aliwataka wananchi wa kisiwa hicho kutafuta hatimiliki ya ardhi au nyumba wanazomiliki ili kuwa na vielelezo vinavyostahiki.

Alisema, kufanya hivyo kutawawezesha kuepukana na migogoro ya ardhi.

"Unapokuwa na hatimiliki ya ardhi au nyumba unajihakikishia usalama wa mali unazomiliki na wala hakuna mtu ambaye atakuja kuwanyang'anya," alisema.

Kwa upande wake, mwanasheria kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), ofisi ya Zanzibar, Fatma Kwale, alisema Tamwa imekuwa ikitoa elimu ya umiliki wa ardhi hasa kwa wanawake baada ya kuona wanawake wengi wanadhulumiwa mali zao kutokana na kutokua na vielelezo stahiki.

Mkutano huo umeandaliwa na Tamwa, ofisi za Zanzibar.

**"Unapokuwa na hatimiliki ya ardhi au nyumba unajihakikishia usalama wa mali unazomiliki na wala hakuna mtu ambaye atakuja kuwanyang'anya," alisema.**

# Serikali yaipa Halotel maagizo muhimu

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imeitaka kampuni ya simu ya Halotel, kutumia mkongo wa taifa wa mawasiliano kupeleka mawasiliano nje ya nchi.

Taarifa ya Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, cha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam ilisema.

Iliongeza kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, ndiye aliyetoa maagizo hayo wakati wa ziara yake ya kukagua miundombinu na mwingiliano wa mawasiliano Kabanga mpakani mwa Tanzania na Burundi.

Nditiye alizuru eneo la maunganisho ya mkongo wa taifa wa mawasiliano ambalo linatumika kupeleka mawasiliano kutoka Tanzania kwenda nchi jirani, ilisema.

Akiwa kwenye maunganisho hayo, Nditiye alibaini kuwa kampuni ya simu ya Halotel imepeleka mawasiliano yake moja kwa moja kutoka Tanzania kwenda Burundi kwa kuunganisha jozi za mawasiliano za kampuni hiyo kwenye mfumo wa mkongo wa Burundi (Burundi Backbone System) badala ya kufanya maunganisho hayo kupitia Mkongo wa taifa wa mawasiliano (NICTBB)

"Nawaelekeza Halotel watumie mkongo wa taifa wa mawasiliano kupeleka mawasiliano nchi jirani ili kufuata utaratibu uliowekwa baina ya nchi moja na nyingine wa kuvusha mawasiliano yake kwenda nchi nyingine kwa kutumia maunganisho ya mkongo wa nchi moja kwenda maunganisho ya nchi nyingine badala ya kuunganisha mawasiliano kutoka kwenye kampuni husika kwenda nje moja kwa moja," alisema Nditiye.

Alifafanua kuwa Halotel hawaruhusiwi kufanya hivyo kwa kuwa wanakiuka utaratibu, tena wanaikosesha nchi mapato na inahatarisha usalama wa nchi kwa kuwa hakuna atakayeweza kufuatilia mawasiliano hayo upande wa pili kwenye nchi jirani.

Mhandisi wa Kampuni ya Simu (TTCL), Marwa Mwita, alipokea maelekezo ya Nditiye na kukiri kuwa hakuna kampuni ya mawasiliano ya simu mkononi inayoruhusiwa kuvusha mawasiliano ya kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine bila kupitia mkongo wa taifa wa nchi husika kama vile Burundi, Rwanda na Tanzania, NICTBB.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Michael Mntenjele alimwarifu Nditiye kuwa wilaya hiyo na viunga vyake vinahitaji mawasiliano ya uhakika na yasiyokuwa na msongamano ili kufanikisha suala la ulinzi na usalama wa taifa.

Nditiye amemweleza Mntenjele kuwa serikali imeielekeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kupitia umoja wa kampuni za simu za Jumuiya ya Afrika (EACO) kudhibiti mwingiliano wa mawasiliano mpakani na kukubaliana kuwa hamna mtandao wa nchi moja kuingia kwenye nchi nyingine ili kila nchi ipate mawasiliano ya nchini kwake.



Baadhi ya washiriki kutoka kampuni mbalimbali wakishiriki mashindano ya kukimbia na magunia katika bonanza lililoandaliwa na kampuni ya Bima ya AAR, kwa ajili ya kupima afya katika viwanja vya Posta Kijitonyama, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Shule binafsi zaomba ruzuku

Neema Sawaka, KAHAMA

WAMILIKI wa sekondari binafsi wametakiwa kuanzisha karakana katika shule zao, badala ya kuwaacha wanafunzi kusoma elimu ya ufundi kinadharia.

Agustino Kasase, mkufunzi kutoka Chuo cha Ualimu Butimba jijini Mwanza, ndiye aliyesema hayo juzi katika mahafali ya Sekondari ya Kwema mjini Kahama.

Aliongeza kuwa iwapo wanafunzi watamaliza shule wakiwa wana elimu, vitendo na nadharia, azma ya Rais John Magufuli ya Tanzania yenye viwanda itafanikiwa.

Alionya kuwa kusoma bila vitendo na mazoezi kunawakwamisha wanafunzi wanaomaliza shule wakiwa hawajui kujitegemea kwani wamekosa ujuzi wa vitendo.

Kasase alisema shule nyingi za sekondari kwa sasa zinatoa elimu kwa njia ya nadharia hali ambayo inafanya wanafunzi wakimaliza shule kukosa elimu ya kujitegemea na kusababisha kundi kubwa la wanafunzi kuhangaika kutafuta ajira.

Alisema sekondari za sasa zina wanafunzi waliomaliza shule, lakini hawawezi hata kushona kifungo cha shati la shule, wala kupika hali ambayo inapaswa kukemewa ili kuwanururu wanafunzi hao.

Kasase alisema suala la kuwa na karakana ni muhimu kwa wanafunzi wanapomaliza elimu ya sekondari watapata nafasi ya kujitegemea kwa urahisi hata wasipofaulu na kuendelea na elimu ya juu.

Mafunzo yatawawezesha kujiajiri katika sekta mbalimbali za kiufundi.

Kaimu Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Mji wa Kahama Stephen Cleophas, alisema Tanzania ya viwanda bila ya kuwa na wataalamu waliobobea haitafanikiwa.

Alisema kwa kuwatumia wanafunzi waliosoma katika shule zenye karakana taifa lina nafasi ya kusonga mbele.

Cleophas alisema kama shule za sekondari zitakuwa na karakana watoto wengi watakuwa na ujuzi wa kufanya kazi kutokana na kozi za kiufundi watakazofunzwa.

Mwalimu wa Taaluma wa Sekondari ya Kwema, Boniphace Sylvester, aliiomba serikali kutoa ruzuku kwa shule binafsi kwani mazingira ya ufundishaji yapo sawasawa na yale ya sekondari za serikali.

Alisema kuwa kama shule binafsi zitapata ruzuku zinaweza kunufaika kama walivyo wenzao waliopo katika sekondari za serikali.

Alieleza kuwa wakinufaika wanakuwa Watanzania watakaolitumia taifa katika mambo mbalimbali ya kukuza uchumi.

Jumla ya wanafunzi 146 walihitimu kidato cha nne katika Sekondari ya Kwema iliyopo Mjini Kahama, kati ya hao wavulana ni 96, huku wasichana wakiwa 50.

# Ushirika wajenga ghala, kujipatia milioni 120/-

Na Sabato Kasika

ILI kujiongezea mapato na kuinua uchumi na hali za wanachama wake ambao ni wakulima wa korosho, chama cha ushirika cha msingi Umoja, kimeanza ujenzi wa ghala lenye thamani ya Sh. milioni 640.

Chama cha Umoja kilichopo mjini Liwale mkoani Lindi, kinatarajia kukusanya kati ya Sh. milioni 80 hadi 120 kwa mwaka, ambazo ni ushuru kutoka kwa watu watakaolitumia kuhifadhi bidhaa zao.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Mpako, alisema wakati akizungumza na Nipashe kutoka Liwale jana na kueleza kuwa ujenzi wa ghala hilo kubwa la pili lenye thamani ya Sh. milioni 640, unalenga kuhifadhi tani 7,000 za korosho.

Alisema ujenzi wa nyumba hiyo ni kutimiza azma ya chama cha Umoja ya kujiongezea vitega uchumi vingi ili kuendelea kuendesha shughuli zake kiufanisi zaidi.

Mpako alisema ghala hilo litakapokamilika litawaongezea kipato zaidi ya kile walichokuwa wakikipata kutoka kwenye ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000.

"Ghala la sasa linatuingizia kati ya Sh. milioni 80 hadi 120 kwa mwaka, fedha hizo zinatokana na ushuru tunaopata kutoka kwa watu na vyama mbalimbali vya ushirika vinavyotunza mazao yao ndani ya ghala letu," alisema Mpako.

"Chama chetu kina vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwamo viti vya kukodisha, vibanda na nyumba, lakini sasa tunaongeza chanzo kingine cha mapato ambacho kina thamani kikubwa zaidi," alisema.

Mpako alisema, Umoja ni chama kikubwa chenye zaidi ya wanachama 1,000 wanaotunza mazao yako katika ghala la chama hicho na hata vyama vingine, hivyo wameona kuna haja ya kuongeza ghala jipya kubwa.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema, mwaka 2016 chama hicho kilinunua mizani kubwa yenye uwezo wa kupima tani 80 ikiwa ni kurahisisha shughuli za kupokea na kupima korosho na kuzihifadhi ghalani.

"Tulifanya hivyo ili kuwavutia zaidi wanunuzi wa koshoro na kuongeza ajira za muda kwa wakazi wa Liwale, hilo limefanikiwa na sasa tumegeukia ujenzi wa ghala kubwa zaidi kuliko lililopo," alisema.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa kuwapo kwa mizani hiyo pia ni miongoni mwa vyanzo wa mapato vya Umoja na kwamba kila mnada shughuli za kupima korosho zinafanyika kwa wingi.

## HABARI KIMATAIFA

# Hofu yatanda Rwanda raia kushambuliwa

**MUSANZE,** Rwanda

KUMEKUWA na wasiwasi miongoni mwa wananchi Wilaya ya Musanze Kaskazini mwa Rwanda baada ya washambuliaji kuwaua watu 14 wiki iliyopita.

"Hali ni mbaya, tunaogopa wanaweza kurudi na kuwaua waliotoroka. Hatulali tena", Isaac Niyonshuti, mfanyabiashara katika eneo la Kabazungu aliiambia BBC.

Washambuliaji hao - wanoashukiwa kuwa wafuasi wa Democratic Forces for the Liberation of Rwanda (FDLR) waliwishambulia vijiji kadhaa na mbuga ya taifa ya Volcanoes National Park - iliyo maarufu kwa sokwe wa milimani wanaopatikana huko.

Vikosi vya usalama nchini humo vilisema viliwaua waasi 19 na kuwakamata wafuasi watano katika opereshení iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita. Maofisa walisema kuwa waasi hao walitekeleza shabulio hilo siku ya Ijumaa wakati wakitafuta chakula kwenye vijiji hivyo.

Juzi Jumapili katika mazishi ya baadhi ya wahanga, mkazi mwingine wa Kabazungu alisema washambuliaji walikusanyika katika eneo hilo kabla ya kuanza kupora mali katika maduka ya biashara.

**Walirudi kwetu, wakaanza na mume wangu walimpiga kwa shoka dogo kichwani na pia watoto wangu wawili waliokuwa nyuma yake.**

Aliwaambia waombolezaji namna mumewe alivyouawa."Walirudi kwetu, wakaanza na mume wangu walimpiga kwa shoka dogo kichwani na pia watoto wangu wawili waliokuwa nyuma yake."

Nilipenya kati kati yao na nikakimbilia kichakani, Nilikaa usiku kucha huko na alfajiri nikarudi na kutafuta mwili wa mumewangu nikaupata uwanjani kwenye ua.

Aliongeza:"Niliarifiwa kwamba watoto wangu wangali hai lakini walijeruhiwa vibaya na walipelekwa hospitalini Kigali."

Maofisa waliwaambia wananchi hao kuwa wasiwe na wasiwasi kwasababu jeshi limerudisha amani. Baada ya shambulio hilo, bodi inayohusika na utalii nchini - Rwanda ilisema vikosi vya usalama vimerudisha utulivu na huduma za kitalii zitaendelea kama kawaida katika mbuga hiyo ya kitaifa.

Washambuliaji waliojihami walianzisha mashambulio kwa kutumia visu, mapanga na mawe katika wilaya hiyo ya Musanze. Idadi ya waliouawa ikiwa imetajwa kuwa watu wanane awali, maofisa sasa wanasema watu 14 waliuawa.



Mazishi ya wananchi waliouawa Rwanda. **PICHA: BBC**

Eneo hilo limelengwa na waasi wa Hutu nchini Rwanda walioendesha shughuli zao katika nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo katika siku za nyuma.

Waasi hao wanalijumuisha kundi la Democratic Forces for the Liberation of Rwanda (FDLR) ambalo viongozi wake wanatuhumiwa kuhusika katika mauaji ya kimbari nchini humo mnamo mwaka 1994, yaliyowahusu watu wa kabila la Tutsi na Wahutu wenye misimamo ya kadri. **BBC**

## Waandamana kunusuru dunia

**BERLIN,** Ujerumani

WANAHARAKATI wa vuguvugu la kupigania mazingira wameanza maandamano kwa kuzuia barabara kuu mjini Berlin Ujerumani na Amsterdam, Uholanzi, katika kile wanachokiita mfululizo wa maandamano ya kushinikiza sera mpya kuhusiana na mazingira.

Waandamanaji kama hao waliingia mitaani na kufunga barabara kuu huko nchini New Zealand na Australia.

Takriban watu 1,000 walifunga eneo la mzunguko wa taa za kuongozea magari la Grosser Stern, lililopo katika bustani ya Tiergarten katikati ya mji mkuu wa Ujerumani, Berlin, katika maandamano yaliyoanza juzi.

Aidha, washirika wa vuguvugu hilo la Extinction Rebellion pia walitengeneza makambi nje ya ofisi ya Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, wakiwasilisha hoja yao ya kutoridhishwa na sera kuelekea mabadiliko ya tabia nchi iliyoandaliwa mwezi uliopita na serikali yake, kabla ya kuanza kwa maandamano hayo makubwa.

Kwa mujibu wa vuguvugu hilo, maandamano hayo yatahusisha majiji 60 kote duniani.

Mjini Amsterdam, mamia ya waandamanaji wamezuia barabara kuu nje ya eneo maarufu la kitalii la Rijksmuseum, ambako pia wameweka mahema.

Maandamano kwenye mji huo yaliendelea licha ya zuio la jiji. Wanaharakati hao walipuuzia miito ya polisi ya kuwataka kuondoka na kwenda kwenye bustani iliyo karibu na eneo walikokusanyika.

Mwanaharakati Elle van Zeeland aliliambia shirika la utangazaji la Uholanzi NOS kwamba kundi hilo litaendelea kusalia hapo hadi serikali itakapokubaliana na madai yao. **DW**



Mpigakura 'akifanya kweli' katika sanduku la kupigia kura mjini Tunis, wakati wa uchaguzi wa wabunge Jumamosi Oktoba 6, 2019. **PICHA: REUTERS**

# Ennahda yaongoza matokeo Tunisia

**TUNIS,** Tunisia

MATOKEO ya awali ya uchaguzi wa bunge nchini Tunisia yanaonyesha kuwa chama cha Kiislamu chenye msimamo wa wastani, Ennahda kinatarajiwa kuibuka kuwa chama kikubwa katika bunge lijalo.

Muda mfupi baada ya vituo vya kupigia kura kufungwa jana jioni, chama cha Ennahda na kile cha kiliberali cha Heart of Tunisia vilijitangazia ushindi.

Lakini Ennahda kiliongoza kwa kupata asilimia 17.5 ya kura wakati cha Heart of Tunisia kikipata asilimia 15.6.

Hata hivyo, matokeo hayo bado ni pigo kwa Ennahda ambacho kinatetea nafasi yake ya sasa ya kuwa na viti vingi bungeni.

Tume ya uchaguzi ya Tunisia ilisema asilimia 41 ya watu walijitokeza kupiga kura katika uchaguzi huru wa tatu wa bunge .

Uchaguzi huo unakuja tangu kutokea kwa vuguvugu la mapinduzi mwaka 2011 lililouondoa madarakani utawala wa kimabavu na kuanzisha demokrasia na kuanza kutumika kwa katiba mpya mwaka 2014.

Wakati huohuo, Radio France International (RFI Kiswahili) inaripoti kuwa vyama viwili hasimu nchini Tunisia, Ennahdha na kile cha na mgombea urais anazuiliwa Nabil Karoui, vyote vinadai kuongoza katika uchaguzi wa wabunge uliofanyika juzi Jumapili nchini humo.

Uchunguzi uliochapishwa na taasisi tofauti nchini Tunisia hata hivyo umebaini kwamba chama cha Ennahdha chenye itikadi za Kiislam kimeshinda idadi kubwa ya viti, 40 kati ya 217, dhidi ya 33 hadi 35 kwa chama cha Bwana Karoui.

Vyama hivi viwili, ambavyo vilidai ushindi mbele ya waandishi wa habari bila kutoa takwimu, vilifutilia mbali muungano wowote wakati wa kampeni.

Matokeo ya awali yanatarajiwa kutangazwa kesho na mamlaka inayosimamia uchaguzi (ISIE), ilisema.

Ikiwa uchunguzi huu utathibitishwa, chama cha Ennahdha kitakuwa kimepoteza tena idadi ya viti na bunge jipya linaloonekana kugawanyika kati ya vyama vyenye nguvu na vile vyenye wafuasi wadogo.

Hata kama kutapatikana mshindi, itakuwa ngumu kwa mshindi huyu kukusanya idadi kubwa ya viti, tofauti na mwaka 2014, wakati bunge liligawanywa kati ya chama cha Nidda Tounes, na Ennahdha, ambavyo vilishikilia idadi kubwa ya viti na mara moja viliamua kuungana. **DW/RFI**

# Wambura wa kwanza

INATOKA UK. 2

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Wambura aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa aliyatenda makosa hayo kwa nyakati tofauti na pia ameiomba impe nafasi ya kushirikiana na jamii inayomzunguka.

Wiki iliyopita Wambura alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mhina kuwa, ameandika barua hiyo kufuatia agizo la msamaha uliotolewa na Rais, hivyo ameuomba upande wa mashtaka wafuatilie barua hiyo ili apate majibu kwa haraka.

Katika mashtaka hayo 17; shtaka moja ni la kughushi, shtaka moja la kutoa na kuwasilisha nyaraka za uongo; mashtaka 13 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na mashtaka mawili ya kutakatisha fedha.

Katika shtaka la kwanza ambalo ni la kughushi, mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo Julai 6, 2004, sehemu isiyojulikana ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

Siku hiyo inadaiwa, Wambura kwa nia ya kutapeli alitengeneza barua ya kughushi ambayo haina kumbukumbu namba akionyesha imeandikwa na E Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Jeck System, anadai kurejeshewa malipo ya mkopo wa USD 30,000 pamoja na riba aliyokuwa ameikopesha TFF.

Katika shtaka la kutoa na kuwasilisha nyaraka ya uongo, mshtakiwa anadaiwa alitoa barua iliyokuwa haina kumbukumbu namba ya Julai 6, 2004, akijifanya kwamba ni barua iliyoandikwa na E. Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Jeck System Ltd, akionyesha kuwa anadai mkopo wa USD 30,000 pamoja na riba waliokopeshwa TFF huku akijua kuwa siyo kweli.

Hata hivyo, kuanzia shtaka la tatu hadi la 15, mshtakiwa anadaiwa kujipatia kiasi cha zaidi Sh. milioni 95 kwa njia ya udanganyifu akidai kuwa fedha hizo ni sehemu ya malipo ya jumla ya kiasi cha fedha mbalimbali na riba kutoka kwa kampuni ya Jeck System Ltd huku akijua kuwa siyo kweli.

Pia katika mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, Wambura anadaiwa kutenda kosa hilo, Juni 17, 2015 huko katika ofisi za TFF, kuwa kwa njia ya udanganyifu, mshtakiwa alijipatia Sh. milioni 10 kutoka TFF kwa kuonyesha kuwa ni malipo ya USD 30,000 pamoja na riba kutoka kwenye kampuni hiyo ya Jeck System jambo ambalo siyo la kweli.

Katika shtaka la utakatishaji fedha, Wambura anadaiwa, kati ya Agosti 15 na Oktoba 21, 2014, makao makuu ya Shirikisho hilo, alijipatia Sh. milioni 25 kutoka TFF, huku akijua fedha hizo ni zao la kosa la kughushi.

Pia shtaka jingine la utakatishaji fedha haramu, mshtakiwa anadaiwa kati ya Machi 16 na Oktoba 21 2015, alijipatia Sh. 75,947,924 kutoka TFF wakati akijua fedha hizo siyo halali na zimetokana na shtaka la kughushi.

**Wakati huo huo**, Wakili Dk. Ringo Tenga na wenzake wameachiwa huru na kutakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 155 au kifungo cha mwaka mmoja jela.

Pia amewataka kulipa fidia ya Dola za Marekani milioni 3.748 na tayari wamelipa Dola 150,000. Mshtakiwa wa sita amehukumiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 30 pamoja kutaifishwa nyumba yake iliyopo Mikocheni. Fedha hizo zitalipwa ndani ya miezi sita.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi wa NMB wakipongezana baada ya kuzindua kampeni ya NMB mkononi mwako ambayo inamwezesha mteja kutumia simu yake kufanya miamala pasipo kwenda benki. Kampeni hiyo ilizinduliwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# TPA yaanika 'upigaji' wa magari mipakani

INATOKA UK. 2

"TPA ilimsamehe yule mama tozo zote kwa sababu ya uzandiki na uhuni tuliomfanyia, akalipa tozo za kawaida, hii imerudisha wafanyabiashara wa magari."

Pia, alisema alikwenda Jiji la Blantyre nchini Malawi ambako magari yanauzwa kama njugu na vijana wadogo wadogo wa jiji hilo huku fedha ambazo zilipaswa kuingia serikalini zikipotea.

"Pale Blantyre, Malawi nilishangaa wanaouza magari ni vijana wadogo wa miaka 20 hadi 21, tulikaa kwenye mawe tukafanya mkutano, walinieleza matatizo yao, mengi ni ya watendaji wa taasisi za serikali," alisema na kuongeza:

"Walinieleza matatizo yao makubwa, mengi ni ya ndani ya serikali ikiwamo huduma mbaya, ikiwamo rushwa kwenye mpaka wa Kasumuro, ambao ni Malawi na Tanzania."

Hapo mpakani, Kakoko alisema, walikuwa wanazuiwa kupita hadi asubuhi, lakini wakijichanga na kutoa rushwa wanaachiwa huku magari yakipotea na bima za kufoji ikiwamo usumbufu wa askari wa usalama barabarani.

"Ukiacha matatizo ya TPA ya watu kuiba vifaa vya magari, sababu nyingine zilifanya tukose biashara kiasi cha kufanya wafanyabiashara wa Zimbabwe kuhamia Bandari ya Msumbiji,"alisema.

Akizungumzia vikwazo vya usafirishaji wa magari barabarani, Kakonko alisema gari ni shehena hivyo haitakiwi kupakia mzigo wala abiria.

Alisema wafanyabiashara wa Uganda walimueleza kuwa dereva mmoja alikamatwa eneo la Tinde, mkoani Shinyanga baada ya bampa la mbele ya gari kukatika na kuamua kulitoa na kuliweka ndani ya gari, kitendo ambacho kilisababisha akamatwe na kuwekwa polisi kwa wiki moja.

"Alikaa polisi kwa wiki moja kuthibitisha kweli bampa ilikuwa ni sehemu ya gari au la, baada ya hapo hakutaka kupitisha magari yake huku, lakini niliongea nao na sasa wamerudi na kupandisha rekodi kutoka magari 93,000 hadi 132,035 kwa mwaka 2017/18 , huku mwaka huu yakiwa magari 159,639," alifafanua.

## Chadema yamjibu msajili

INATOKA UK. 2

la Polisi na kufanya marekebisho ya Katiba ya Chama kukidhi matakwa ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa nchini.

Oktoba Mosi, mwaka huu, ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, iliiandikia barua Chadema kutaka maelezo ya kwanini kisichukuliwe hatua kwa kushindwa kufanya uchaguzi wake mkuu.

Kupitia barua hiyo iliyotiwa saini na Sisty Nyahoza, ilisema uongozi wa Chadema umemaliza muda wake tangu Septemba 14, mwaka huu, hivyo anataka maelezo kwa nini Chadema isichukuliwe hatua za kisheria kwa kukiuka sheria hiyo, katiba na kanuni zao. Chadema ilipewa hadi jana saa 9:30 alasiri iwe imejibu barua hiyo.

Awali, Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji, alisema hawajavunja katiba na badala yake wameifuata baada ya kuahirisha uchaguzi wake mkuu kutokana na vikao vyao vya ngazi ya chini kuzuiwa na mamlaka na kwamba utafanyika ifikapo Desemba 18, mwaka huu.

## JPM awatolea uvivu 'mafataki'

INATOKA UK. 3

ni miaka 30 akishaenda gerezani ataelewa nini maana ya mimba. Hii ni aibu kubwa katika mkoa wenu," aliongeza.

Rais Magufuli pia aliwaomba viongozi wa dini nchini kutumia muda wao wanapokuwa katika mahubiri kuwafundisha watoto ili kuwanusuru na matukio ya kupata mimba wakiwa shuleni.

Wakati huohuo, Rais Magufuli aliwaruhusu wafanyabiashara wadogo mkoani humo kuendelea kufanya biashara zao katika soko la Mandela baada ya kuzuiwa na halmashauri tangu mwaka 2016.

"Haiwezekani tatizo tangu mwaka 2016 hadi leo halijatatuliwa. Sasa ninaamua hapa hapa, endeleeni kufanya biashara hapo. Haiwezekani mchicha na nyanya zikauzwa ghorofani. Na ninawaahidi nitawaletea Sh. milioni 200 ziwasaidie katika ujenzi wa soko. Na nyie halmashauri tafuteni sehemu nyingine ya kujenga soko lenu," alisema Rais Magufuli.

Kuhusu mradi wa maji, Rais Magufuli alisema kabla ya kujengwa, mkoa wa Rukwa ulikuwa unapata maji kwa asilimia 52 na sasa utapata asilimia 70. Naye Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alisema mradi huo utakuwa na uwezo wa kusambaza maji lita milioni 20.5 kwa siku wakati mahitaji ya maji mkoa wa Rukwa ni lita milioni 13.

Alisema serikali imetenga Sh. trilioni 3.98 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maji 547, miradi 468 ikiwa vijijini, miradi 79 nikiwa mijini.

Aidha, Rais Magufuli aliwaahidi wakazi wa Rukwa kuwa serikali imeshatenga Sh. bilioni 55.2 kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege mkoani humo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.

**VIWANJA/NYUMBA.** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Nyumba inauzwa Kaloleni Arusha ina frame za biashara,nyenye SQ 59 mil 800. Nyumba inauzwa Usariver ya bedroom4 mil 70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA CHETI



**Gloria Nyamahanga anatangaza kupotea kwa cheti cha Ualimu chenye index namba E539/033 kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Ifunda mwaka 2002.**

**Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**DAR/MSI/RB/345084/2019**

XXXXXX

### KUPOTEA KWA CHETI




**MARIAM EMANUEL KILAMIANI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0201/0043 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka katika Shule ya Sekondari ASHIRA GIRLS.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Polisi Taarifa:**
**SBR/IR/RB/2364/2016**

XXXXXX

### KUPOTEA KWA CHETI



**MWITA WAMBURA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato nne chenye index namba S0718/0045 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Nyansincha.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chcochocte cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**TAR/NYA/RB/304915/2019**

115446202


### HATI YA KIAPO

Mimi **HALIFANI SHABANI MAKAU** wa Mazimbweni Tanga, nikiwa na akili zangu timamu Hakimu/Wakili kama ifuatavyo:

(1)Kwamba mimi HALIFANI SHABANI MAKAU kiwanja no. 901 kitalu "D" Tanga mjini.
(2)Kwamba hati ya kumiliki kiwanja hicho imepotea Polisi kwa ajili ya kupewa loss report TAN/RO/3595 /2019
(3)Kwamba kwa kiapo hiki naomba ifahamike popote kuwa hati hiyo imepotea.

**UTHIBITISHO**
Nathibisha kwamba maelezo niliyoyaeleza hapo juu ni kweli tupu. Kadri nijuavyo kwa sharia za kiapo na kwa uthibitisho zaidi ninafika mbele ya Hakimu/Wakili nakutia sahihi yangu, nimetia hii leo tarehe 04/7/2019

MWAPAJI



215450502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**Mahakama ya Mwanzo ya Kawe**
**Madai nambari. 152/2019**

**Mdai HAPPYNESS PROCHES TARIMO**
**MDAIWA AMBIKILE EPHRAM MWANGATA**
**Kwa AMBIKILE EPHRAM MWANGATA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**KUITWA SHAURINI**

Hivyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya ………..Tarehe 15/10/2019 saa 2.00 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itadhibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshundwa /mmeshindwa .

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakamahii leo tarehe 7/10/2019

215449902

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 80 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late CHARLES SHAMBA MAHUNGUCHILA**
**And**
**In the matter of the Application for letters of Administration by SAIMON SHAMBA MAHUNGUCHILA**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections (if any) to the grant should be filed on or before day of 23rd October, 2019.

The will of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Date 30th this day of September 2019

215449002

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**FAMUEL EDWIN MKOJERA** anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI aina BAJAJI BOXER yenye namba za usajili MC924 BKU chassis na MD2A214GWD93537 Engine PFZWGD44045 Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DOD/DOD/RB/327074/2019

215449102

### KUPOTEA KWA KADI

**JULIUS KISAMAKI KALWILA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.149 ANK aina ya Toyota Mark II. Yeyote atakaiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya Polisi:
KAH/RB/TR/781/2019.

215449202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;190/2019**

Ombi la MUSSA JUMA RAMADHANI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MAUA MUSSA MAGONGA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/09/2019.

215449802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;200/2019**

Ombi la DANIEL DAVID TILILO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CHIKU MANENO CHIWANGA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 31/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/10/2019

215449702


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# VALVERDE ASHANGAA KADI NYEKUNDU YA DEMBELE




**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, aliachwa akiiponda kadi nyekundu aliyoonyeshwa Ousmane Dembele mwishoni mwa mchezo wa ushindi mnono dhidi ya Sevilla, akidai kwamba Mfaransa huyo hakumtamkia mwamuzi maneno ya kuudhi.

Dembele alitolewa nje kwa kadi nyekundu dakika mbili kabla ya mchezo kumalizika kwa kupinga kadi nyekundu aliyoonyesha 'dogo' wa Barcelona Ronald Araujo kwenye mchezo huo wa Jumapili walioshinda mabao 4-0.

Na Valverde amesema adhabu hiyo kwa Dembele haikuathiri kiwango chote cha mchezo huo.

Barca ilipata ushindi wao wa nne mfululizo kwenye mashindano yote, wakifunga mabao matatu ndani ya dakika nane za mwanzo, kabla ya nahodha, Lionel Messi kufunga la nne kipindi cha pili kwa mpira wa adhabu ndogo.

Valverde alikisifia kikosi chake kwa kiwango kizuri walichokionyesha wakati mabingwa hao mabao yake yakifungwa na Luis Suarez, Arturo Vidal, Dembele na Messi.

"Tulikuwa na wakati mzuri wa kucheza, na kiwango chetu ndicho kilichoamua matokeo," alisema Valverde akiwaambia waandishi wa habari.

"Matokeo ni muhimu, lakini hutakiwi kuwasamehe wapinzani wetu.

"Kadi nyekundu? Ni maamuzi ya mwamuzi. Kila mmoja ana mtazamo wake. Niliona mchezo mzuri kabisa.

"Haikuonekana kama ni tatizo la Araujo, lakini mara zote niliona kila kitu kipo sawa kwa timu yangu.

"Sijui ni kitu gani Dembele alimwambia mwamuzi, lakini sidhani kama ni sentensi ndefu, kwa sababu ni ngumu mno kumsikia akizungumza Kihispania."

# Guardiola: Liver mbona inakamatika

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amekiita kipigo cha Manchester City kutoka kwa Wolves "siku mbaya", lakini anaamini kikosi chake bado kinaweza kuikamata Liverpool licha ya kupitwa pointi nane kwenye mbio za ubingwa.

Mabao mawili ya Adama Traore ya kipindi cha pili yaliisaidia Wolves kuinyamazisha City kwa mabao 2-0 na kuiacha Liverpool ikitawala mbio za ubingwa huo katika hatua za awali kabisa kuelekea katika wiki ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Kwa mara ya kwanza msimu huu Liverpool wana nafasi ya kushinda taji la Ligi Kuu, kwani imeanza kwa kasi ya kutopoteza mchezo wowote wa ligi.

Lakini Guardiola bado ana imani na amesema: "Nawajua watu hawa. Bado wana nafasi na lolote linaweza kutokea.

"Tofauti ni kubwa, najua hilo. Kwa sababu nyingi, wao (Liverpool) hawajapoteza pointi. Si vizuri kufikiria timu moja ikiwa inaongoza kwa tofauti ya pointi nane. Ndio kwanza Oktoba hii.

"Kuna pointi nyingi. Lakini ni bora kufikiria kuhusu hilo. Ni bora kufikiria nini kinachofuata."

Man City imekuwa na wakati mgumu kwenye safu yake ya ulinzi ikiwa inamtegemea zaidi Fernandinho kutokana na mabeki wake kuwa majeruhi.

"Ni siku mbaya," alisema Guardiola.

"Kuna wakati inatokea. Tulianza vizuri na baadaye tukajikuta hatupo mchezoni na tukaruhusu mabao mawili."





# *Simeone: Washambuliaji wanatakiwa kuwa na njaa*

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amesifia safu ya ushambuliaji katika kikosi cha Atletico Madrid, lakini amesema inahitaji "kujituma zaidi na kuwa na njaa" ya kufunga mabao.

Atletico walilazimisha sare ya bila kufungana kwenye mchezo wake wa pili mfululizo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, wakati waliposhindwa kuipenya ngome ya ulinzi ya Real Valladolid kwenye mchezo huo uliopigwa dimba la Jose Zorrilla, juzi Jumapili na Simeone alibainisha kuwa kikosi chake kilianza taratibu.

'Rojiblancos' hao walionekana kuimarika katika kipindi cha pili, lakini nafasi nyingi walizozipata walishindwa kuzitumia, huku Angel Correa akikosa nafasi nyingi za kufunga.

Simeone alisifia safu ya ulinzi ya Valladolid, ambao walikosa penalti kipindi cha kwanza kwa kusema: "Wapinzani wetu walikuwa bora zaidi kipindi cha kwanza. Sisi hatukuwa na nafasi kabisa.

"Kipindi cha pili tulikuwa bora zaidi, lakini tulishindwa kutumia nafasi tulizozipata. Mara kadhaa tulikaribia kufunga mabao, lakini mambo yalikuwa magumu."

Alipoulizwa kuhusu safu yake ya ushambuliaji kuwa na matatizo ya kufunga, Simeone alisema: "Tulikuwa na nafasi na sasa washambuliaji wanatakiwa kujituma zaidi na kuwa na njaa ya kufunga.

"Niliwaona (Alvaro) Morata na (Diego) Costa wakiwa na nafasi, lakini wakashindwa kuitumia vizuri.

HABARI MICHEZO

# Tottenham ipo kwenye matatizo, asema Dier

**LONDON,** England

ERIC Dier amebainisha Tottenham wapo "kwenye matatizo" baada ya kuanza na mwanzo mbaya msimu huu.

Baada ya kipigo cha mabao 7-2 kutoka kwa Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Spurs walijikuta wakikumbana na kichapo kingine cha mabao 3-0 dhidi ya Brighton and Hove Albion kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

Mauricio Pochettino yupo kwenye presha huku Tottenham ikiwa nafasi ya tisa katika msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa ni miezi minne baada ya kufungwa kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Liverpool.

Dier amekubali kwamba, Spurs wanapitia kwenye wakati mgumu wakati huu wakiingia kwenye mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa baada ya kupoteza mechi nne kati ya tano zilizopita.

"Kwa uhakika tunapitia kwenye kipindi kigumu. Wanasema wakati mgumu ndio unakufanya uwe imara? Hapana," alisema Dier akinukuliwa na Gazeti la Mirror.

"Ukipoteza kama tulivyopoteza mechi mbili zilizopita, ni kawaida. Kwa upande wetu hiki ni kipindi kibaya zaidi, lakini tunatakiwa kushikamana ili kupita kwenye wakati huu.





# LUKAKU LAZIMA AJIFUE ZAIDI - CONTE

**MILAN,** Italia

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte amesema mshambuiaji wake, Romelu Lukaku anatakiwa kujifua zaidi ili mwili wake uwe na uwiano mzuri uwanjani.

Lukaku alikuwa kwenye kikosi cha Inter kilichoambulia kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus kwenye mchezo maarufu kama 'Derby d'Italia' uliopigwa dimba la San Siro, juzi Jumapili.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo akitokea Manchester United kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili la majira ya joto, alirudi kwenye kikosi baada ya kuukosa mchezo wa kipigo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona Jumatano iliyopita kutokana na matatizo ya misuli.

Alipoulizwa kuhusu Lukaku, Conte aliwaambia waandishi wa habari: "Romelu ni mchezaji ambaye ni lazima ajifue zaidi, kwa sababu mwili wake unahitaji mazoezi zaidi kupata uwiano mzuri, kujifua, kucheza na kuwa kwenye mwili mzuri.

"Huu ndio mwanzo wa msimu, alikuwa na matatizo ya mgongo na sasa anatakiwa kujifua zaidi.

"Lakini nafiriki alifanya kila kitu uwanjani, bahati mbaya kwamba kwenye mchezo dhidi ya Barcelona hatukuwa na Lukaku na ilikuwa muhimu kuwa naye. Na hatukuwa naye.

"Hata hivyo, Romelu alicheza kwa kujituma mno leo (juzi), alijaribu kwa ubora wake, na sasa naamini anaweza kumaliza tatizo hili dogo na kuwa fiti kwa asilimia 100."

Lukaku amefunga mabao matatu Inter tangu alipotua hapo akitokea United kwa ada ya euro milioni 80 Agosti mwaka huu.

# *Sarri: Ushindi Inter utaiimarisha Juve*

**TURIN,** Italia

MAUZIRIO Sarri ameonyesha kuridhishwa kwake na namna wachezaji wa Juventus walivyocheza na kuweza kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Inter Milan kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, juzi Jumapili.

Juve ilipata ushindi wa mechi tano mfululizo na kupata matokeo bora zaidi chini ya kocha wao mpya, Sarri na kuwa na mwanzo mzuri zaidi msimu huu.

Lautaro Martinez alisawazisha kwa penalti kwenye mchezo uliopigwa katika dimba la San Siro baada ya Paulo Dybala kuwaweka Juve mbele katika dakika ya nne, lakini Gonzalo Higuain akitokea benchi alifunga bao la ushindi zikiwa zimesalia dakika 10 mpira kumalizika.

Na sasa Juve imepaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu na kuwapiku wapinzani wao hao na Sarri amesema hawezi kujiona akiwa kwenye nafasi nzuri, kwani ligi ndio kwanza imeanza.

"Nafikiri bado tuna nafasi ya kujiimarisha zaidi. Bado tupo kwenye hatua za mwanzo kabisa," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Timu ina wachezaji wenye uwezo wao binafsi kwa mmoja mmoja na wanazidi kuimarika. Hii inamaanisha kwamba tunaweza kupata matokeo mazuri zaidi kwa siku zijazo, hata kama hatutacheza kwa kiwango cha juu cha asilimia 100.

"Tumekaa kileleni kwa sasa. Jambo muhimu ni kwamba tulicheza vizuri na kwa kujiamini dhidi ya timu ambayo imeshinda kila mchezo.

"Tulianza vizuri, hivyo hiyo ni ishara nzuri kwetu."


Matthijs de Ligt alizawadiwa penalti na kuisawazishia Inter, wakati beki huyo kijana wa Juve alipomfanyia faulo Nicolo Barella aneo la hatari.

Sarri amekubali kwamba, De Ligt amekuwa na wakati mgumu wa kuzoea soka la Italia tangu alipotua hapo akitokea kwa miamba wa Uholanzi, Ajax na amekuwa akicheza nafasi ya Giorgio Chiellini ambaye ni majeruhi na anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu.

"De Ligt hazungumzi vizuri Kiitaliano, lakini anazoea haraka staili ya soka letu, staili ya kujilinda na namna ya kucheza, ingawa amekuwa na wakati mgumu," alisema.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE GEA: KILA KITU UTD SASA VULULUVULULU

## Ni kipindi kibaya zaidi tangu niwepo hapa, samahani mashabiki, hatuwezi kufunga hata bao...

**NEWCASTLE,** England

KIPA David de Gea amesema "kila kitu ni vululuvululu (ovyo ovyo)" na Manchester United, kufuatia kushindwa tena kufurukuta kwenye Ligi Kuu England baada ya juzi kukubali kipigo kutoka kwa Newcastle United.

**De Gea, 28, hakujizuia katika tathmini yake kuhusu hali ya sasa ya Manchester United, akisema "kila kitu kinakwenda vululuvululu" na ipo katika kipindi kibaya tangu ajiunge na klabu hiyo.**

Kipa huyo alitoa tathmini yake kufuatia kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Newcastle United juzi, Jumapili, matokeo ambayo yanakiacha kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer kikishika nafasi ya 12, kikiwa na alama tisa tu kutokana na mechi nane.

De Gea alisisitiza kwa kutoa wito kwa Solskjaer kukiboresha huku akieleza kuwa katika mwenendo mbovu zaidi katika kipindi chake cha miaka minane hapo Manchester.

Alipoulizwa nini kilichoharibika, De Gea aliiambia Sky Sports: "Kila kitu. Nadhani mambo mengi yanahitaji kuboreshwa. Walikuwa timu bora leo.

"Sijui nini cha kusema, ukweli. Ninajaribu tu, kuendelea kupigana, kuendelea kujizatiti kila siku. Ni wakati mgumu kwetu, kipindi kigumu, ila sisi ni United na tunahitaji kuendelea kupigana."

Alipoulizwa kama ni kipindi kibovu zaidi tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2011, De Gea alisema: "Ndiyo. Pengine wakati mbaya zaidi, kipindi kibaya zaidi, tangu niwapo hapa. Njoo, hatuwezi kufunga bao hata moja katika michezo miwili. Samahani kwa mashabiki."

Kiungo Matty Longstaff, 19, alifunga bao hilo pekee lililoiua United ambayo ilitimiza mechi 11 bila ushindi ugenini katika mtanange huo uliopigwa Uwanja wa St James' Park, lakini ikiwa ni mechi ya kwanza kwa kinda huyo kuichezea Newcastle kwenye Ligi Kuu.

"Tutaendelea kupigana kwa uhakika, tutarejea, lakini kwa sasa tupo katika hali ngumu. Ni kipindi kigumu kwetu. Kipindi kigumu zaidi tangu nimekuwapo hapa. Sijui kwa nini ama nini kinatokea.

"Timu inapaswa kupiga hatua. Tunao majeruhi wengi lakini hatupaswi kusingizia hilo. Sisi ni Manchester United, tunahitaji kujifua kwa nguvu, kupigana na kushinda mechi."

## ZISIKUPITE

### SOLSKJAER KURITHIWA

KAMPUNI za kamari zimeongeza dau juu ya uwezekano wa Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer kutimuliwa kazi, hali hiyo ikitokana na kupokea kipigo dhidi ya Newcastle juzi, huku Kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino akipewa nafasi ya kutwaa mikoba yake. ***(Sun)***

### ATUMIWA MASHUSHUSHU

MANCHESTER United ilituma mashushushu wake kwenda kumtazama mshambuliaji wa Lyon, Moussa Dembele, 23, juzi Jumapili. ***(Mail)***

### EMERY KUMFUATA BOLY

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery anataka kutoa ofa kwa beki wa Wolves, Willy Boly, 28. Klabu hiyo inaweza kuongeza dau mara mbili ya pauni milioni 10 ilizolipa kwa Porto kwa beki huyo wa kati raia wa Muivory Coast kama atataka kutua Uwanja wa Emirates. ***(Sun)***

### KANTE AZUA VITA REAL, JUVE

REAL Madrid ipo tayari kutoa upinzani kwa Juventus kwa kiungo wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante, 28. Miamba hiyo ya La Liga inaweza kulipa ada ya takriban pauni milioni 70. ***(Sport, via Mail)***

### 'KANE ONDOKA SPURS'

BEKI wa zamani wa Liverpool, Glen Johnson amemtaka mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane, 26, kuondoka hapo Kaskazini mwa London na kutazama kujiunga na Manchester City. ***(Manchester Evening News)***

### DE BEEK BASI TENA UTD

MANCHESTER United imepoteza matamanio yake ya kumsajili kiungo wa Ajax, Donny van de Beek baada ya kutakiwa kulipa pauni milioni 35 kwa nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi. ***(Mirror)***

### KLOPP AHUSISHWA NA MADDISON

KOCHA Jurgen Klopp anaweza kujaribu kuisaka saini ya James Maddison, amesema kiungo wao wa zamani Steve McMahon. ***(Stadium Astro, via Express)***

### GIGGS AMSHAURI SOLSKJAER

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anahitaji kusajili wachezaji watano zaidi kabla ya kurejea katika kiwango chake, kwa mujibu wa kocha wa Wales na mkongwe wa Old Trafford, Ryan Giggs. ***(Sun)***

### GIAMPAOLO CHUPUCHUPU MILAN

AC Milan ilikuwa katika mpango wa kumtimua kocha Marco Giampaolo wakati wa mapumziko katika mchezo walioibuka na ushindi dhidi ya Geona. ***(SempreMilan)***

### AITAJA BIRMINGHAM

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Aston Villa, Gabriel Agbonlahor, ambaye ni mfungaji wa wakati wote kwenye Ligi Kuu katika klabu hiyo, amesema wapinzani wao Birmingham City, walijaribu kuitaka huduma yake wakati akiwa kinda. ***(Birmingham Live)***

### WATKINS ANUKIA SHEFFIELD

KOCHA wa Sheffield United, Chris Wilder anavutiwa na mshambuliaji wa Brentford, Ollie Watkins na itatoa takriban pauni milioni 15 kwa Muingereza huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Sun on Sunday)***

HABARI MICHEZO

## Taifa Stars kambini kuiwinda Rwanda

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha timu ya Taifa (Taifa Stars), kimeingia kambini jana tayari kuanza maandalizi ya mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Rwanda (Amavubi), unaotarajiwa kuchezwa Oktoba 12, mwaka huu jijini Kigali.

Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Juma Mgunda, alisema jana kuwa kikosi hicho kitaanza mazoezi rasmi leo, baada ya wachezaji wote waliopo hapa nchini kuripoti.

Mgunda alisema wamefurahishwa na muitikio wa nyota wote walioitwa katika kikosi hicho, na anaamini watakapoanza mazoezi, wataendelea kuona ushindani wa kuwania namba unaongezeka.

"Timu inaripoti leo (jana), na mazoezi yataanza kesho (leo), hivi sasa tutaamini kila mchezaji anajua jukumu lake, ni mchezo wa kirafiki, lakini ni muhimu sana kwetu," alisema Mgunda.

Taifa Stars inatarajia kutumia mchezo huo kujiandaa na mechi ya marudiano ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Sudan utakayochezwa Oktoba 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa El Merreikh Omdurman nchini humo baada ya ule wa awali kukubali kipigo cha bao 1-0 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

## Kocha Chuoni atoa neno Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kushuhudia timu yake ikishinda mechi mbili tu kati ya nne ilizocheza Ligi Kuu Zanzibar hadi sasa, Kocha wa timu ya Chuoni, Ramadhani Madundo, amesema bado anaimani timu hiyo itabadilika na kucheza vizuri na hatimaye kuvuna alama nyingi zaidi katika ligi hiyo inayoendelea visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema timu hiyo ina mapungufu madogo madogo ambayo yanaweza kurekebishika ikiwamo idara ya ushambuliaji pamoja na ulinzi jambo ambalo anapaswa kulifanyia kazi kabla ya ligi kuchanganya.

Alisema wachezaji wapo vizuri na wanajitahidi kupambana, lakini mpira hautabiriki, hivyo ni jukumu lake kama mwalimu kuhakikisha timu inabadilika kutokana na hali ya mchezo uwanjani.

Alisema kwa sasa anachokiangalia zaidi upande wa washambuliaji wake kutumia nafasi wanazozipata jambo ambalo linatakiwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

"Wachezaji wanajitahidi kucheza vizuri na kupambana, lakini bado tatizo lipo la kiufundi zaidi hususan katika kupachika mabao, tunapata nafasi lakini tunazitupa," alisema.

Chuoni tayari imeshuka dimbani mara nne ikitokea sare mchezo mmoja na kupoteza mmoja huku ikishinda mechi mbili.

# MCHENGA YANUKIA UBINGWA WA SPRITE BBALL KINGS 2019

**Na Sabato Kasika**

MCHENGA Bball Stars wameendeleza ushindi wa pili mfululizo katika fainali ya Sprite Bball Kings 2019 baada ya juzi, Jumapili kuichapa Tamaduni kwa jumla ya vikapu 104 kwa 89, hivyo endapo leo itashinda itatawazwa mabingwa kwa mara ya tatu mfululizo.

Mechi hiyo ambayo ni ya fainali ya mchezo wa pili ilichezwa kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa baada ya fainali ya kwanza iliyopigwa viwanja vya Don Bosco Ijumaa iliyopita, Mchenga Bball Stars kushinda kwa vikapu 122 kwa 121.

Mchenga Bball Stars kwa sasa inaongoza kwa mechi mbili mfululizo na iwapo itashinda katika fainali ya mchezo wa tatu unaofuata, itakuwa imejihakikishia ushindi kwa msimu wa tatu mfululizo.

**Msemaji wa mchezo huo, Goza Chuma alisema, fainali ya mchezo wa tatu itachezwa leo kwenye viwanja vya Don Bosco, na kwamba Tamaduni itajiuliza tena na iwapo itashindwa, basi Mchenga Bball Stars watakuwa mabingwa wa mashindano hayo.**

"Tamaduni wakishinda mechi hiyo, itabidi kuwe na fainali nyingine, kwani bingwa ni lazima ashinde mechi tatu mfulizo, hivyo kama Mchenga wataendeleza ubabe, basi ndio watakuwa mabingwa," alisema Chuma.

Alisema mashindano hayo ya mpira wa kikapu kwa wanaume ya Sprite Bball Kings yanaandaliwa na East Africa Television na East Africa Radio na kupewa nguvu na kinywaji cha Sprite.

Mashindano hayo yalianza rasmi Agosti mwaka huu kwa timu 42, katika hatua ya mchujo kisha 16-bora, robo fainali, nusu fainali na sasa yako kwenye fainali ikizikutanisha Mchenga Bball Stars na Tamaduni.

FALCAO HUYO....



Mshambuliaji wa Yanga, David Molinga 'Falcao', akimtoka mchezaji wa Coastal Union ya Tanga, Stanley Kenedy, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kaka: Dada alivyoshinda mil. 260/- za SportPesa*

**Na Mwandishi Wetu**

KAKA wa mshindi wa Jackpot ya SportPesa ya Sh. milioni 260. 3, Scolastika Ngwalueson, Edgar ametoa ushuhuda wa ushindi wa dada yake huyo baada ya kufanikiwa kushinda mamilioni hayo.

Edgar ambaye amekuwa akimfundisha dada yake namna ya kubashiri, amempongeza na kuwashauri Watanzania kuamini kuanzia ukweli wa mchezo huo baada ya nduguye huyo kushinda.

Scolastika ameweka rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kushinda Jackpot hiyo ikiwa ni siku chache baada ya washindi wawili kuchota jumla ya Sh. milioni 825 za Jackpot na kugawana Sh. milioni 412 kila mmoja.

Akieleza jinsi alivyoshinda alisema: "Mimi ndiye niliyekuwa namsaidia dada yangu kubashiri na SportPesa kabla ya kushinda mamilioni hayo na haitakuwa mara ya kwanza kwangu kumsaidia.

"Mara kadhaa alikuwa akibashiri kwa kuniomba nimsaidie kwa kutumia simu yake yeye mwenyewe na alikuwa akiniomba nimsaidie kucheza kutokana na uwezo wangu wa kuzifahamu timu mbalimbali.

"Kabla ya kumsaidia kucheza nilikuwa naangalia rekodi ya kila timu husika kabla ya kubashiri na ndivyo hivyo ilivyotokea kwa dada yangu kabla ya kushinda mamilioni hayo.

"Kwani niliangalia rekodi za kila timu katika mechi husika kabla ya kuweka ubashiri wangu na kufanikiwa ubashiri huo kwa dada yangu kushinda.

"Ninaamini baada ya ushindi huo wa mamilioni, maisha yake yataanza kubadilika hayatakuwa kama ya zamani na kikubwa ninamtaka atumie fedha hizo kwa vitu vya msingi."

**AWASHAURI WATANZANIA**

"Mimi ndiye shuhuda wa kwanza wa ushindi wa dada yangu na ukweli ni kwamba, SportPesa hawampendelei mtu yeyote na michezo yao inakuwa ya wazi.

"Unachotakiwa mtu ni kuweka utabiri wako mzuri tu na kwa usahihi, kama ukishinda basi haraka unapatiwa fedha zako na hilo nimelithibitisha baada ya dada yangu kushinda mamilioni hayo."

# Michezo

Jumanne Oktoba 8, 2019

Nipashe




De Gea: Kila kitu Utd sasa ni vululuvululu UKURASA 30

**BAO HILO...**




Mshambuliaji wa Barcelona, Luis Suarez, akibinjuka hewani mithili ya baiskeli miguu juu na kuifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 4-0 dhidi ya Sevilla kwenye mechi ya La Liga iliyopigwa Uwanja wa Camp Nou juzi. Anayejaribu kuzuia bila mafanikio ni beki wa kati wa Sevilla, Mreno Daniel Carrico. **HABARI UK. 28**

## Stars yachelewesha rungu Mkude Simba

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam, umesitisha kutoa uamuzi juu ya hatima ya kiungo wake, Jonas Mkude, imefahamika.

Mkude anakabiliwa na makosa ya utoro, ambayo yalisababisha akakosekana katika msafara wa timu hiyo uliokwenda mikoa ya Kanda ya Ziwa (Kagera na Mara), kwa ajili ya kucheza dhidi ya Kagera Sugar na Biashara United.

Taarifa zilizopatikana kutoka uongozi wa Simba zinaeleza kuwa, tayari Mkude alishafika kwa uongozi na kujitetea, pamoja na viongozi wa benchi la ufundi nao walitoa taarifa zao kuhusu kiungo huyo.

Chanzo chetu kimesema kuwa, uongozi ulitarajia kutoa uamuzi jana, lakini wakasimamisha mchakato huo kutokana na nyota huyo kuwa katika kambi ya timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inajiandaa na mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Rwanda.

"Suala la Mkude limesimama kwa muda kwa sababu ya kuitwa katika kikosi cha Stars, hukumu yake ilikuwa itolewe leo (jana) Jumatatu, lakini ameshajieleza na sisi viongozi wa timu, pia tulitoa taarifa kwa upande wetu, " kilisema chanzo chetu.

Wakati huo huo, kikosi cha mabingwa hao watetezi kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wake wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC utakaochezwa Oktoba 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

# Utata ulipo bao la Yanga vs Coastal

## ●●● Mshika kibendera namba mbili atajwa, huku sasa VAR...

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga, kwa mara ya kwanza msimu huu juzi waliandika ushindi wao wa kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union kwa bao pekee lililozua utata kwa wachezaji wa timu pinzani, mashabiki, wadau wa soka na wachambuzi wa mchezo huo nchini.

**Katika mechi hiyo ya tatu kwa Yanga msimu huu, iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, vijana hao wa Kocha Mwinyi Zahera, walipata bao lao dakika ya 51 kupitia kwa Abdulaziz Makame ambalo lilidumu kwa dakika zote 90 na kuifanya timu hiyo kushinda kwa bao 1-0.**

Hata hivyo, bao hilo lilizua utata mkubwa huku wengi wakidai mwamuzi wa kati na yule wa akiba hawakuwa makini na walilikubali kimakosa kwa sababu mpira ulikuwa haujavuka mstari wa golini.

**Bao lilivyofungwa**

Ulikuwa mpira wa kona uliopigwa na winga Mrisho Ngassa dakika ya 51 na kumkuta beki wa Yanga Ali Ali aliyeachia krosi iliyotua kichwani kwa Makame ambaye aliiunganisha langoni mwa Coastal Union, lakini ikamkuta mmoja wa mabeki wa timu hiyo na kuucheza kwa kichwa.

Hata hivyo, mwamuzi wa mchezo huo, Abubabar Mturo kutoka Mtwara aliamuru mpira kutengwa katikati ya dimba la Uhuru kwa kuwa lilikuwa ni bao halali kutokana na beki aliyeokoa kuucheza mpira huo ukiwa umezama kimyani.

Wachezaji wa Coastal Union walimlalamikia refa Mturo wakidai mpira uliokolewa kabla ya kuvuka mstari wa goli, jambo ambalo pia mashabiki wengi na wachambuzi wa soka waliamini hivyo na umeendelea kuwa mjadala mkubwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii.

**Utata ulipo**

Kwanza kabisa wachezaji wa Coastal, walisita kumbughudhi ipasavyo Makame kufuati mshika kibendera namba mbili, Credo Mbuya kunyosha kibendera juu kabla ya Makame kuunganisha golini kwa kichwa akiashiria mchezaji huyo alikuwa ameotea.

Hata hivyo, kabla ya Makame kuucheza kwa kichwa Mbuya alishusha kibendera chini baada ya kubaini kuwa langoni mwa Coastal Union kulikuwa na beki aliyerudi nyuma wakati kipa wao, Soud Abdallah alipokuwa mbele kuwania kudaka mpira, hivyo moja kwa moja hapakuwa na kuotea.

Pili kuhusu beki wa Coastal Union, kabla ya kuucheza mpira huo alikuwa kwenye mstari wa golini na kisha mpira ulipopigwa alirudi ndani ya goli na kuucheza, utata hapo unakuja kwamba akiucheza mpira mwili ulikuwa ndani ya goli lakini mpira ulikuwa haujavuka mstari.

Kutokana na ukweli kwamba kitendo kile kilikuwa cha haraka sana, kwa mujibu wa mchambuzi wa Azam TV, Ally Mayay, anasema: "Ni kweli wakati anaucheza mpira huo alikuwa katika mstari, lakini ili kuucheza mpira alirudisha kichwa ndani ili kuvuta kasi na wakati huo mpira ulishavuka mstari."

**Ni refa au mshika kibendera?**

Kutokana na eneo alilokuwa refa, Mturo ni wazi mshika kibendera namba mbili, Mbuya jicho lake ndilo lilikuwa sahihi kabisa kukubali ni bao ama si bao kwa kuwa alikuwa usawa wa mstari wa mwisho unaotoka moja kwa moja golini, hivyo kulikubali ama kulikataa yeye ni muhusika sahihi.

**VAR ni muhimu?**

Utata kama huu ndio uliochangia kuwapo kwa Teknolojia ya Msaada wa Video kwa Refa (VAR) kwa baadhi ya Ligi Kuu Ulaya na michuano ya kimataifa, hivyo kama ingekuwa inatumika Ligi Kuu Bara pasingekuwapo na sintofahamu hiyo.

**Nafasi ya Yanga, Coastal**

Kwa matokeo hayo Yanga iliyoshuka dimbani mara tatu inakwea hadi nafasi ya 12 kutoka mkiani kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 ikiongozwa na Simba iliyoko kileleni kutokana na kushinda mechi zake zote nne wakati Coastal Union yenyewe ipo nafasi ya 15.

Ligi hiyo kwa sasa imesimama kupisha Kalenda ya Fifa na itaendelea tena Oktoba 23, mwaka huu kwa michezo mbalimbali kupigwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >